Nipashe
Jumatatu Desemba 19, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581164
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US




UKURASA 13




**Udahili** kidato cha kwanza wawagawa wadau wa elimu



UKURASA 2

RIPOTI MAALUM

# Ilivyo mikataba ya bodaboda inavyowaachia vilio, simanzi

UKURASA 4





Madereva wa bodaboda wakiwa kazini. **PICHA: MAKTABA**

## Shimo la mgodi lilivyoua mtoto wa miaka 2

UKURASA 9



## CHADEMA yatangaza kuanza mikutano ya kisiasa nchi nzima

UKURASA 3

MICHEZO MAKATA AIANIKA RUVU SHOOTING UK.28 KATUNI UK.6



Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi na mkewe Mariam Mwinyi, wakipata maelezo kutoka kwa Mtumwa Rashid Khamis wa Kikundi cha Bopwe Vegetable & Fruit Product, alipotembelea maonesho ya wajasiriamali katika hafla ya ufungaji wa Kongamano la Sita la Kiswahili la Kimataifa Wete, Pemba jana. **PICHA: IKULU**

# Udahili kidato cha I wagawa wadau

**Na Jenipher Gilla**

UDAHILI wa wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2023 umewagawa wadau wa elimu katika makundi mawili ya wanaounga mkono utaratibu wa wanafunzi wa shule moja ya msingi kupelekwa shule moja ya sekondari na wengine kuupinga kwa madai una madhara kitabia na kisaikolojia.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wadau hao walisema ikiwa wanafunzi wa shule moja ya msingi kudahiliwa kwenye shule moja ya sekondari kuna uwezekano mkubwa wa kuhamisha tabia, kuzungumza kilugha zaidi na kushindwa kujifunza mambo mapya ya kupanua uelewa wao.

Mwalimu Gratian Mukoba alisema kuwapanga wanafunzi walewale shule moja ya sekondari haina afya kwa kuwa wanahitimu darasa la saba na kwenda elimu ya kiwango kingine wakiendeleza tabia zilezile.

"Kama miongoni mwao kuna wanafunzi walikuwa wanajua kuwaigiza walimu, wataendeleza kufanya hivyo hivyo, kama kuna wachekeshaji na watundu vilevile, tabia zitahama kutoka shule ya msingi kwenda sekondari, hata namna ya kutunza nidhamu itawawia ugumu walimu," alisema Mukoba ambaye aliwahi kuwa Rais wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT).

Alisema wanafunzi wanajuana na kama wana makundi yao, watayaendeleza, hivyo utaratibu wa kuwachanganya na wanafunzi kutoka maeneo mengine ulipaswa kuendelezwa.

Mtaalamu wa Saikolojia wa Taasisi ya Global Source Watch, Dismass Lyasa, alisema mtoto anahitaji kujichanganya na watu wa aina tofauti, ili kujifunza mambo mapya na kwenda na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, ulimwengu na utandawazi.

Alisema kuwaweka darasa moja wanafunzi wote wanaotoka eneo moja kunaongeza uwezekano wa kushindwa kufanya vizuri darasani kwa sababu ya kuzoeana kulikopitiliza, pia kuzungumza lugha za kikabila kutokana na mazingira wanayotoka, hali itakayowaondolea ari ya kujifunza.

Alisema mfumo huo utadumaza elimu, pia maendeleo ya nchi kwa ujumla na utajenga matabaka ya wasiojua kubaki hawajui na wanaojua kubaki na kujua kwao.

"Serikali iendelee na mpango wa zamani wa kuwachanganya wanafunzi kijinsia na hata mikoa na wilaya, ili kuwasaidia wanafunzi kubadilishana taarifa, pia kujifunza mila desturi na tamaduni nyinginezo.

"Wanafunzi wa eneo moja wakiwekwa darasa moja, hasa vijijini, wanaweza hata kuongea lugha za kwao badala ya ile inayohitajika darasani," alisema.

### KAULI YA SERIKALI

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Dk. Charles Msonde, alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo, alisema kitendo cha wanafunzi wa darasa moja kutoka shule moja ya msingi kupangwa shule moja ya sekondari kunatokana na mfumo maalum uliotengenezwa kufanya hivyo ili wanafunzi, hasa wa vijijini, watembee umbali mfupi kufuata elimu.

Alisema serikali ina shule za bweni 38 zinazochukua wanafunzi milioni 1.1 sawa na asilimia 0.3, huku asilimia 99.7 wakienda kwenye shule za kata ambazo kila shule inachukua wanafunzi kutoka shule kadhaa zilizoko kwenye eneo hilo.

"Mfumo ule unakuwa umeshapanga kuwa shule hii ya sekondari italishwa na shule hizi za msingi zilizo karibu, na lengo ni kutaka wanafunzi wawe na uwezo wa kutembea kwenda shule kwa urahisi.

"Ukiwapanga tu bora shule maana yake utajenga mazingira ambayo siyo rafiki kwa wanafunzi kufika shuleni.

"Ndiyo maana unaona wanafunzi wa shule moja wote wanakwenda Kisutu (mfano), ni kwa sababu hiyo Kisutu ndiyo shule iliyopangwa kuchukua wanafunzi kutoka shule hiyo ya msingi na nyingine zilizoko eneo hilo.

"Ikitokea wanafunzi wa shule hizo wakawa wengi, mfumo huo umetengenezwa kuwapeleka shule zilizo jirani," alifafanua.

Dk. Msonde alisema miaka ya nyuma wanafunzi walikuwa wanapangiwa shule za nje ya eneo lao kwa kuwa shule za sekondari zilikuwa chache, lakini kuwapo shule za kata kumetoa fursa ya wanafunzi wengi kupata elimu, hivyo wanapangiwa shule za karibu ili kuwarahishia huduma hiyo bila kujali wametoka shule zipi za msingi.

"Malengo yetu ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inamtaka kila mtoto atoke elimu ya msingi aende hadi kidato cha nne, na hii ni ya lazima. Sasa katika utekelezaji wa hii sera, tunamtengenezea mtoto mazingira mazuri.

"Unapompangia mtoto shule iliyoko mbali na makazi yake, unamtengenezea tabia za utoro kutokana na kutembea mwendo mrefu kila siku," alisema.

Alibainisha kuwa hayo ni maandalizi ya mfumo wa elimu wa miaka 10 wa 16423+ elimu kuanzia mwaka 2024, akisema mwanafunzi akimaliza darasa la sita, atapelekwa kuanza masomo ya sekondari kwenye shule iliyoko karibu kwa lengo la kuhakikisha watoto wote wanasoma hadi kidato cha nne.

Dk. Msonde alifafanua, akisema '1' ni elimu ya awali, '6' ni darasa la kwanza hadi la sita, '4' ni elimu ya sekondari ya chini ambayo ni kidato cha kwanza mpaka cha nne na watoto wanaosomea ufundi, maarifa ya jamii, '2' ni kidato cha tano na sita na watakaosomea mafunzo ya ufundi na maarifa ya jamii na '3 ni chuo kikuu.

Alisema kuwa siyo kila kata wanafunzi wa shule moja ya msingi wote watapelekwa shule moja ya sekondari, bali inatokana na eneo husika na shule zilizoko kwenye eneo hilo.

Alitolea mfano shule za vijijini ambako shule ya sekondari inajazwa na shule tano za msingi, hivyo shule hizo zikiwa na wanafunzi wachache, wote watakutana kwenye shule hiyo moja.

### WADAU ELIMU

Mwenyekiti wa Taifa wa Shirikisho la Wamiliki wa Shule na Vyuo Binafsi Tanzania (TAMONGSCO), Leonard Mao, alisema mfumo huo ni mzuri kwa kuwa unawapunguzia wanafunzi changamoto ya usafiri ingawa una shida kwa watoto kutoijua vizuri jiografia ya nchi.

"Mtoto akisoma eneo moja halafu hiyo miaka 10 asibahatike kwenda sekondari, ina maana eneo pekee atakalokuwa analifahamu ni hili alilozaliwa na kukulia.

"Lakini serikali ina nia njema katika hili, kwa sababu lengo ni kuhakikisha watoto wote wanapata elimu iliyo bora bila changamoto yoyote," alisema.

### UDAHILI ULIVYO

Katika kufuatilia udahili huo, Nipashe imebaini kuwa wahitimu wote 64 (wasichana 33) waliofaulu Mtihani wa Darasa la VII katika Shule ya Msingi Masunula wilayani Shinyanga mkoani Shinyanga, wamechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari ya Kata ya Usule.

Wanafunzi hao wanakwenda kuungana Usule na wenzao 43 (wasichana 29) kutoka shule jirani ya Sumbigu.

Udahili huo pia unaonyesha wahitimu wote 108 (wasichana 54) kutoka Shule ya Msingi Feza ya wilayani Kinondoni mkoani Dar es Salaam wamechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Kawe Ukwamani.

Vilevile, wahitimu wote 243 (wasichana 127) waliofaulu Mtihani wa Taifa wa Darasa la VII mwaka huu kutoka Shule ya Msingi Kimanzichana wilayani Mkuranga mkoani Pwani, wamechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Mkamba wilayani humo.

Ni hali iliyoshuhudiwa pia kwa wahitimu wote 77 waliofaulu mtihani huo kutoka Shule ya Msingi Bwiti wilayani Mkinga mkoani Tanga ambao wamepangwa kujiunga na Shule ya Sekondari Mavovo wilayani humo.

# CHADEMA yatangaza kuanza mikutano ya kisiasa

**Na Jenifer Gilla**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetangaza kuanzia Januari mwakani kitaendelea na mikutano ya hadhara nchi nzima hadi Rais Samia Suluhu Hassan atakapotoa kauli kuhusu suala hilo.

Hivi karibuni, Rais Samia ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), alisema ataendeleza nia na azma yake ya utamaduni wa kusimamia majadiliano ya kiungwana na vyama vya siasa ili kuimarisha misingi ya demokrasia, umoja na maridhiano ya kitaifa.

Alitahadharisha kuwa majadiliano hayaivui CCM dhamana waliyopewa ya kuwa chama tawala, bali yanawafanya wavute wengine (wapinzani) wakae na kukubaliana namna ya kuendesha siasa kwa ustaarabu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa CHADEMA mkoa wa Kinondoni, Henry Kileo, alisema uamuzi wa chama hicho unakuja siku chache baada ya Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, kutamka kuwa chama hicho hakitajitoa kwenye maridhiano na CCM.

Kileo, aliwaambia waandishi wa habari kuhusu kupokea agizo ya Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, kuwataka wabunge wote wa wananchi wa chama hicho warudi majimboni kwa ajili ya kujiandaa na operesheni ya chama itakayoanza Januari, 2023 ikiwamo kufanya mikutano ya hadhara.

"Tofauti na hapo hakuna atakayesimamisha mikutano, kwa sababu sisi sasa ndio tutakaokuwa tunavunja katiba kwa sababu ipo na inaturuhusu, halafu bado tunataka kubembeleza kutekeleza wajibu wetu, tumekaa kimya kwa muda mrefu sasa usije ukatafsiriwa kwamba ni uoga," alisema Kileo.

Alisema suala la kufanya maridhiano na serikali sio la mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mboye peke yake bali ni la wanachama wote kwa kuwa walipelekewa ajenda hiyo na kamati na Baraza Kuu likaridhia kuwa jambo hilo lifanyike kwa manufaa ya taifa.

"Kuna hulka au kasumba imezuka watu wanataka kugeuza jambo hili ni la Freeman, sio jambo la Freeman ni jambo la CHADEMA tumeridhia kwenye Baraza Kuu. Kamati Kuu ilitueletea tukaridhia. Tusimgeuzia mtu (Freeman) mshale 'as if' (kama) yeye analihitaji sana hili jambo, CHADEMA inalihitaji na CCM wanalihitaji," alisema.



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Nanyumbu mkoani Mtwara, Hassan Ismail, akitoa elimu ya namna ya kujikinga na ajali za barabarani kwa madereva wa pikipiki za abiria 30 baada ya madereva hao kupatiwa vifaa mbalimbali ikiwamo kofia ngumu jana wilayani Nanyumbu. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Rais Samia kufunga lango la handaki Bwawa la Nyerere

**Na Frank Monyo**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kufunga lango la handaki la mchepuko kwenye Bwawa la Umeme la Julius Nyerere Desemba 22, mwaka huu, ili kuruhusu maji yaanze kujaa.

Ufungaji huo unatarajiwa kushuhudiwa na wageni 2,300 kwenye eneo hilo la mradi, Watanzania 2,000 na ugeni wa watu 300 kutoka Misri ambao utaambatana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Nchi hiyo.

Wageni wengine ni Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, wakuu wa mikoa, mawaziri na makatibu wakuu wa wizara mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kwenye eneo la mradi huo ulioko Bonde la Mto Rufiji, Waziri wa Nishati, January Makamba alisema mpaka sasa ujenzi wa bwawa hilo umefikia asilimia 78.68 ambayo ni hatua ya awali ya kuanza kujaza maji, ikitarajiwa kuchukua misimu miwili ya mvua iliyo kamili.

"Wakati mradi unaanza kutekelezwa ili kujengwa tuta katikati ya mto, ni lazima maji yachepushwe kwa njia nyingine ili yaendelee mbele, yakupe nafasi ya sehemu kavu kujenga handaki hili lenye urefu wa mita 700 sawa na viwanja saba vya mpira wa miguu kwa jumla ya gharama zilizotumika Sh. bilioni 235," alisema.

Waziri January aliongeza kuwa mageti ya kuziba mchepusho yamewasili na yameshafungwa.

"Kutokana na umuhimu na ukubwa wa mradi huo na umuhimu wa mradi kitaifa, ishara ya mradi huu kwa malengo yetu na ndoto yetu kwa maendeleo na hatua hii ya kujaza maji kwenye bwawa, itazinduliwa na kushuhudiwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan tarehe 22, Desemba mwaka huu Alhamisi.

"Akifika kwenye mradi, atabonyeza kitufe ambacho kitashusha geti la kuziba handaki lililokuwa linachepusha maji, kwa tukio hilo maji yataanza kujaa kwenye bwawa," alisema January.

Alisema kuwa hatua hiyo inakwenda kujibu mijadala ya baadhi ya watu waliokuwa wakidhani kwamba mradi huo hautokamilika kwa muda uliopangwa lakini hata uwezekano wa kujaza maji kuwa shakani kutokana hali ya ukame inayoendelea.

"Kuna watu walikuwa wanauliza ninyi watu wa serikali, tena wengine wakasema ninyi watu wa CCM, kuna ukame ambao kila siku mnalalamika ambao ndiyo chanzo cha upungufu wa umeme inakuwaje tena mnajenga bwawa kuzalisha umeme kwa maji ambayo kila siku mnalalamika ukame, kwanini msiache na kufanya mambo mengine?" Alisema.

Akifafanua dhana hiyo ya kupoteza muda, January alisema kuna aina mbili za kuzalisha umeme kwa kutumia maji, hatua ya kwanza maji yanakuja kwenye mto na yanatiririka moja kwa moja kwenye mitambo, yanajengewa eneo la kukusanywa halafu yanaendesha mitambo, mfano Bwawa la Kihansi.

Alieleza namna nyingine ya miradi hiyo kuwa ni kujenga bwawa na kuyakusanya maji mengi halafu unayaingiza kwenye mitambo, unayazungusha na kuzalisha umeme, mfano Bwawa la Mtera.

"Sasa unapojenga bwawa na kujaza kama hivi, mvua hata isiponyesha kwa miaka mitatu na lisitokee tone hata moja, bado tuna uwezo wa kuzalisha umeme kwa sababu maji yale umeyahifadhi," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO, Maharage Chande, alisema bwawa hilo lina uwezo wa kuhifadhi lita bilioni 33.2 za maji na kama zikitumika na mitambo yote, itaweza kuendesha mitambo kwa kipindi cha mwaka mmoja.


**Abrasen & Co.®**
**Advocates and Legal Consultants**

**TANGAZO LA UUZWAJI WA VIWANJA VYA MAKAZI**

Kwa mamlaka na maelekezo tuliyopewa na kampuni ya **TATEPA PUBLIC LIMITED COMPANY,** tunatangaza uuzwaji wa viwanja 31 vilivyopimwa kwa matumizi ya makazi tu. Viwanja hivyo vinapatikana eneo la Kinyanambo A karibu na Shule ya Msingi Gangilonga – Mafinga Mjini, Mkoani Iringa. Bei inatofautiana kwa kila kiwanja kulingana na ukubwa wa kiwanja chenyewe.

**Kwa mawasiliano zaidi tafadhali piga simu nambari +255 764 464 524 au +255 716 389 942.**

**Imetolewa na; Essau Abraham Sengo, Esq.**
**Wakili.**
**Abrasen & Company Advocates,**
**P.O Box 3810, Mbeya – Tanzania.**
**NIC Investment Building, Ghorofa ya Pili.**

TATEPA

217197302



**Stakeholders consultation meeting for the Carbon Voluntary Project Activity "Protect the environment, use clean cookstoves!" under the "Green Tanzania Cookstoves Programme"**

OffgridSun in collaboration with Inuka Youth Development Organization develops a clean cooking project in Tanga Region called "Tunza Mazingira, tumia jiko banifu! – Protect the environment, use clean cookstoves!". The project is an activity (VPA) under the Gold Standard Programme of Activities (PoA) "Green Tanzania Cookstove Programme" implemented by OffgridSun with the goal is to improve livelihoods of local population and protect environment in Tanzania by distributing improved cookstoves across the country to reduce CO2 emission derived by the use of biomass fuel for domestic purposes. The programme is developed under the Gold Standard framework and seeks to obtain Verified Emissions Reductions (VER).

The project Tunza Mazingira, tumia jiko banifu is implemented in ten villages in Mazingara, Mkata and Kwachaga Wards within Handeni District, Tanga Region, for a total of about 10.000 households targeted.

OffgridSun is welcoming stakeholders to provide their feedback through the organization of a stakeholders' consultation meeting to gather suggestions. The meeting will be held in Mkata, Handeni District at Ukumbui Wa Halmashauri (VETA) on the **20th of January 2022 from 8.00 am to 13.00 pm time local time.**

Interested people are invited to participate by contacting the number below. Those who wish to send their feedback or to ask more information about the project, can contact OffgridSun by writing a mail to **projects@offgridsun.com** or calling the numbers **+255682701460 or +393516142230 (whatsapp).**

217199802

# Ilivyo mikataba ya bodaboda inavyowaachia vilio na simanzi

**Na Halfani Chusi**

BODABODA si jina geni masikioni mwa watu, wengi wao hutumia usafiri huo kama nyenzo muhimu ya kuwahi kufika mahali fulani.

Mbali na umuhimu huo, kwa sasa usafiri huo umekuwa nyenzo tegemezi kwenye ajira, vijana wengi wamejiajiri humo na wanaendesha familia zao kupitia kazi hiyo.

Shida inakuja pale bodaboda wengi wamekuwa wakipewa pikipiki kwa mikataba kandamizi, ambayo haipo kisheria, hivyo husababisha wengi wao kushindwa kumaliza mikataba na kumiliki pikipiki zao.

Kimsingi, usafiri huo mzizi wa jina lake ni jijini Kampala, Uganda ambako umekuwa ukitumika kwa zaidi ya miongo minne sasa, wasifu wote wa aina ya huduma hiyo inavyoendeshwa ni vilevile ilivyotawala nchini kwa sasa.

Umaarufu huo wa jijini Kampala, matumizi ya bodaboda yakahamia ng'ambo ya pili hadi mjini Bukoba, ambako kuna unasaba wa kushabihiana kwa mengi na jiji hilo la nchi jirani, hadi kufikia miaka ya 1990, ukawa umeteka umaarufu huo.

Baadaye kwenye miaka ya 2000 ndipo mvuto huo ukasambaa kitaifa, ukikolezwa na jijini Dar es Salaam, sasa ikichukua sura ya usafiri mkongwe kitaifa, mijini na vijijini, zaidi ukitawaliwa na pikipiki kutoka China.

Kundi kubwa la waliojiajiri humo wengi wao ni wahitimu wa vyuo mbalimbali ambao wanasotea humo wakisubiri ajira, hali iliyowavuta hata kinamama kujiajiri humo kwa ajili ya kusaka chochote kitu.

Si ajabu kwa maisha ya leo kumwona mwanamke akiendesha bodaboda, hii ni kutokana na vile wanavyoelezea wao kuwa biashara hiyo inalipa.

Malaki Malangisa, bodaboda wa maeneo ya Sinza wilayani Kinondoni, anasema bodaboda wamegawanyika kwenye makundi matatu ya wanaoendesha bodaboda za kwao wenyewe, wanaoendesha kwa mkataba na wale wanaoendesha kwa kupeleka hesabu ya siku (day worker).

"Utaratibu wa wale wanaoendesha kwa mkataba uko hivi; bosi anakwenda dukani kununua pikipiki, baada ya hapo anampa kijana ili amletee marejesho (hesabu) kwa muda watakaokubaliana.

"Kwa siku huwa ni Sh. 10,000, wengi wao kwa sasa kutokana na kupanda kwa bei ya pikipiki hawatoi mkataba wa mwaka mmoja, kama ilivyokuwa awali, wanatoa kwa mwaka mmoja na miezi miwili, yaani miezi 12 hadi 15," anasema.



Baadhi ya madereva bodaboda wakiwa kazini. **PICHA: MTANDAO**

### KINACHOWASIBU

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe mkoani Dar es Salaam umebaini mikataba mingi wanayopewa bodaboda ina ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Ajira na Uhusiano Mahala pa Kazi, hali inayofanya bodaboda wengi kushindwa kumaliza na hivyo kudhulumiwa haki zao.

Juhudi za Nipashe kubaini kuwapo hali hiyo zilianza pale waandishi wake walipomkuta dereva wa bodaboda maeneo ya Ubungo Liver Side, akiwa ameshikilia kofia ngumu (helment) akibugujikwa na machozi.

Kijana huyo aliyejitambulisha kwa jina la Madii Suleiman (27), mkazi wa Tegeta Nyuki wilayani Kinondoni, muda wote alishindwa kuongelea kwa ufasaha kusimulia mkasa wake, akitawaliwa na jaziba, machozi yakimlenga, analazimika kuliambia gazeti hili kilichosababisha pikipiki yake kuchukuliwa.

Anasema alikuwa na mkataba na bosi wa pikipiki walikubaliana kwa miezi 12 awe anapeleka kila siku Sh. 10,000 na gharama za matengenezo juu yake, baada ya mwaka pikipiki inakuwa yake lakini ghafla hali ilibadilika mwishoni.

"Nilikuwa na mkataba wa pikipiki, nimefanya kazi miezi 11 na siku saba, nilikuwa ninapeleka Sh. 10,000 kila siku, kwa wiki Sh. 70,000, nilishindwa kupeleka hesabu kwa wakati mwezi huu kwa sababu katika wiki ya kwanza kazi ilikuwa ngumu, nikapata Sh. 50,000 badala ya Sh. 70,000.

"Nikampigia simu kumweleza bosi wangu kama wiki hii nimekwama kidogo, bosi hakutaka kunielewa, akaniuliza 'mkataba wetu mimi na wewe unasemaje?' Nikamjibu unasema 'ukichelewesha hesabu kwa muda wa siku mbili unapokonywa pikipiki', akaniambia 'ninakupa leo na kesho, hayo mambo hujapata mimi sihusiki nayo'.

"Basi nikaendelea kupambana, kazi iliendelea kuwa ngumu mpaka siku mbili hizo zinafika nikawa sijatimiza ile Sh. 20,000 iliyobaki, nilikuwa nimepata Sh. 10,000 katika ile 20,000 iliyokuwa imebaki, ghafla akaja yeye na ndugu yake wakanipokonya pikipiki huku zikiwa zimebaki siku 21 kumalizana naye ili iwe mali yangu," anasimulia kijana Suleiman.

Kimahesabu kijana huyo amepeleka kwa mmiliki huyo wa pikipiki Sh. milioni 3.39 huku ikiwa imesalia Sh. 210,000 pikipiki iwe mali yake kulingana na makubaliano ya mkataba wao.

Kijana Suleiman anasema pikipiki hiyo ilinunuliwa kwa Sh. milioni 2.4 na kimahesabu hapo, mpaka bosi anampokonya, alikuwa tayari ameshapata faida ya Sh. 990,000.

Nipashe inafunga safari hadi maeneo ya Tabata Mwananchi, nyumbani kwa bosi wa kijana huyo, Martini Malolela, anayekiri kilichonenwa na aliyekuwa mfanyakazi wake huyo.

"Ni kweli nilikuwa na mkataba naye (Suleiman), tulikubaliana kwa mwaka mmoja lakini yeye ndiye aliyeshindwa kwa mujibu ya makubaliano ya mkataba wetu. Mkataba wetu ulikuwa unasema katika wiki moja akichelewesha hesabu siku mbili, amevunja mkataba, mimi hapo nina rukhsa ya kuchukua chombo changu.

"Alikuwa hajawahi kuchelewa, ni wiki hiyo ya mwezi wa mwisho ambayo alifanya kosa hilo. Mimi huwa sipendi masihara katika kazi. Hiyo pikipiki tayari nimeshampa mkataba mtu mwingine, yeye ndiye kavunja mkataba, siyo mimi!" Anasema Malolela na kukiri hapakuwa na mwanasheria yeyote katika kuingia mkataba huo uliovunjwa.

Kilichomsibu kijana Suleiman kinatajwa kuwakumba vijana wengi waliojitosa kwenye biashara ya usafiri wa bodaboda.

Malaki Malangisa, bodaboda maeneo ya Sinza wilayani Kinondoni, anasema mikataba mingi wanayopewa ina upungufu mwingi kisheria, ikimjali zaidi mwajiri kuliko mwajiriwa.

"Mkataba wangu hauna sehemu inayosema nikiugua, ninatakiwa nipumzike kupeleka hesabu. Kwa hiyo, hapa ninaomba Mungu nisipate tatizo lolote maana nikiugua, hii pikipiki ndiyo basi tena.

"Kitu kingine kibaya zaidi, mabosi wengi mwanzoni huwa wanakuwa wapole sana lakini akishaona unakaribia kumaliza mkataba, wengi wao huwa wanaanza kuleta figisu, mradi tu akupokonye pikipiki ili apate faida mara mbili," anasema.

Mengi Mathias, bodaboda maeneo ya Makumbusho wilayani Kinondoni, anasema mabosi wengi wanatoa mikataba kandamizi, akifafanua kwa kauli: "Mkataba wangu una upungufu mkubwa lakini nilikubaliana nao kwa sababu sikuwa na kazi na nilikuwa nimeshaangaika kutafuta pikipiki kwa muda mrefu bila mafanikio.

"Ukikataa kutokana na masharti ya mkataba, bosi anatafuta mtu mwingine. Sasa kwa mazingira kama hayo, lazima utaichukua tu hivyo hivyo. Tunaomba serikali iangalie namna ya kututetea.

"Hili kundi ni kubwa, lina watu wengi na kuna kesi nyingi kwa viongozi wetu kati ya mabosi na madereva, malalamiko ni hayo hayo ya kupokonya pikipiki bado wiki mbili, tatu."

Hamisi Mgoba, bodaboda maeneo ya Tegeta, anasema bodaboda wengi wanaingia kwenye mtego wa mabosi wao kutokana na kukosa elimu ya mikataba na kwamba wengi hawashirikishi wanasheria wanapoingia mikataba kwa kuogopa gharama za kumlipa mwanasheria.

Mwenyekiti wa Bodaboda Mkoa wa Dar es Salaam, Maiko Masawe, anakiri kuwapo shida hiyo, akibainisha ofisi yake imeshashughulikia kesi za aina hiyo zaidi ya 100.

"Kweli kuna tatizo hilo kwa madereva na mabosi wa pikipiki, wengi wao wanapewa mikataba kandamizi. Unakuta kijana amebakisha wiki moja amalize mkataba lakini anapokonywa chombo na bosi kwa sababu ndogo tu, wakati mwingine wanafikia hata hatua ya kugombana na kupelekana polisi.

"Kinachowaponza bodaboda wengi, ni kwamba wana njaa (hawana fedha), kwa hiyo muda mwingine huwa wanaingia mkataba bila kuomba ushauri kwa watu wenye uelewa katika kutafsiri mkataba, kuona kama una mizania sawa kwa pande zote.

"Sasa baada ya kuona hali hiyo imezidi kuwa tishio, tumeamua kuja na njia ya kuwaepusha na mikataba toka kwa watu binafsi na kuwahamishia kwenye taasisi nyingine.

"Tumeongea na Benki ya NMB ili iwe inawakopesha kwa riba nafuu kwa sababu mkataba wao ni miezi 12 na unapeleka Sh. 7,000 kwa siku, lakini mkataba wa mtu binafsi ni miezi 14 hadi 15 na dereva anapeleka Sh. 10,000 kila siku, kwa hiyo unaweza kuona ni kwa namna gani kuna utofauti mkubwa.

"Hivyo, niwatake madereva kuendelea kuchangamkia fursa kuchukua pikipiki zinazotolewa na NMB kwa kuwa zina masharti nafuu na hazina mikataba kandamizi," Masawe anasema.

*ITAENDELEA KESHO

# NAMNA YA KUTAMBUA STEMPU HALALI ZA KODI ZA KIELEKTRONIK (ETS)

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

Stempu ya kodi ya kielektroniki **(ETS)** ni alama maalum **(label)** inayobandikwa au kuchapishwa katika bidhaa ili kuonesha kuwa bidhaa hiyo imelipa kodi.




Kwa kutumia **App** iitwayo **"Hakiki Stempu"** ambayo inapatikana kwa wenye simu janja (smart phones) aina zote mtumiaji wa bidhaa anaweza kuhakiki.




**HATUA ZA KUFUATA**


**1.** Pakua (download) App yako ya **"HAKIKI STEMPU"** kwa watumiaji wa **Android** kutoka **(Google Play)** na kwa watumiaji wa **iOS** kutoka **(Apple Store)** kwa kuandika neno **"HAKIKI STEMPU"** na kuinstall katika simu yako, kisha ukishakamilisha utaiona App husika katika simu yako.




**2.** Baada ya kuipakua na kuinstall, moja kwa moja fungua App hiyo na kisha ukurasa wa mwanzo (Splash Screen) utatokea ambapo Vigezo na Masharti **(Terms & Conditions)** zitaonekana ambapo utatakiwa kuzikubali **(Accept)** ili kuweza kuendelea mbele zaidi.




**3.** Kisha, App ya **"Hakiki Stempu"** itapenda kupata ruhusa ya kutumia kamera ya simu yako ili iweze kuscan bidhaa husika, hivyo utapaswa kukubali kwa kubonyeza kitufe cha **"OK"** na hapo App itakupeleka katika ukurasa wa **KuScan** bidhaa hiyo, ndipo utaweza kuhakiki alama za usalama kwa kuscan stamp yako iliyobandikwa kwenye bidhaa husika.



**4.** Eneo linalotakiwa kuwa scanned ni eneo **namba 2** kwenye **QR Code** kama inavyoonekana katika picha hapa.




**5.** Mara baada ya kulengesha kibox cha kuscan katika QR Code iliyo kwenye stempu, App itascan yenyewe na kukuuliza iwapo unaona mabadiliko ya rangi katika stempu iwapo ukiiangalia kwenye mwanga, na utabonyeza sehemu ya **"YES"** kama inavyoonekana katika picha.




**6. Hakiki Stempu** itakupatia majibu ya uhalali wa stempu iliyobandikwa katika bidhaa kama ifuatavyo,

**>>** Iwapo Bidhaa ni halali, basi simu yako itaonesha **namba** na **herufi** kama zilivyo kwenye stempu yaani; **jina la bidhaa, aina ya bidhaa, imezalishwa lini, jina la mzalishaji** na **namba ya Barcode.**




217199702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi Ligi Kuu Bara walindeni wachezaji

**MBIO** za Ligi Kuu Bara mzunguko wa pili zimeanza kwa kasi kila timu ikijaribu kuchanga karata zake vema ili mwishoni mwa msimu kuweza kutimiza malengo iliyojiwekea mwanzoni mwa msimu huu wa 2022/23.

Tunatambua kila klabu imejiwekea malengo yake kwani zipo ambazo lengo lao ni kutwaa ubingwa, zingine zikiwania nafasi nne za juu tu ili kukata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa. Lakini zipo ambazo lengo lao ni kuepuka tu kushuka daraja ili msimu ujao ziendelee kuwamo latika ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kuanzia msimu ulioisha.

Malengo yote hayo yatachangiwa na kiwango bora, kujituma kwa wachezaji, mbinu za makocha, afya njema za wachezaji, uwezeshwaji kutoka kwa viongozi wa klabu na mengineyo kama hayo ndani na nje ya uwanja.

Hata hivyo, wakati makocha, wachezaji na hata viongozi wa klabu wakijitahidi kutekeleza wajibu wao ipasavyo, inaonekana tatizo kubwa limekuwa kwa waamuzi kushindwa kuchezesha kwa kuzingatia sheria 17 za soka duniani.

Tumekuwa tukitoa kilio chetu hapa mara kwa mara kwa waamuzi kushindwa kutenda haki uwanjani jambo ambalo linasababisha baadhi ya timu kupoteza alama visivyostahili na zingine kunufaika na maamuzi ya waamuzi ya ovyo.

Lakini wakati tukitoa kilio hicho cha baadhi ya timu kupoteza isivyostahili na nyingine kunufaika kutokana na maamuzi maovu, kumejitokeza tatizo lingine ambalo ni la hatari, kwa waamuzi kushindwa kulinda afya za wachezaji uwanjani.

Waamuzi wamekuwa wakimezea rafu mbaya wanazochezewa baadhi ya wachezaji, jambo ambalo sasa zimeonekana ni kawaida, hivyo kuzidi kuhatarisha afya zao, kitu ambacho kinaweza kuathiri hadi matokeo ya timu husika.

Ifahamike kitendo cha mwamuzi kumezea adhabu inayostahili kadi hususan ya njano, basi kinampa nafasi mchezaji husika kuzidi kucheza faulo akiamini ni jambo la kawaida, lakini akijua hana kadi inayoweza kumsababishia kutolewa nje ya uwanja na kuiathiri timu yake.

Suala hilo limekuwa likisababisha baadhi ya wachezaji kucheza faulo za hatari zaidi dhidi ya wenzao, kitu ambacho hatuombei kitokee, lakini kwa mwenendo huo kikivumiliwa kinaweza kusababisha hata mauti uwanjani.

Hivyo, tunataka kuona waamuzi wakianza kutoa adhabu kwa wacheza faulo, iwe dakika ya kwanza ama ya mwisho na iwe ni kwa mchezaji timu yale imeshapoteza ama inaongoza na bila kujali ukubwa wa timu, kama kadi inayostahili ni njano ama nyekundu, itolewe tu bila hofu.

Hatutaki kuona baadhi ya madhambi yakimezewa mate kwa sababu hizo ama kwa kuwa mchezaji husika anatoka klabu kubwa nchini, sisi tunachotamani kukiona ni afya kwanza ya wachezaji zinalindwa ipasavyo kwa kufuata sheria 17 uwanjani na si vinginevyo.

Tulitamani kuona waamuzi wetu wakiwa wamejifunza kutoka fainali za Kombe la Dunia namna wenzao walivyokuwa makini kwa kila kitu kwa kuzingatia sheria 17 za soka duniani kwani walionyesha kujali hata muda wa nyongeza, faulo zinazochezwa na wachezaji, lakini pia penalti zikitolewa hadi mbili kwa timu moja jambo ambalo kwa hapa Ligi Kuu hilo ni vigumu kufanywa hususan kwa timu inayoongoza.

Ni wakati sasa kwa waamuzi wetu kubadilika na kwenda sambamba na sheria 17 za soka ili kulisaidia soka letu na kuliwezesha kufika kule tunapotamani kufika walipo wenzetu duniani, na hilo litawezekana tu kama sheria zitafuatwa na waamuzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# TPLB ilivyoshindwa kwenda na muda Kombe la Dunia

**NAKUMBUKA** Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia, siku chache kabla ya michuano ya Kombe la Dunia 2022 kuanza, aliishauri Bodi ya Ligi nchini (TPLB), kuangalia uwezekano wa kubadilisha hakukuwa muda wa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ili zisigongane.

Karia akasema kuna mechi zenye mvuto kwenye michuano hiyo, hivyo wakaishauri bodi kuangalia kama kuna uwezekano wa kupeleka mbele au kurudisha nyuma zile mechi za ligi ambazo zitaangukia kwenye mechi hizo.

Binafsi, naona kwa asilimia kubwa hakukuwa na kitu kama hicho. Nilikuwa naona mechi za ligi zikichezwa muda ule ule ambao umepangwa hata kama kuna mechi za Kombe la Dunia.

Nilikuwa naona hata sehemu ambazo watu wanaangalia mpira kwenye televisheni kunakuwa na TV mbili zimewekwa, nyingine ni ya kuangalia mechi ya Ligi Kuu na nyingine Kombe la Dunia ambazo zilikuwa zinachezwa kwa wakati mmoja.

Labda zile zilizokuwa zinachezwa saa nane mchana na saa nne usiku. Tena zile za saa nane zilikuwa zikigongana na baadhi ya mechi za ligi zilizokuwa zikichezwa muda huo wa mchana. Labda kwa sababu nyingi zilikuwa si zenye mvuto.

Kuna mechi za Kombe la Dunia zilikuwa zinachezwa saa 12:00 jioni hasa za kuanzia robo fainali na saa 2:00 usiku, hizi kwa kiasi kikubwa ziliingiliana mno na muda wa mechi za Ligi Kuu. Zilikuwa zinapishana kipindi kimoja, yoyote ile ikianza, iwe ya Kombe la Dunia au mechi ya ligi.

Ukiangalia muda wa mechi za Kombe la Dunia zilizokuwa zinachezwa mwaka huu nchini Qatar, utaona zilikuwa zikiwachanganya sana mashabiki wanaotaka kwenda kuangalia mechi za Ligi Kuu uwanjani, hasa wale wa saa 1:00 usiku.

Mfano mdogo tu, Jumamosi iliyopita kulikuwa na mechi ya kusaka mshindi wa tatu kati ya Croatia na Morocco, huku Yanga ikiwa inacheza mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Ambao hawakuathirika ni wale walioamua kubaki majumbani na kupata fursa ya kuangalia mechi zote mbili kupitia TV kwa wakati mmoja. Hii inaathiri sana mapato ya ligi kwa sababu wengi hawaendi uwanjani. Ukienda uwanjani huioni mechi ya Kombe la Dunia, lakini ukibaki utaona mechi zote mbili.

Na ilikuwa hivyo kwa mechi kadhaa. Mechi za Benjamin Mkapa hazikuwa na sababu ya Bodi ya Ligi kuzichezesha saa 1:00 usiku wakati wa michuano hiyo ikiendelea. Ilipaswa ichezwe saa 10:00 ili mashabiki waje kwa wingi, halafu saa 12:00 watoke waende 'vibanda umiza' au majumbani kuangalia mechi hizo.

Nakumbuka pia mwezi uliopita Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, alikiri kuwa idadi ya mashabiki imepungua uwanjani na bodi ipo katika kufanya tathmini na kutafuta ufumbuzi wa sababu ya watu kutoingia uwanjani kama ilivyo miaka ya nyuma.

Kutokana na hali hiyo, TPLB ikasema ipo katika mchakato wa kupata mshauri wa kufanya tathmini ya kupungua kwa watu uwanjani na kushuka kwa mapato ya mlangoni katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Binafsi, naamini moja kati ya sababu ni hii ambayo imejitokeza kwenye michuano hii, na inaweza kuendelea wakati wa Ligi Za Ulaya zikirejea tena.

Wala haihitaji mshauri kujua kuwa kama Manchester United inacheza dhidi ya Arsenal saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki, halafu kuna mechi Uwanja wa Benjamin Mkapa muda huo kama itapata mashabiki wengi.

Umefika wakati sasa Bodi ya Ligi kwenda kulingana na kasi ya dunia inavyokwenda, kwani mashabiki wa soka ni wale wale. Cha kufanya ni kutafuta utaratibu wa kuwavuta kwenye mechi za ligi kwa kuangalia muda wa mechi zenye mvuto Ulaya, halafu unarudisha nyuma muda au kupeleka mbele ili kuwapata wote na baadaye kuwaachia wote waende kuangalia mechi zingine.

Vita ya kunyang'anyana ni mbaya kwa TPLB, matokeo yake mashabiki wanapungua uwanjani, kwani wanatumia gharama ndogo kuangalia mechi maeneo ya majumbani kwao, huku wakiangalia pia ligi za Ulaya.

# Serikali yabaini tatizo urasimishaji ardhi

**Na Anthony Ishengoma**



WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (pichani), ametoa siku 14 kwa Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Dar es Salaam kukaa na kampuni za upimaji ardhi mkoani humo ili kujiweka sawa kuhakikisha urasimishaji mkoani Dar es Salaam unakwamuliwa kwa kuwa muda uliopangwa kwa kazi hiyo unakaribia kufikia tamati.

Aliagiza hayo jana kwenye Viwanja vya Mbagala Kuu mkoani Dar es Salaam, akionya kuwa kampuni za urasimishaji na upimaji wa viwanja ambazo zimechukua fedha za wananchi na kushindwa kukamilisha kazi hiyo, zitatakiwa kurudisha madeni, pia kufutwa ili iwe funzo kwa kampuni zingine ambazo zinafanya kazi kinyume cha taratibu na kushindwa kufikia malengo.

Waziri Mabula pia alimtaka Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke na Kamishna Msaidizi wa Ardhi Dar es Salaam kuhakikisha maombi yote ya hati ambayo wananchi wamewasilisha na kukamilisha malipo, yawe yamefanyiwa kazi na wananchi wamepatiwa hati zao ifikapo mwishoni mwa mwezi huu.

Vilevile, waziri huyo aliziagiza halmashauri zote nchini ambazo ni mamlaka za upangaji ardhi, kuhakikisha zinatenga fedha kwa ajili ya kupima kupanga na kumilikisha ardhi badala ya kuachia suala hilo kubaki kuwa mzigo kwa wizara ilhali ni majukumu ya halmashauri kufanya kazi hiyo.

Waziri Mabula pia alipiga marufuku Mkoa wa Dar es Salaam kuendelea kutoa hati zinazozalishwa kwa njia ya analogia kwa wakazi wa mkoa huo na badala yake watoe hati za kidijitali kwa kuwa mfumo wa ILMIS unafanya kazi.

Aliwataka kuendelea kuhuisha kanzidata za ardhi katika mfumo wa kidijitali na kuzitaka halmashauri nyingine nchini kuendelea na kazi hiyo.

Waziri huyo aliwaonya wale wote wanaoendelea na uvamizi kwenye maeneo ya watu bila kwenda ofisi za halmashauri nchini kujiridhisha kuwa wanatenda kosa la jinai na kuonya watendaji wa kata na vijiji kuuza ardhi kwa kuwa hilo sio jukumu lao, bali wenye mamlaka hiyo ni ofisi za halmashauri.

Dk. Mabula aliongeza kuwa wananchi lazima wafuate sheria za ardhi zilizoko na kuonya kuwa kuna baadhi ya watu waliofanya uvamizi na wakatakiwa kulipa mwenye eneo lake lakini wameshindwa kufanya hivyo, hivyo sheria zitafuatwa na kuhakikisha wanatolewa kwenye maeneo hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Temeke, katika hotuba yake ya kumkaribisha mgeni rasmi ili kushiriki utoaji hati kwa wananchi hao, alisema kuna watu wanapoteza umiliki kutokana na kutopima ardhi, suala linalosababisha migogoro ya ardhi kwa kuwa kuna baadhi ya wananchi wakijua eneo halina hati, wanatengeneza nyaraka feki na kupora mali za wananchi.

Kamishna Msaidizi wa Ardhi Dar es Salaam, Shukrani Kyando, alisema urasimishaji jijini Dar es Salaam unakabiliwa na vikwazo kadhaa, ukiwamo uelewa mdogo wa wananchi kuhusu suala la urasimishaji na baadhi ya kampuni zinategemea michango ya wananchi, hivyo kushindwa kuendesha urasimishaji kama ilivyopangwa.

# Watakaopisha mradi wa Tembo Nickel kunufaika

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wanaotarajiwa kupisha mradi wa uchimbaji madini wa Tembo Nickel, wameanza kupatiwa elimu ya kilimo na ufugaji wa kisasa.

Waliopewa mafunzo hayo ni miongoni mwa wajumbe wa Mkutano wa Uhamishaji Watu Makazi (RWG), waliopata fursa ya kuhudhuria maonesho ya saba ya kilimo mseto yaliyofanyika Novemba 24 hadi 26 mjini Musoma mkoani Mara.

Maonesho hayo yaliyokuwa na kaulimbiu ya 'bayonuai kwa usalama wa chakula na kipato', yaliwawezesha wananchi hao ambao wengi ni wakulima na wafugaji, kujifunza mbinu za kufanya kilimo bora bila kutumia mbolea za madukani na kufuga mifugo bila kutegemea dawa za dukani.

Meneja Msaidizi wa Kituo cha Vi Agroforest, kilichoko mjini Musoma, Silvester Philemon, akitoa elimu kwa wananchi hao alisema wanahamasisha kilimo hicho kwasababu ni salama kwa chakula kinachozalishwa pamoja na afya ya udogo.

"Kwa elimu hii, unaweza kutumia vitu vilivyokuzunguka nyumbani kuhakikisha mbogamboga zako zinakuwa, mifugo yako haiugui, pia unatunza mazingira kwa kutengeneza jiko la kutumia gesi ya kinyesi cha mifugo kwa teknolojia rahisi kabisa," alisema.

Alisema, kupitia kituo chao cha mafunzo cha Vi Agroforest kilichoko Musoma, wanatoa mafunzo ya kilimo hicho na ufugaji kwa makundi mbalimbali.

Elimu hiyo ya uzalishaji hutolewa shuleni, kwa vijana na kinamama.

Wajumbe hao wakiongozwa na Eraldius Batakanwa, walisema elimu waliyoipata imewasaidia pia utengenezaji wa jiko la gesi itokanayo na kinyesi cha mifugo.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA HUDUMA YA MPITO KWA WAGUSWA WA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA KUMBUKUMBU NA: REQ-00000075

EACOP Ltd Tanzania, Kampuni ya Mafuta na Gesi inakaribisha Kampuni zinazojihusisha na Kilimo, Usambazaji wa Chakula zenye uzoefu, na ambazo ziko tayari kutoa Huduma za Usambazaji wa Chakula kwa Waguswa wa Njia ya Bomba katika Mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

Bomba hilo litapita kwenye jumla ya Mikoa nane (8) ambayo ni **Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga.** Pia linagusa **Halmashauri za Wilaya 27** na **vijiji 231.**

### MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA

Mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (hapa ikijulikana kama "Mradi") unahitaji Ardhi kwa ajili ya ujenzi wa Bomba pamoja na miundombinu mingine. Kwa sababu hiyo, Mradi unaratibu zoezi la Utwaaji wa Ardhi kwa waguswa walioguswa makazi na kiuchumi.

Ili Kupunguza athari za Uhamishaji wa Watu na Makazi, mradi unatarajia kutoa huduma ya mpito kwa waguswa wa Njia ya Bomba na miundombinu ya juu. Huduma ya chakula inatolewa kama nyongeza ya Fidia katika kusaidia Jitihada za Kaya iliyoguswa na Mradi kumudu kupatikana kwa chakula katika kipindi cha mpito (baada ya eneo la ardhi kutwaliwa na hadi urejeshaji wa hali za maisha ya mguswa kufikiwa). Chakula kitakachosambazwa kinajumuisha: Mahindi, Maharage, Mchele, Mafuta ya Kupikia na Chumvi.

Mradi unahitaji Kampuni zenye sifa, na uzoefu katika kutoa huduma ya usambazaji wa chakula kutoa huduma ya usambazaji wa Chakula katika vipenGele vitatu: 1) Ununuzi wa bidhaa za chakula, 2) Uhifadhi na Ufungashaji wa bidhaa za chakula , na 3) Usambazaji wa chakula kwa waguswa/Kaya zilizoguswa kila mwezi. Makadirio ya kiwango kinachohitajika ni kama inavoonekana hapo chini:

**Kipengele 1a: Ununuzi wa bidhaa za Chakula kwa waguswa/kaya zilizoguswa wenye athari zaidi kwa kipindi cha miezi 12**

| Mkoa | Idadi ya Vijiji | Makadirio ya Kiwango kwa Miezi 12 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mahindi (kg) | Mchele (kg) | Maharage (kg) | Mafuta (lt) | Chumvi(kg) |
| Kagera | 34 | 39,840 | 39,840 | 39,840 | 9,960 | 1,992 |
| Geita | 40 | 47,336 | 47,336 | 47,336 | 11,834 | 2,367 |
| Shinyanga | 16 | 14,280 | 14,280 | 14,280 | 3,570 | 714 |
| Tabora | 30 | 51,240 | 51,240 | 51,240 | 12,810 | 2,562 |
| Singida | 31 | 42,900 | 42,900 | 42,900 | 10,725 | 2,145 |
| Dodoma | 23 | 17,280 | 17,280 | 17,280 | 4,320 | 864 |
| Manyara | 11 | 25,740 | 25,740 | 25,740 | 6,435 | 1,287 |
| Tanga | 46 | 83,820 | 83,820 | 83,820 | 20,955 | 4,191 |
| **JUMLA** | **231** | **322,436** | **322,436** | **322,436** | **80,609** | **16,122** |

**Kipengele 1b: Ununuzi wa bidhaa za chakula kwa waguswa/kaya zilizoguswa wenye athari za wastani kwa kipindi cha miezi 6**

| Mkoa | Idadi ya Vijiji | Makadirio ya Kiwango kwa Miezi 6 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mahindi (kg) | Mchele (kg) | Maharage (kg) | Mafuta (lt) | Chumvi(kg) |
| Kagera | 34 | 224,280 | 224,280 | 224,280 | 56,070 | 11,214 |
| Geita | 40 | 240,366 | 240,366 | 240,366 | 60,092 | 12,018 |
| Shinyanga | 16 | 86,020 | 86,020 | 86,020 | 21,505 | 4,301 |
| Tabora | 30 | 98,140 | 98,140 | 98,140 | 24,535 | 4,907 |
| Singida | 31 | 167,700 | 167,700 | 167,700 | 41,925 | 8,385 |
| Dodoma | 23 | 89,640 | 89,640 | 89,640 | 22,410 | 4,482 |
| Manyara | 11 | 44,070 | 44,070 | 44,070 | 11,018 | 2,204 |
| Tanga | 46 | 104,170 | 104,170 | 104,170 | 26,043 | 5,209 |
| **JUMLA** | **231** | **1,054,386** | **1,054,386** | **1,054,386** | **263,597** | **52,719** |

- Muombaji anapaswa kuonyesha mnyororo wa utoaji huduma **uliopo** wenye uahkika wa kusambaza kiawango kinachohitajika wakati wote wa utekelezaji wa Mradi.
- Muombaji anapaswa kuonyesha **uthibitisho** wa Usajili katika mamlaka zinazohusika na afya na usalama wa chakula.

**Kipnegele 2: Kuhifadhi na Kufungasha bidhaa za chakula kwa kipindi cha miezi 12**

- Waombaji wanapaswa kuonyesha **Uthibitisho** wa Ghala analomiliki au alilokodi kwa ajili ya kuhifadhia bidhaa.
- Waombaji wanapaswa kuonyesha **Uthibitisho** wa eneo la kufungashia bidhaa, teknolojia na vifaa vinavyotumika katika kufungasha bidhaa.

**Kipengele 3: Usambazaji wa bidhaa kwa waguswa/kaya zilizoguswa kwa kipindi cha miezi 12**

- Waombaji wanapaswa kuonyesha **Uthibitisho** wa vyombo/vifaa pamoja na mtandao wa Usafirishaji/Usambazaji wa bidhaa za chakula
- Waombaji wanapaswa kuonyesha **Uthibitisho** wa mfumo wa usambazaji, ugawaji, uhakiki wa wanufaika, pamoja na ufwatiliaji wa kiwango cha chakula kilichogawiwa kwa waguswa, pamoja na mbinu za kuzuia udanganyifu.

Waombaji wanapaswa kuleta maombi kwa Vipengele vyote. Waombaji ambao wangependa kutoa huduma kwa kipengele kimoja watapaswa kutoa sababu mahsusi za kufanya hivyo.

### VIGEZO MUHIMU

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa Usajili wa Kampuni Kutoka katika Mamlaka zinazohusika na Usajili wa shughuli za Makampuni(BRELA, TBS, OSHA)
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni.
- Kampuni zinazotumia wasambazaji wa kutoka maeneo yaliyoguswa na mradi ziwasilishe taarifa za wasambazaji wao pia.
- Inashauriwa, muonyesha nia awe amekwisha jisajili au ametuma maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoajina msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi.
- Uthibitisho wa taarifa za Ukaguzi wa hesabu wa kampuni za hivi karibuni.
- Uthibitisho wa mtandao wa wasambazaji wa maeneo yanayopitiwa na mradi, ikielezea miundombinu muhimu kuwezesha usambazaji wa huduma ya chakula. Taarifa zionyeshe mawasilaino na eneo analopatikana msambazaji.
- Uthibitisho wa vifaa/maeneo ya kuhifadhia, kufungasha, na kusambaza chakula na hali ya ubora wa vifaa Pamoja na maeneo ya kutolea huduma
- Uthibitisho wa uwezo wa kukusanya na kutunza kiwango cha chakula kinachotakiwa kwa waguswa muda wote wa utekelezaji wa Mkataba.
- Uthibitisho wa mfumo na taratibu za kiafya na kiusalama unaotumiwa na Kampuni.

217196102

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (Ukubwa Usiozidi **MB20**) hadi kufikia saa **11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **02/01/2023**. Kichwa cha Barua Pepe kiwe: **REQ-00000075** HUDUMA YA MPITO KWA WAGUSWA.

**Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.**
**Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.**

**Muhimu:** EACOP itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yaliyoonesha nia kulingana na Tangazo hili la Nia ya kutoa Huduma, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP Ili kubaini makumpuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila ya kutoa sababu kwa kamapuni husika.

# Kikosi kazi kudhibiti umwagikaji mafuta baharini, ziwani chaundwa

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) kwa kushirikiana na wadau wake, limeanzisha kikosi kazi cha kukabiliana na umwagikaji wa mafuta kwenye maziwa na bahari nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa TASAC, Meneja wa Viongozea Meli, Ulinzi na Mazingira wa shirika hilo, Celestine Mkenda alisema mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam kuwa kumekuwa na kumwagika mafuta baharini na kwenye maziwa ambako ndiko hutumika kuyaingiza nchini.

Alisema hali hiyo inasababisha athari na hasara kubwa za kiuchumi hususani kwa viumbe hai kufa na kiafya kwa wanaoendesha shughuli zao majini.

"Na hivi karibuni kulitokea tukio la kumwagika mafuta baharini mkoani Tanga, ilileta athari kubwa na sababu kuyasafisha ni gharama kubwa kutokana na kuhitaji vifaa maalum vya kufanyia kazi hiyo.

"Hivyo, kupitia kuunda kikosi kazi ambacho kinajumuisha wadau kutoka sekta ya umma na binafsi, itakuwa rahisi. Na katika kufanikisha hili, tumekutanisha waagizaji wa mafuta nchini kwa lengo la kujipanga kuuunda kikosi kazi hiki ili kuona ni jinsi gani tunajipanga na kupitia umoja huu.

"Tutanunua vifaa kwa pamoja, kuwa na rasilimali na mafunzo ya pamoja na endapo mafuta yatamwagika kwenye bahari na maziwa yetu, inakuwa rahisi kuyasafisha na kupunguza madhara yake," alisema.

Clever Mwaikambo kutoka Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu, alisema ni jambo jema serikali kuamua kuunda timu hiyo kwa sababu kampuni nyingi zimekuwa zikishindwa kumudu gharama za kusafisha kunapotokea mafuta kumwagika majini.

"Kama wadau wa TASAC, tulikwenda kujifunza katika nchi zingine namna ya kudhibiti mafuta yanayomwagika kwenye maji, huwa ni hatarishi kwa viumbe hai na yanasababisha madhara kiuchumi na kiafya, mikoko nayo huwa inakauka kabisa na mazingira kuyarudisha kwenye hali yake linapotokea hilo huwa ni ngumu sana," alisema Mwaikambo.

Halfan Amri Hassan kutoka Mamlaka ya Usafirishaji Baharini Zanzibar, alisema kuunda kwa umoja huo kutaleta tija kubwa katika sekta hiyo na kutaokoa hasara ambazo kampuni na serikali zimekuwa zikipata pale mafuta yanapomwagika kwenye maji na kuharibu rasilimali.

John Benard, Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Kampuni ya Total Tanzania, alisema kampuni nyingi zimekuwa zikishindwa kulipa gharama zinazotokana na kumwagika mafuta na kwamba uanzishwaji wa timu hiyo utasaidia kwa kiwango kikubwa kukabiliana na hatari hiyo.




Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua (kulia), akimkabidhi mfano wa hundi ya ushindi wa zawadi ya kufunguliwa duka lenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa Oswald Mwansumbule aliyejishindia kupitia Kampeni ya Amsha Ndoto Amsha Shangwe inayoendeshwa na Kampuni ya Vodacom Tanzania, jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. Wengine ni Meneja Masoko wa M-Pesa, Noel Mazoya (kushoto), Meneja Mauzo na Mkakati wa Biashara wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Magreth Lawrence na masta shangwe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aagiza walengwa TASAF wapewe mikopo ya halmashauri

**Na Veronica Mwafisi**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi (pichani), amewataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kutoa kipaumbele cha kuwapatia mikopo walengwa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) walio kwenye vikundi, kupitia fedha za asilimia 10 ya mapato ya halmashauri.

Amesema fedha hizo zinazotengwa kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu, vinapaswa kutolewa kwa kwa kundi hilo la walengwa wa TASAF ili mikopo hiyo iboreshe maisha ya kaya maskini nchini kama ambavyo serikali imekusudia.

Ndejembi aliagiza hayo mwishoni mwa wiki kwa wakurugenzi wa halmashauri nchini wakati akihitimisha ziara yake ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini katika Mkoa wa Dar es Salaam unaotekelezwa kupitia TASAF.

Alisema ametembelea vikundi mbalimbali vya walengwa wa TASAF kwenye halmashauri zote zilizoko Dar es Salaam na kuona utekelezaji wa kazi za vikundi mbalimbali vinavyojumuisha vijana, wazee, watu wenye ulemavu na wanawake.



"Wilayani Kinondoni kuna vijana walio kwenye vikundi vya TASAF walipatiwa mikopo wa pikipiki ambapo wamemudu kurejesha, pia wanawake wa Temeke walio kwenye vikundi vya TASAF wamepatiwa mikopo ya Sh. milioni 10 na Ilala wamepatiwa Sh. milioni 30 ambayo imewawezesha kuboresha maisha yao na kujishughulisha na ujasiriamali," Ndejembi alifafanua.

Mwakilishi wa Mtendaji Mkuu wa TASAF, Salome Mwakigomba, alisema mfuko huo umefanya jitihada kubwa kuhamasisha uundaji wa vikundi vya walengwa kwenye halmashauri zote ambazo Mpango wa Kuzinusuru Kaya Maskini unatekelezwa, hivyo wakipatiwa mikopo hiyo ya asilimia 10 wataendelea kuboresha maisha yao.

Mwakigomba alisema TASAF itatekeleza maelekezo ya Ndejembi ya kuwahamasisha walengwa wa TASAF kuwa na miradi endelevu ili wajiongezee kipato kitakachowawezesha kuboresha maisha yao.

Naibu Waziri huyo alihitimisha ziara yake ya kikazi mkoani Dar es Salaam iliyolenga kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma pamoja na kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kuzinusuru Kaya Maskini unaoratibiwa na TASAF.

## Kampeni matumizi salama ya pombe yawafikia maelfu

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti Breweries (SBL) imesema kupitia kampeni yake ya 'Unywaji Kistaarabu, Endesha Kistarabu' imewafikia zaidi ya madereva 5,000 nchini kwa kuwapa elimu wanafunzi 8,200 kuhusu madhara ya unywaji katika umri mdogo pamoja na kuwashawishi zaidi ya watu 2,000 kujifunza kuhusu matumizi ya pombe salama ndani ya mwaka 2022.

Jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Uhusiano wa Umma wa SBL, John Wanyancha, alibainisha hayo wakati wa uzinduzi wa ripoti ya SBL kuhusu shughuli endelevu chini ya kampuni tanzu ya East Africa Breweries Limited (EABL) ambayo imeonyesha mafanikio katika nyanja ya mazingira, jamii na utawala.

Wanyancha alisema kupitia mpango wake wa kijamii na kimaendeleo wa miaka 10 uitwao Society 2030: Spirit of Progress, unaoakisi maeneo sita ya unywaji pombe kistarabu, ujumuishi na utofauti, uendelevu makini, utunzaji maji, kufanya biashara vizuri na kaboni ya chini, SBL imedhihirisha utendaji mzuri.

"Katika kubadilisha mitazamo ya watu kuhusu matumizi ya pombe, SBL inatumia kampeni yake ya 'Unywaji kistarabu, endesha kistarabu, Jifunza kuhusu pombe' kupitia tovuti maalum ya DrinkiQ, ikiwafikia zaidi ya madereva 5,000 nchi nzima na kuelimisha zaidi ya wanafunzi 8,200 juu ya unywaji katika umri mdogo na kushawishi zaidi ya watu 2,000 kujifunza kuhusu matumizi ya pombe (DrinkiQ) ndani ya mwaka 2022.

"SBL inajivunia kuwa mstari wa mbele katika kuchochea maendeleo endelevu kwa njia ya kibunifu na ya kipekee inayoakisi ujumuishi. Tunategemea kuendeleza mpango huu na kutimiza malengo mengi," alisema Wanyancha.

Aliongeza kuwa katika nyanja ya ujumuishi na utofauti inayoangaliwa na serikali na sekta binafsi, SBL imejikita katika kutoa ufadhili wa masomo ya Kilimo Viwanda kupitia programu yake ya Kilimo Viwanda, iliyofadhili zaidi ya wanafunzi 200 wanaotoka katika familia zisizo na uwezo huku wanawake na watu wenye ulemavu wakipata nafasi sawa.

Kaimu Mkuu wa Chuo cha Kaole Wazazi College, Maxmillian Sarakikya, alisema mchango wa SBL kwenye elimu ni muhimu.

"Hii kampuni imefanya jambo kubwa sana kuinua vijana kimasomo hasa kilimo, tendo la kuigiwa kama mfano na kampuni na wadau wengine wa elimu," alisema Sarakikya.

Mwakilishi wa FDH, Michael Salali na Mwenyekiti wa taasisi hiyo alisema: "Tunajivunia kushirikiana na SBL katika agenda ya kutanua ujumuishi na utofauti wa watu, katika hilo SBL imewainua watu wenye ulemavu kwa kuwapa mafunzo ya kilimo, fedha na ujuzi," alisema.

# CRDB, Visa kuleta mapinduzi kwenye Sekta ya Utalii nchini

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB na kampuni ya kimataifa ya mifumo ya malipo ya Visa International wamekubaliana kushirikiana kuanzisha huduma ya kadi za kidijitali kwa ajili ya kuboresha huduma za malipo kwenye sekta ya utalii nchini.

Kupitia kadi hizo, Benki ya CRDB na Visa wanatarajia kutoa njia rahisi zaidi ya kufanya na kupokea malipo kwa wateja na kampuni za sekta ya utalii na usafirishaji kwa usalama na uharaka kulinganisha na mifumo mingine ya malipo.

Ushirikiano huo mpya na Visa, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, amesema ni hatua muhimu katika kufikia lengo la benki hiyo la kuleta mapinduzi kwenye mfumo wa kiikolojia wa malipo ya katika sekta ya utalii na usafiri nchini.

"Sekta ya malipo iko katikati ya mapinduzi na kuna hitaji kubwa la kampuni na mamlaka za utalii na usafiri kusimamia vyema uzoefu mzima wa malipo, alisema Nsekela juzi jijini Washington DC, Marekani.

Alisema sekta hiyo inazidi kushamiri na kuna wimbi kubwa la watalii nchini kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kupitia filamu ya 'Tanzania The Royal Tour'.

Sekta ya utalii nchini inazidi kuimarika baada ya janga la UVIKO-19. Ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inaonyesha mapato ya sekta hiyo yameongezeka maradufu hadi kufikia dola milioni 2,243.8 mwezi Septemba kutoka dola milioni 1,106. Watalii pia wameongezeka kwa asilimia 63.5 hadi 1,332,476.

Katika muktadha huo, Nsekela alisema kampuni katika sekta ya utalii na usafirishaji zinahitaji ufumbuzi wa hali ya juu na muunganisho katika mifumo ya kisasa ya malipo ambayo itakidhi mahitaji ya wateja wao ambao wengi wanapendelea huduma za kidijitali ambazo ni rahisi kutumia.

"Ushirikiano huu mpya na Visa utaisaidia Benki ya CRDB katika kuboresha mifumo yake ya kidijitali hususani katika huduma za kadi, jambo ambalo litakwenda kuboresha uzoefu wa huduma za malipo kwa taasisi, kampuni na wateja," alisema.

Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa Visa, Alfred Kelly Jr, alisema mfumo huo wa malipo kupitia kadi za kidijitali utakwenda kusaidia kuongeza ufanisi wa malipo na kutaimarisha mikakati ya malipo kwa wadau wote walio kwenye mnyororo wa thamani wa sekta ya utalii na usafirishaji Tanzania.

"Tunafurahia kuendeleza ushirikiano wetu na Benki ya CRDB, ushirikiano uliojikita zaidi katika kutumia utaalamu na ubunifu wa mifumo ya malipo kutoka kwa mashirika yote mawili ili kusaidia kukua kwa sekta ya utalii na usafirishaji," alisema na kubainisha zaidi kuwa watafanya kazi kwa pamoja ili kufanikisha ajenda ya ujumuishi wa kifedha nchini.

Benki ya CRDB na Visa pia walikubaliana kuanzisha huduma ya kutuma fedha kuvuka mipaka ili kurahisisha kuchochea biashara na kuwawezesha Watanzania wanaoishi nje ya nchi kutuma fedha nyumbani kwa urahisi na usalama.

"Rais Samia amefanya kazi kubwa sana ya kufungua nchi, biashara inapanuka, hivyo tunatakiwa kuweka miundombinu imara ya malipo ili kusaidia kuichochea. Hii ni pamoja na kuwawezesha Watanzania walioko ughaibuni kuwekeza nchini," alisema Nsekela.

Mkutano kati ya Benki ya CRDB na Visa ulifanyika pembezoni mwa Mkutano wa Viongozi wa Marekani na Afrika. Mapema mwezi huu viongozi wa mashirika hayo walikutana Qatar ambako wanashirikiana kuwapatia mashabiki wa Kombe la Dunia la FIFA huduma za malipo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto), akizungumza na Mwenyekiti na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Visa International, Alfred Kelly, kuhusu ushirikiano baina ya taasisi hizo katika kuanzisha huduma za malipo ya kidijitali katika sekta ya utalii. Mkutano huo ulifanyika wakati wa Mkutano wa Viongozi wa Marekani na Afrika Washington DC, Marekani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kisima cha mgodi kilivyoua mtoto

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MTOTO Danifodi Daudi mwenye umri wa miaka miwili na miezi minane, amefariki dunia baada ya kutumbukia kwenye kisima cha maji kwenye Mgodi wa Nyamatagata mkoani Geita.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani hapo, Edward Lukuba, alisema tukio hilo lilitokea Desemba 16, mwaka huu, majira ya saa 4:20 asubuhi.

Alisema walipata taarifa za tukio la mtoto kuzama kwenye shimo ambalo lilikuwa kama kisima na mara moja askari wa jeshi hilo waliokuwa zamu, waliambatana na mtoa taarifa hadi eneo la tukio kwenye Mgodi wa Nyamatagata, Kata ya Nyakabale wilayani Geita.

Lukuba alisema kuwa baada ya kufika eneo la tukio waliukuta mwili wa mtoto ukielea kwenye maji na askari wake waliuopoa na kukabidhi mwili wa mtoto huyo kwa askari polisi kwa uchunguzi zaidi.

Kaimu Kamanda huyo aliwataka wamiliki wa migodi huo kuhakikisha wanapomaliza kuchimba dhahabu, wawe wanafukia mashimo hayo ili kuepuka vifo vya aina hiyo.

Mama mzazi wa mtoto huyo, Pendo Ayubu (28) alisema amepanga kwenye nyumbani ya kufikia wageni iliyoko kwenye Mgodi wa Nyamatagata na kwamba mtoto wake huyo alikuwa amepotea tangu Desemba 14, mwaka huu majira ya saa 12 jioni.

Alisema kuwa siku hiyo, baada ya kumaliza kumwogesha, alikwenda nje kucheza na wenzake na yeye akatoka kwenda kununua mboga sokoni.

Pendo alisema kuwa baada ya kurejea nyumbani, aliwauliza watoto waliokuwa wakicheza naye alikokuwa mwanawe na walimjibu kuwa alikuwa amechukuliwa na baba mmoja mrefu na alikwenda naye dukani kumnunulia juisi lakini hakurejea tena kwenye nyumba hiyo ya wageni.

Alisema baada ya kuona mtoto wake hajarudi, alitoa taarifa kwenye ofisi ya Jeshi la Jadi (Sungusungu) kisha wakaanza kumtafuta.

Aliendelea kusimulia kuwa Desemba 16, mwaka huu, majira ya asubuhi alipigiwa na simu na mtu asiyemfahamu na kuambiwa kuwa kwenye kisima kuna mtoto amefariki dunia na mwili wake unaelea juu ya maji na alipofika eneo la tukio hilo alimtambua ni mwanawe.

Shuhuda wa tukio hilo Penina Charles (47), mfanyabiashara kwenye Mgodi wa Nyamatagata alisema mwili wa mtoto huo ulionwa ukielea na mama aliyekuwa anaokota chupa za maji.

Babu wa mtoto huyo, Shija Pungata (52) alisema mjukuku wake Danifodi Daudi amefariki kwa sababu mgodi wa Nyamatagata maeneo mengi yako hatarishi kutokana na mashimo mengi ya wachimbaji wa dhahabu hayajafukiwa ilhali hayatumiki tena.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Zahara Michuzi, alisema alishapiga marufuku watu kuingia na watoto wadogo kwenye maeneo la mgodi huo kwa kuwa ni maeneo hatarishi kwa kundi hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Safia Jongo alipoulizwa na Nipashe kuhusiana na tukio hilo, alidai kutokuwa na taarifa, akiahidi kufuatilia.

# Makosa 3,270 ya barabarani mwezi mmoja mkoa mmoja

**Na Said Hamdani,** LINDI

KATIKA kupambana na ajali zinazotokana na vyombo vya moto na watumiaji wake, Jeshi la Polisi Mkoa wa Lindi kupitia kitengo chake cha Usalama Barabarani, limebaini makosa 3,273 kwa kipindi cha mwezi mmoja uliopita.

Kamanda wa Polisi mkoani hapo, Pilli Mande alibainisha hayo mwishoni mwa wiki alipotoa taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha Novemba Mosi hadi 30 mwaka huu mbele ya waandishi wa habari ofisini kwake mjini Lindi.

Alisema kufuatia makosa hayo, watuhumiwa watatu (pasi na kutaja majina yao) waliohusika kuendesha vyombo vya moto na kusababisha vifo kutokana na uzembe, wamefikishwa mahakamani kujibu mashtaka yaliyowakabili na wengine baada ya kukutwa na hatia wametozwa faini.

Kamanda Mande alisema katika kuhakikisha usalama unaendelea kuimarishwa barabarani, askari wa jeshi hilo wakiongozwa na Kamanda wa Kitengo cha Usalama Barabarani, Peter Magayane, wamewafikia na kuwapa elimu abiria 3,852 waliokuwa wanasafiri na mabasi 120 makubwa na madogo kutoka na kuingia mikoa ya kusini.

Alisema kuwa katika kipindi hiki cha mwishoni mwa mwaka, jeshi hilo limejipanga vizuri kuhakikisha ulinzi na usalama unaimarishwa maeneo yote ya mkoa huo.

Kamanda Mande alitoa wito kwa wananchi kutojihusisha na vitendo vya uhalifu, akionya kuwa mtu au kikundi chochote cha watu kitakachojihusisha na vitendo vya uhalifu, Jeshi la Polisi kupitia askari wake halitasita kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria, ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani kujibu mashtaka yatakayowakabili.



Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara (wa pili kushoto), akimsikiliza mfanyakazi wa mgodi wa Barrick North Mara akielezea kuhusu kifaa cha uokozi wakati wa maonyesho yaliyofanyika 'Siku ya Family Day 2022' ambayo hukutanisha wanafamilia wa wafanyakazi wa mgodi huo. (Wa pili kulia) ni Meneja Mkuu wa Mgodi, Apolinary Lyambiko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TPDC yajitosa kuukabili uhaba wa samani shuleni

**Na Said Hamdani,** LINDI

SHIRIKA la Maendeleo na Petroli Tanzania (TPDC) limeikabidhi Shule ya Sekondari Kikonda iliyoko Kata ya Tingi wilayani Kilwa samani zenye thamani ya Sh. milioni 5.668 kwa lengo la kuwawekea mazingira rafiki ya kujisomea wanafunzi wa shule hiyo.

Msaada huo wa viti 85 na meza zake, umekabidhiwa kwa uongozi wa shule hiyo na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa shirika hilo, Oscar Mwakasege.

Akifuatana na Kaimu Mkuu wa Ulinzi na Usalama wa Miundombinu ya Gesi Asilia, Fredy Msigwa, wakati wa kukabidhi msaada huo mwishoni mwa wiki, Mwakasege alisema uongozi wa shirika umeamua kutoa msaada huo kwa sekondari hiyo ili kusaidia kutatua kero zinazowakabili wanafunzi katika kukuza viwango vyao vya elimu.

Mwakasege alisemaTPDC imekuwa mstari wa mbele kusaidia kutatua kero zinazoikabili jamii, zikiwamo za afya na maji, akisisitiza msaada huo utasaidia kukuza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa sekondari hiyo.

Kaimu Mkuu wa Ulinzi na Usalama wa Gesi Asilia, Fredy Msigwa, alisema huo ni mwendelezo wa kusaidia kuchangia kusogeza huduma karibu na wananchi pamoja na jamii kunufaika na rasilimali zilizoko nchini.

"Hii siyo mara yetu ya kwanza kufika na kutoa misaada, kwani tumeshakabidhi chumba kimoja cha darasa Shule ya Msingi Njia Nne," alisema Msigwa.

Mkuu wa Sekondari ya Kikanda, Christopher Fulgensi, aliishukuru TPDC kwa msaada huo na kueleza kuwa utawasaidia wanafunzi kujifunza kwa ufanisi zaidi.

Baadhi ya wanafunzi wanaosoma shuleni huko waliohudhuria hafla ya makabidhiano hayo, waliahidi kusoma kwa bidii na kufanya vizuri kitaaluma.

# Tanzania yatamba kuliteka soko la nyama la kimataifa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TANZANIA imefanikiwa kuongeza kasi na kuliteka soko la nyama kwenye nchi mbalimbali duniani kutokana na ubora wa bidhaa zake.

Msajili wa Bodi ya Nyama nchini, Dk. Daniel Mushi, alibainisha hayo mjini Morogoro, akieleza kuwa tayari Tanzania inauza nyama kwenye nchi za Qatar, UAE, Oman, Saudi Arabia, Bahrain, Jordan, Kuwait, Hong Kong, Vietnam, Kenya na Comoro.

Dk. Mushi alibainisha kuwa kwa kipindi cha miezi mitano kuanzia Julai hadi Novemba mwaka huu, jumla ya tani 4,374 za nyama zenye thamani ya dola za Marekani 16,760,284.45 zimesafirishwa kwenda masoko ya nje ya nchi.

Alisema uzalishaji wa nyama nchini umeendelea kuongezeka ambapo kwa mwaka 2020/21, jumla ya tani za nyama 738,165.99 zilizalishwa kupitia viwanda na machinjio mbalimbali nchini.

Alisema kuwa kwa mwaka wa 2021/22 uzalishaji wa nyama uliongezeka kwa asilimia 4.3 ukilinganisha na mwaka wa fedha wa 2020/21 ambao jumla ya tani 769,966.66 zilizalishwa.

"Upatikanaji wa masoko hayo umechangiwa na kuendelea kuongezeka kwa viwanda vya nyama na machinjio ya kisasa na biashara ya nyama hasa kwenye soko la nje imeendelea kukua kwa kasi," alisema Dk. Mushi.

Aliongeza kuwa kwa mwaka 2020/21, Tanzania iliuza jumla ya tani 1,774 katika masoko mbalimbali ya kimataifa na mwaka uliofuata (2021/22) iliuza jumla ya tani 10,415 sawa na ongezeko la asilimia 487.

Alisema ukuaji huo umechangiwa na jitihada kubwa zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi za kutafuta masoko mapya ya nyama nje ya nchi.

"Kuanzishwa kwa viwanda vya nyama kama Nguru Hills Ranch Ltd, umekuwa kichocheo muhimu kwenye ukuaji wa mauzo ya nyama nje ya nchi pamoja na maendeleo ya tasnia ya nyama kwa ujumla," alisema Dk. Mushi.

Akizindua machinjio ya kisasa ya mifugo ya Nguru Hills Ranch Ltd yaliyojengwa wilayani Mvomero mkoani Morogoro, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na uongozi wake mahiri.

Ndaki alisema uongozi huo mahiri umeifanya nchi iendelee kupiga hatua kubwa za maendeleo ya kiuchumi na kijamii zikiwamo sekta za mifugo na uvuvi ambazo masoko yamefunguka.

"Hivi sasa tumeteka masoko ya nje na sasa tunatarajia kuanza kuuza soko la China na hii ni baada ya Rais kufanya ziara huko na milango imefunguka kwa mazao ya nyama kutoka Tanzania na mojawapo ni samaki na nyama ya ng'ombe," alisema Ndaki.



## Wageni waonyesha shauku kujifunza mazao ya utalii

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

WAHIFADHI na maofisa wa Wizara ya Maliasili na Utalii, waliokuwa wakishiriki maonyesho ya kimataifa ya utalii na uwekezaji yaliyofanyika nchini Qatar, wamesema raia wa kigeni waliokuwa wakifuatilia michuano ya fainali ya Kombe la Dunia wameonyesha shauku ya kuja nchini, kujua kwa undani zaidi juu ya mazao ya utalii wa Tanzania.

Akizungumzia fursa hiyo jana, Ofisa Utalii Mwandamizi wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), George Mwagane, alisema bidhaa za utalii zinazotoka hapa nchini, zimekuwa kivutio kikubwa cha wageni kutoka mataifa mbalimbali waliokuwa wakishuhudia fainali za Kombe la Dunia.

Kwa mujibu wa Mwagane, idadi kubwa ya wageni waliojiandikisha katika daftari la waliotembelea banda la Tanzania, wamejiorodhesha na kuahidi kuja Tanzania kuwekeza na wengine kufanya utalii katika hifadhi.

Wahifadhi hao pamoja na maofisa wa wizara hiyo, walikwenda Qatar kwa ajili ya maonyesho maalumu ya utalii na uwekezaji yaliyofanyika katika Jiji la Doha.

Mwagane alisema ushiriki wa Tanzania katika maonyesho hayo na mwitikio wa wageni ulioko unaashiria kuwapo kwa uwezekano wa kufikiwa lengo la kuwa na watalii milioni tano na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii kufikia Dola za Marekani billioni sita ifikapo mwaka 2025.

Ofisa Utalii Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori nchini (TAWA), Elirehema Maturo, akieleza mafanikio kuhusu maonyesho hayo alisema: "Watalii wengi walipokuwa wakifika kwenye banda letu, walikuwa wanauliza maswali mengi na walivutiwa zaidi na fursa  za uwekezaji zilizoko kwenye tasnia ya utalii wa picha.

Maonyesho hayo ya kimataifa ya Doha yalianza rasmi Novemba 18, mwaka huu na yalimalizika Desemba 18, mwaka huu.

# Wabunge EAC wapendekeza kuondolewa vikwazo uchumi

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

BUNGE la nne la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) limevunjwa rasmi jijini Arusha baada ya kumaliza muda wake, huku baadhi ya wabunge wakitaka wakuu wa nchi wanachama wa jumuiya hiyo kutafuta namna bora ya kuondoa vikwazo vya kiuchumi.

Aidha, wamependekeza nchi wanachama wa jumuiya hiyo, kubuni vyanzo vya mapato vitakavyoiwezesha EAC kuendesha shughuli zake bila ya kuendelea kutegemea michango ya nchi wanachama na msaada wa wahisani kutoka nje.

Wazikungumzia wakati wa kikao cha mwisho cha Bunge hilo kilichofanyika mwishoni mwa wiki jijini Arusha, baadhi ya wabunge akiwamo Dk. Ng'waru Maghembe wa Tanzania, alisema baadhi ya masuala yanayoendelea kuikabili EAC ni kukosa mapato ya kujiendesha nje ya michango ya nchi wanachama.

Kutokana na tatizo hilo, Dk. Maghembe, alipendekeza mawaziri wa jumuiya hiyo wanapaswa kukutana, kupanga na kujadili aina mpya za vyanzo vipya ili kuiondoa jumuiya katika mtanziko wa mapato.

Kwa mujibu wa Dk. Ng'waru katika kipindi cha miaka mitano ya Bunge hilo walifanikiwa kupitisha miswada 20 ukiwamo wa nchi wanachama wa EAC kuwa na sarafu moja na kujadili maazimio 29 na kuandaa ripoti 45.

"Tunahitaji kuwa na vyanzo vyetu wenyewe kama nchi wanachama wa EAC, wote tunashuhudia jinsi ambavyo kutegemea michango inayotolewa na nchi wanachama inavyokuwa na mtanziko, hasa ukizingatia kwamba kuna nchi ambazo bado zina matatizo makubwa ya kiuchumi.

"Aidha, kuna suala lingine kubwa la kutafuta ufumbuzi wake, ambalo ni uhaba wa rasilimali watu unaosababisha watendaji kulazimika kufanya kazi ya ziada. Ziko nafasi nyingi ambazo ziko wazi ambazo zinahitaji watendaji, mfano hapa kwenye Bunge unakuta karani wa kamati analazimika kufanya kazi ya watu wawili. Anahudumia kamati mbili, badala ya moja," alisema.

Katika kikao hicho wabunge walimchagua Dk. Ng'waru Jumanne Maghembe kwa mara nyingine kutumikia wadhifa huo.

Mbunge kutoka Kenya, Aden Abdulkadir na Fred Mukasa kutoka nchini Uganda, kwa nyakati tofauti waliunga mkono pendekezo la mawaziri wa jumuiya hiyo, kutilia maanani umuhimu wa kubuni vyanzo vipya vya mapato na wakuu wa nchi za EAC, kuongeza jitihada zaidi kuondoa vikwazo vya kiuchumi kwa wananchi  wa ngazi za chini.



Mkuu wa Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara, Janeth Mayanja (kulia), akishirikiana na wananchi kuandaa miundombinu ya mabomba ya maji kwenye Kata ya Wareta juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Vyuo vya uhasibu vyatakiwa kupitia, kuhuisha mitaala

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameagiza vyuo vyote nchini vinavyotoa mafunzo ya uhasibu, fedha, uchumi na ukaguzi, kupitia na kuhuisha mitaala yao ili kuhakikisha fani hizo zinajumuisha kikamilifu stadi za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki jijini Arusha aliposhiriki  mahafali ya 24 ya Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA).

Hotuba yake iliyosomwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, Othuman Mtuka.

Aliagiza kuhuisha mitaala kwa kuwa sasa hivi mifumo mingi ya kiuhasibu serikalini na katika sekta binafsi inafanyika na inaendeshwa kwa kutumia TEHAMA hivyo kuna umuhimu wake.

Alisema vyuo hivyo vinapaswa kutilia mkazo uwekwaji kwenye akili isiyo asili, kuwawezesha wahitimu wa fani hizo wawe wenye tija na stadi kwenye soko la dunia.

"Chuo hiki na vingine vinavyotoa mafunzo ya biashara na uongozi vinatakiwa kuhuisha mitaala yao ili kujumuisha masuala ya uhasibu wa mazingira, jamii na utawala bora kwa kuwa uhimilivu wa taasisi ya umma na zile za binafsi unategemea kwa kiasi kikubwa uzingatiaji wa masuala haya.

Alisema wizara itaendelea kuwaunga mkono katika jitihada za kuboresha mazingira ya utekelezaji wa majukumu yao ya msingi ikiwamo kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa ufanisi kwa ajili ya kusaidia serikali.

"Kuhusu eneo la utafiti, ningependa kuona chuo kikijikita zaidi kufanya utafiti kwenye masuala ya uimarishaji wa makusanyo ya mapato ya serikali kwa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, usimamizi na udhibiti wa fedha za umma na kuimarisha matumizi ya TEHEMA katika sekta mbalimbali ili kuchochea tija na kuongeza ufanisi," aliongeza.

Alisema matumaini ya serikali ni kuona wataalamu wameandaliwa vyema kupitia mitaala hiyo na wanakuwa mstari wa mbele kutoa majawabu ya matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii, kwa ajili ya kujenga uchumi wa nchi na maendeleo ya mtu mmoja mmoja.


Kaimu Mkuu wa Chuo cha IAA, Dk.Cairo Mwaitete, alisema serikali kupitia mradi wa elimu ya juu kwa mageuzi ya kiuchumi, imetoa Sh. bilioni 44 kwa ajili ya kuboresha miundombinu na elimu katika chuo hicho.

Alisema kati fedha hizo Sh.bilioni 11 zitatumika kwenye ujenzi wa miundombinu ya elimu kwenye makao makuu ya chuo hicho, Sh. bilioni 14 zitatumiwa kwenye kampasi ya Manyara na Sh. bilioni 17 zitatumiwa kwenye kampasi mpya ya Songea.

Alisema serikali imetoa fedha nyingine Sh.bilioni tatu ambayo itakwenda kuendeleza ujenzi katika kampasi ya Manyara ili iwe ya kisasa, kutoa fursa kwa watu wengi kwenda kusoma.

Alisema pamoja na kuwa na miundombinu hiyo, wataboresha mitaala iendane na wakati sambamba na kuwajengea uwezo makufunzi wao na kwa mwaka huu wanatarajia kuwapeleka katika mafunzo wakufunzi 20.

Dk. Mwaitete alisema kumekuwa na ongezeko la wanafunzi 13,000 kutoka 3,000 kwa mwaka 2017/2018 na kwa mwaka huu  idadi imeongezeka hadi kufika 3,529 kutoka 2,481.





# RC anusa harufu ya ufisadi Halmashauri ya Korogwe

**Na Hamida Kamchalla,**
KOROGWE

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, amemwagiza Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe, kukagua upya taarifa ya mapato na matumizi ya miradi ya maendeleo ya halmashauri hiyo ya kipindi cha miaka mitano.

Kwa mujibu wa Mgumba, halmashauri hiyo inahitaji kufanyiwa ukaguzi wa ndani wa hesabu zake kuanzia mwaka 2017 hadi Desemba mwaka huu, kutokana na kugubikwa na sintofahamu inayojitokeza mara kwa mara katika utekelezaji wa miradi yake.

"Hii halmashauri imekuwa ni kawaida kusuasua kiutendaji. Haiwezekani kila mtu anajua kuanzia mkurugenzi wake, watendaji na wakuu wa idara wananyoosheana vidole kila inapotokea shida ya kiutendaji.

"Mkaguzi wa Ndani angalia taarifa za mradi huu (ujenzi majengo Hospitali ya Wilaya), kama ipo uilete, kama hakuna kagua uiandae na siyo kwenye mradi huu tu, fanya hivyo kwa miradi mingine yote lakini kwenye taarifa ya bajeti ya mwaka mzima 2021/22.

"Kuhusu mapato, miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa kutegemea mapato ya ndani na kutekelezwa pamoja na ile mingine ya nje, afanye ukaguzi wake. Vilevile na pesa za vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu kukagua kuanzia mwaka 2017 hadi leo (Desemba 2022)," alisema Mgumba.

Akijibu malalamiko ya wananchi kuhusu kuwapo viashiria vya ubadhirifu wa fedha katika halmashauri hiyo, Mgumba, alisema baada ya kupokea taarifa ya ukaguzi wa ndani, atampeleka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na yeye kupitia upya taarifa zote za miradi zilizofanywa na Mkaguzi wa Ndani ili kubaini kama na yeye atakuwa ametumika kuficha ubadhirifu.

Baada ya maelekezo hayo, Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri hiyo, Erick Ndunguru, alisema kazi ya kwanza atakayoanza nayo ni kukagua taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya mwaka 2021/22, katika muda usiozidi siku 30.

Wiki iliyopita, Mgumba alimsimamisha kazi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe, Nicodemus Bei na maofisa wake wengine wa tano, kupisha uchunguzi kutokana na tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mgumba alifikia uamuzi huo, baada ya kukagua na kubaini miradi mitano ya ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya Magunga, zahanati tatu za Mgombezi, Old Korogwe na Kilole, Soko la Kilole na shule moja ya sekondari haijamalizika.



Meneja wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Mkoa wa Kilimanjaro (SIDO), Allen Mhidze (kulia), akisisitiza wajasiriamali kujifunza namna bora ya kuhifadhi bidhaa za vyakula zinazozalishwa bila kutumia kemikali, kuhifadhiwa kwenye majokofu ya asili ili visiharibike kwa haraka, alipokagua bidhaa hizo kwa wananchi wa chini waliojengewa uwezo na Shirika la kiraia la TUSONGE CDO jana Manispaa ya Moshi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

## Waziri Mhagama: Maadili kwa watumishi yameongezeka

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amesema ukuaji wa maadili katika utumishi wa umma umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 64.4 mwaka 2014 hadi 75.9 kufikia mwaka huu.

Alitaja mafanikio hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha pili cha baraza la sita la wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kilichofanyika katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro.

Alisema serikali inaridhishwa na namna kiwango cha maadili kwa watumishi wa umma kwa sasa kinavyoimarika, huku akizitaka taasisi zote za umma nchini, kuhakikisha zinaimarisha utaratibu wa kisheria na kikanuni wa vikao vya wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria ya Mwaka 2004.

"Wiki iliyopita nimesoma hali ya matokeo kwa uzingatiaji wa maadili katika utumishi wa umma, matokeo ya utafiti uliofanywa na mtafiti, chini ya ofisi yangu kwa mwaka 2022, hali kwa sasa inaridhisha.

"Hali ya uzingatiaji wa maadili katika utumishi wa umma kwa mwaka 2022 umeongezeka kufikia asilimia 75.9 kutoka asilimia 66.9 mwaka 2014,"alisema.

Pia alisema matokeo ya ongezeko la utafiti huo yamechangiwa na serikali kuchukua hatua za kuweka misingi imara ya usimamizi wa maadili, mazingira wezeshi na kuimarisha uwajibikaji katika utumishi wa umma.

"Naagiza, waajiri kote nchini tambueni suala la vikao vya wafanyakazi, wasizuiwe kwa namna yeyote ile kujiunga na vyama vya hivyo. Hii siyo hisani ya mwajiri ila ni matakwa ya kisheria, hivyo litimizwe ili kutoa uwanja mpana kwa wafanyakazi kujadili matatizo yao," alisisitiza.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, aliahidi kuendelea kuongeza jitihada mbalimbali za katika uwajibikaji na ushirikiano katika utafiti ili kuhakikisha utatuzi wa matatizo ya wananchi unafanyika kulingana na takwimu na matokeo ya utafiti.

# Madiwani Arusha wataka Gambo ashughulikiwe

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MADIWANI wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, wamekiomba Chama Cha Mapinduzi (CCM) na serikali kumchukulia hatua za kinidhamu, Mbunge wa Arusha, Mrisho Gambo, kwa kuwatuhumu viongozi wa serikali kuwa wanataka kumuua.

Aidha, wamelitaka Jeshi la Polisi, kutofumbia macho madai ya Gambo ya kudai kwamba madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Arusha wamehongwa viwanja katika Mradi wa Bondeni City unaotarajiwa kujengwa katika kituo kipya cha mabasi yaendayo mikoani na nje ya nchi katika eneo la Muriet.

Diwani wa Kata ya Baraa, Jacob Mollel, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu madai hayo, alisema tuhuma za Gambo ni za uongo, uzushi na zenye lengo la kujitafutia umaarufu kisiasa.

Mollel ambaye ni mjumbe wa Kamati ya Fedha na Utawala ya Halmashauri ya Arusha, alisema hakuna fedha ya halmashauri inalipwa bila kamati hiyo kuidhinisha na kwenda katika baraza la madiwani na Gambo ni mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo.

"Mbunge wetu ametuvua nguo sisi madiwani wa CCM na serikali ya Mkoa wa Arusha, kwa kusema uongo hivyo tunaomba hatua kali dhidi yake zichukuliwe ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia za kuzusha uongo kama huu na kusababisha taharuki jijini hapa,"alisema.

Alisema Mradi wa Bondeni City, ulipitishwa katika kikao cha baraza la madiwani, katika kikao cha Novemba 22, mwaka huu, kwa kupiga kura na hakuna diwani aliyepinga kati ya madiwani 33 waliohudhuria kikao hicho, hivyo maamuzi yalikuwa halali kwa mujibu wa taratibu za vikao.

Diwani wa Kata ya Ngarenaro, Isaya Doita, ambaye ni mjumbe wa kamati hiyo alisema kauli ya Gambo ni kujitukana yeye mwenyewe kwa kuwa yeye ni mjumbe wa baraza la madiwani na Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Utawala.

"Kamati ya Fedha na Utawala hukutana kila mwezi kupitisha bajeti na mambo mengine muhimu ya Jiji na Gambo ni mjumbe na kamati hiyo, kamati iliidhinisha Sh.milioni 100 bila kufuata utaratibu, sakata hilo haliwezi kumwacha salama maana naye ni mojawapo," alisema.

Alisema Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, aliwahi kuagiza tuhuma ambazo ziko kwa Mkaguzzi Mkuu wa Serikali (CAG), zinapaswa kuchukuliwa hatua na kama tuhuma anazodai ziko mezani asubiri utekelezaji na siyo kuwahimiza kufanya mambo anayoyataka yeye.

Doita alisema Gambo hana uhusiano mzuri na Mstahiki Meya wa Jiji la Arusha, Maximilian Iranqhe, wala madiwani na hata sasa hana uhusiano mzuri na Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Arusha Hargeney Chitukuro.

Alisema utendaji kazi wa Gambo ni wa kusikitisha na wa kushangaza, kwamba ni wa kuviziana kama paka anavyovizia panya.

Diwani wa Kata ya Lemara, Naboth Silasile, alisema kauli ya Gambo dhidi ya madiwani na watendaji wa Jiji ni uzushi, uongo, uchonganishi zenye lengo la kujitafutia umaarufu.

Alisema hakuna diwani, aliyepewa kiwanja katika Mradi wa Bondeni City kwa kivuli cha udiwani na kama ana uthibitisho kwa tuhuma alizozitoa asisite kutoa hadharani ili hatua zichukuliwe.

Nipashe
Spotika



**MARCELO BROZOVIC; CHAPOMBE, MVUTA FEGI ALIYEVUNJA REKODI** UK. 16



# MIKIKIMIKIKI...

Beki wa Croatia, Joško Gvardiol (kulia), katika harakati za kumdhibiti mshambuliaji wa Morocco, Youssef En-Nesyri, kwenye mechi ya kutafuta mshindi wa tatu wa Kombe la Dunia 2022, iliyopigwa nchini Qatar juzi. Croatia ilishinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**

## ISIKUPITE

LIONEL Messi amempiku kwa mchezo mmoja zaidi nyota wa zamani wa Ujerumani, Lothar Matthaus, kwa kucheza mechi nyingi Kombe la Dunia la FIFA (26). Messi aliweka rekodi hiyo katika mechi ya fainali dhidi ya Ufaransa jana.



# WACHEZAJI 5 BORA ROBO FAINALI QATAR

Robo-fainali ya 2022 haikuwa na upungufu wa uchezaji mzuri wa mtu binafsi na hapa chini tutaangalia kwa haraka wachezaji watano ambao walijitokeza. Hawa ndio wachezaji watano bora ambao walifanya vema katika robo fainali ya Kombe la Dunia la FIFA 2022...

Kipa wa Croatia, Dominik Livakovic, alitinga robo fainali ya Kombe la Dunia la FIFA 2022 baada ya mikwaju ya penalti iliyofanikiwa dhidi ya Japan (aliokoa mara tatu).



Dominik Livakovic

**DOHA, Qatar**

KOMBE la Dunia la FIFA la 2022 limemalizika rasmi jana nchini Qatar na lilituzawadia migengano minne mikali na matokeo kadhaa ya kushtua katika robo-fainali.

Croatia ya Luka Modric iliiondoa Brazil ya Neymar kwa mikwaju ya penalti, huku Morocco ya Achraf Hakimi wakimaliza ndoto ya Cristiano Ronaldo na Ureno ya Kombe la Dunia. Argentina na Ufaransa zilitoka kifua mbele katika mechi nyingine mbili, kwa kuzishinda Uholanzi na England.

Robo-fainali ya 2022 haikuwa na upungufu wa uchezaji mzuri wa mtu binafsi na hapa chini tutaangalia kwa haraka wachezaji watano ambao walijitokeza. Hawa ndio wachezaji watano bora ambao walifanya vema katika robo fainali ya Kombe la Dunia la FIFA 2022...

**#5. Emiliano Martinez - Argentina**

Kipa wa Argentina, Emiliano Martinez, kwa mara nyingine alipanda daraja katika mikwaju ya penalti kwa nchi yake. Martinez alisimamisha penalti mbili muhimu wakati Argentina ilipoilaza Uholanzi katika robo fainali.

Huku mechi ikiwa sawa kwa mabao 2-2 hadi mwisho wa muda wa ziada, Uholanzi na Argentina walianza kwa mikwaju ya penalti iliyojaa wasiwasi. Martinez aliipa Argentina mwanzo wa ndoto, akiokoa ya Virgil van Dijk na Steven Berghuis. Van Dijk alienda kushoto na mkwaju wake wa penalti mtamu, lakini Martinez akauzuia kwa mkono mkali wa kushoto.

Berghuis, kwa upande mwingine, alikwenda kulia. Martinez alikisia uelekeo na akaondoa uokoaji mwingine mzuri ili kuzuia juhudi zake. Lionel Messi, Leandro Paredes, Gonzalo Montiel na Lautaro Martinez walifunga mikwaju yao na kupata ushindi wa 4-3.

**#4. Luka Modric - Croatia**

Nahodha wa Croatia, Luka Modric kwa mara nyingine tena alithibitisha kwamba umri si kitu ila namba kwake, akifunika kila majani kwenye robo fainali dhidi ya Brazil. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, aliamuru hali ya mchezo kwa kutumia pasi zake fupi fupi, akiwa kama beki msaidizi inapohitajika na kwa ujasiri akafunga mkwaju wake wa penalti.

Modric aliamua kusahihisha huku akipiga mkwaju wake wa penalti na akaisaidia Croatia kushinda mikwaju 4-2 katika robo fainali.

Mshindi huyo wa Ballon d'Or 2018 alikamilisha pasi 105 (usahihi wa 91.3%) dhidi ya Brazil katika robo fainali ya Kombe la Dunia la FIFA 2022. Pia alitoa mipira mirefu sita iliyosahihi.



Lionel Messi



**#3. Antoine Griezmann - Ufaransa**

Ufaransa iliitoa England kwa nafasi ya nusu fainali. Mchezo huo ulikuwa wa karibu sana kuhitaji sehemu kubwa, lakini 'Les Bleus' walijizatiti vema kuwafunga 'Simba Watatu' 2-1 katika pambano lao muhimu la robo fainali. Aurelien Tchouameni na Olivier Giroud walipata bao kwa vijana wa Didier Deschamps, lakini ni Antoine Griezmann aliyenyakua tuzo ya mchezaji nyota kwa uchezaji wake wa kusisimua.

Griezmann alitoa pasi mbili za mabao huku Les Bleus wakiishinda England katika robo ya mwisho. Alicheza pasi rahisi ya mraba kwa Tchouameni dakika ya 17 na kiungo huyo akapata kona ya kushoto ya wavu wa England kwa shuti kali la mbali.

Uzuri wa Griezmann ulikuja kujulikana katika dakika ya 78, alipotoa zawadi kwa pasi nzuri aliyompa Giroud aliyefunga mabao mawili.

**#2. Dominik Livakovic - Croatia**

Kipa wa Croatia, Dominik Livakovic, alitinga robo fainali ya Kombe la Dunia la FIFA 2022 baada ya mikwaju ya penalti iliyofanikiwa dhidi ya Japan (aliokoa mara tatu).

Dhidi ya Brazil, aliupeleka mchezo wake hadi kiwango cha juu, na kufanya kuokoa moja baada ya nyingine. Livakovic hakuwahi kusita kukimbilia nje ya safu yake, aliamuru safu yake ya nyuma kwa mamlaka.

Katika mchezo wa wazi, Livakovic aliokoa bao 11, saba kati ya hayo akiyatoa ndani ya maeneo la hatari. Pia alitoa mipira mirefu sita sahihi na kukamilisha pasi 26 (usahihi wa 78.8%). Isingekuwa kwa ushujaa wa Livakovic, Croatia isingefanikiwa kuwabana 'Selecao' kwa sare ya 1-1 baada ya dakika 120 za soka na kusukuma mchezo kwenye mikwaju ya penalti.

Huko, pia, Livakovic alithibitisha uwezo wake, akizima penalti ya Rodrygo. Nikola Vlasic, Lovro Majer, Luka Modric na Mislav Orsic walibadilisha nafasi zao na Marquinhos wa Brazil akagonga nguzo wakati Croatia ikishinda 4-2 kwenye mikwaju.

**#1. Lionel Messi - Argentina**

Nahodha wa Argentina, Lionel Messi, alikuwa mchezaji wao wa kuvutia zaidi katika ushindi wa robo fainali dhidi ya Uholanzi, aliingia kwa pasi na bao moja.

Asisti ya Messi kwa Nahuel Molina katika dakika ya 35 ilikuwa jambo la kupendeza. Akichukua mpira upande wa kulia, Messi aliingia katika nafasi ya kati, akiwakokota wachezaji kadhaa pamoja naye. Wakati Waholanzi wakiwa na shughuli nyingi kujaribu kumzuia, Messi alimwona Molina akiingia katikati ya beki wa kushoto na beki wa kati wa kushoto. Alicheza pasi nzuri ya chini kwenye njia yake, na beki wa kulia alitumia umaliziaji wa hali ya juu kuipa timu yake bao la kuongoza.

Messi alifunga bao mwenyewe katika dakika ya 73, akipiga penalti yake upande wa kulia na kuifanya Argentina kuongoza kwa mabao 2-0. Wout Weghorst aliharibu karamu ya Argentina kwa muda kwa kusukuma mchezo hadi muda wa ziada na kisha mikwaju ya penalti. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 35, pia alitoa penalti hiyo, akiweka kando penalti yake ya ufunguzi na kuwapa 'La Albiceleste' mwanzo walioukuwa wakitafuta.

Katika robo-fainali ya Kombe la Dunia la FIFA 2022, Messi pia alicheza pasi tatu muhimu, akashinda mipira 10 ya chini, akapata faulo nane, na kukamilisha pasi 37 (usahihi wa 82.2%).

SOKA BONGO

# TPLB NA MAKALI ZAIDI KWA WAAMUZI RAUNDI YA PILI



Rais wa TFF, Wallace Karia (kushoto)na Katibu Mkuu wa Shirikisho hilo, Wilfred Kidao. **PICHA: MAKTABA**

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, timu 16 zinazoshiriki ligi zimeanza kucheza mechi za raundi ya pili, lakini Bodi ya Ligi nchini (TPLB), ilikiri kwamba bado kuna changamoto kubwa katika suala zima la waamuzi kwenye ligi hiyo.

Mwenyekiti wa TPLB, Steven Mguto, katika tathmini yake ya mzunguko wa kwanza, amesema kuwa kila kitu kimekwenda vizuri na hakuna malalamiko yoyote kutoka kwa wachezaji na hata klabu kuhusu kucheleweshewa malipo yao, lakini changamoto kubwa imekuwa suala zima la waamuzi.

Katika ligi hiyo ambayo imeingia mzunguko wa pili, Yanga ipo kileleni mwa msimamo baada ya kujikusanyia alama 41 ikifuatiwa na Azam FC yenye pointi 36 mbili mbele ya Simba kabla ya mchezo wao dhidi ya Geita Gold jana.

Baadhi ya waamuzi walionekana kuwa tatizo katika kuzitafsiri sheria 17 za soka ama kwa kutojua au kwa dhamira yao mbaya wenyewe, jambo ambalo lilikuwa kero raundi ya kwanza.

Hadi mzunguko huo unakamilika, timu ya Polisi Tanzania ndiyo inayoburuza mkia hata sasa ikiwa na alama tisa ikifuatiwa na Ruvu Shooting na Ihefu FC zenye pointi 11 na 14 katika nafasi ya 13 na 14, hivyo kwa ligi hiyo inaelekea katika raundi ngumu zaidi, jambo ambalo suala la waamuzi kuvurunda linapaswa kumulikwa zaidi.

Ni ukweli usiopingika waamuzi wa soka nchini wamekuwa chanzo kikubwa kwa baadhi ya timu kumaliza mzunguko wa kwanza katika nafasi zisizostahili. Katika hilo, zipo zilizonufaika kwa kuzawadiwa pointi ambazo zimezifanya kumaliza nafasi za juu, lakini kuna baadhi ambazo zimeporwa alama zao na kujikuta zikimaliza mzunguko wa kwanza kwa kushika nafasi za chini ama za kati.

Hiyo inamaana kama huu ndio ungekuwa mzunguko wa pili, baadhi ya timu zingeshuka daraja ama kwenda kucheza mechi za mchujo 'play off ' kutokana na maamuzi mabovu ya baadhi ya waamuzi, lakini hata bingwa angepatikana pasipo haki kutendeka.

Kwa kuthibitisha hilo, tayari Shirikisho la Soka nchini (TFF), TPLB, pamoja na kamati zake ikiwamo cha Chama cha Waamuzi nchini (FRAT), imeonyesha meno yake kwa kuwafungia baadhi ya waamuzi waliobainika kufinyanga sheria 17 za soka.

Hivyo, kuelekea mzunguko huu wa pili wiki hii pamoja na TPLB kukiri kuwapo tatizo, waamuzi hawana budi kujitathmini zaidi na kugeukia katika kutenda haki na ionekane kweli ikitendeka ili ligi yetu izidi kuwa bora na kuvutia wawekezaji wengi zaidi.

Si hilo tu, bali pia waamuzi wakichezesha kwa haki tutapata wawakilishi bora wa nchi kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu Afrika, ambazo zitabeba jukumu la kwenda kuipeperusha bendera ya Tanzania.

Hivyo, TFF, TPLB na FRAT hawana budi kuongeza makali zaidi kwa waamuzi wanaozifinyanga sheria 17 za soka kwani lengo letu ni kutaka kuona anapatikana bingwa aliyestahili na hata timu zinazoshuka daraja na zile za kucheza mechi za mchujo kuwania kubaki na kupanda Ligi Kuu, ziwe zile zilizostahili kutokana na maamuzi bora na si vinginevyo.

Maamuzi mengi ya ovyo yanayofanywa na waamuzi wetu si makosa ya kibinadamu kama mara kadhaa inavyodaiwa, bali wanadhamiria kwa sababu zao binafsi, hivyo mzunguko huu wa pili TFF na TPLB zisilale maana ndicho kipindi ambacho uvurundwaji mkubwa hufanyika.

Lakini umefika wakati wa waamuzi wetu kujitathmini wenyewe kwamba wanatosha kuifanya kazi hiyo na kuanza kubadilika ili kuwa miongoni mwa wale wanaopewa nafasi mara kwa mara ya kuchezesha michuano ya kimataifa kama zilivyo nchini jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Sudan.

## NJE YA UWANJA

UFARANSA 2022, ni timu ya kwanza tangu Brazil 1998, kuweza kucheza mechi ya fainali ya Kombe la Dunia la Fifa mfululizo baada ya kutwaa taji hilo msimu uliopita michuano hiyo.





# MARCELO BROZOVIC; CHAPOMBE, MVUTA FEGI ALIYEVUNJA REKODI YA KUKIMBIA KOMBE LA DUNIA

**DOHA, Qatar**

MARCELO Brozovic ni kiungo wa kati wa Croatia ambaye alivunja rekodi yake mwenyewe ya kukimbia umbali mrefu zaidi kuwahi kutokea katika mchezo mmoja wa Kombe la Dunia.

Sehemu kubwa ya mafanikio ya Croatia yenye idadi ya watu milioni 3.87 ni safu ya kati ya wachezaji Luka Modric, Mateo Kovacic na Marcelo Brozovic.

Modric amesifiwa sana katika maisha yake ya soka ambayo yamejumuisha mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid, huku Kovacic akionekana kuichezea Chelsea kwenye Ligi Kuu England kila wiki.

Brozovic, ambaye anacheza kiungo cha chini cha Croatia, pia amefurahia kazi ya kuvutia na anang'ara sana kule Inter Milan.

Hata hivyo, mchezaji huyo aliyeicheza mara 82 Croatia, mara kwa mara anafikia kilele kipya, huku akivunja rekodi yake mwenyewe ya Kombe la Dunia ya umbali mkubwa zaidi kuwahi kukimbiwa na mchezaji katika mechi ya hatua ya 16-bora dhidi ya Japan.

Brozovic alifunika umbali wa kilomita 16.7 katika dakika 120 kabla pia hajafunga penalti yake.

Hii ilikuwa mita 400 zaidi ya rekodi ya awali - pia ikishikiliwa na Brozovic - wakati wa ushindi wa Croatia dhidi ya England katika nusu fainali nchini Urusi miaka minne iliyopita alipokimbia kwa umbali wa kilomita 16.3.

Dhidi ya Brazil, alitolewa nje katika dakika ya 114, lakini bado aliweza kukimbia kwa mwendo wa kilomita 15.7.

Stamina yake isiyoyumba inakufanya uamini kuwa huyu ni mwanamichezo aliyejipanga vizuri katika kilele cha mchezo wake.

Lakini Brozovic anaishi maisha tofauti kabisa na inavyotakiwa mwanasoka kuishi.


Makala haya kupitia Sportsmail inamtazama kiungo huyo mahiri na jinsi anavyoendelea kuimarika licha ya maisha yake yenye utata mkubwa nje ya soka.

Ingawa bila shaka ndiye mchezaji fiti zaidi kwenye Kombe la Dunia, Brozovic ni mtu anayependa sana pombe na sigara.

Anajulikana kwa kusherehekea ushindi mkubwa kwa moshi wa sigara na bia.

Kwa mfano, baada ya Croatia kuishinda Ufaransa kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa wakati wa majira ya joto yaliyopita, Brozovic alinaswa akivuta sigara kwenye chumba cha kubadilishia nguo cha Stade de France, huku chupa ya bia ikiwa pembeni yake.

Hii ilikuja baada ya pia kupigwa picha akiwa na mchezaji mwenzake wa Inter Milan, Alex Cordaz baada ya 'Nerazzurri' hao kutwaa taji la Coppa Italia dhidi ya Juventus Mei - huku Brozovic akifurahia akiwa na sigara na bia.



Marcelo

Kiungo huyo katika msimu wake wa tisa na Inter baada ya kuzichezea Hrvatski Dragovoljac, Lokomotiva na Dinamo Zagreb za kwao ameichezea miamba hiyo ya Italia zaidi ya mechi 300.

Hata hivyo, muda wake pale kwenye dimba la San Siro haujawa wa kawaida, ambapo Brozovic alijitoa baada ya kupigwa chini kwenye mechi ya Ligi ya Europa dhidi ya Hapoel Be'er Sheva mwaka 2016, na kusababisha kocha wa wakati huo, Frank de Boer kumtimua kwenye kikosi.

Katika msimu wa 2017-18, pia aliwapigia makofi mashabiki baada ya kuzomewa kutokana na matokeo duni dhidi ya Bologna kwenye Serie A - huku kiungo huyo akitozwa faini kwa kosa hilo.

Kisha, mwaka wa 2020, alipewa adhabu na klabu hiyo alipopigwa marufuku kwa kuendesha gari akiwa amelewa baada ya kukamatwa na polisi akipita kwenye taa nyekundu.

Vile vile, wakati wa Euro 2020, Brozovic alipigwa picha akiwa kwenye mazoezi ya Croatia akinunua sigara saa chache kabla ya nchi yake kufungwa 5-3 na Hispania baada ya muda wa ziada - na kuzua maswali juu ya maisha yake kama mwanasoka wa kimataifa.

Si pombe na sigara pekee zinazomweka matatani Brozovic, kwani aliwahi kuripotiwa anatoka kimapenzi na aliyekuwa mke wa mchezaji mwenzake wa Inter Milan, Mauro Icardi.

Hata hivyo, mwanamke huyo, Wanda Icardi, alikanusha madai hayo.

Brozovic ana tattoo mkononi mwake inayoonyesha pozi lake maarufu - Epic Brozo, na kiungo huyo anasherehekea kila bao analofunga kwa ishara hiyo maalum.

Pia ana tattoo maalum kwenye mkono wake wa kulia - ishara ya mkono kwenye kidevu, inayojulikana kama 'thinking face emoji'.

Kila anapofunga, anapiga picha huku akisherehekea kidole gumba kwenye kidevu chake na kidole chake cha shahada kikielekea shavuni.

Hii inatokana na picha ambayo kiungo huyo alikuwa ameipakia miaka iliyopita kwenye Instagram. Brozovic alikuwa ameketi kwenye gari na wasichana wawili kando yake na kujiweka katika nafasi hiyo maalum - ilizua taharuki kubwa mtandaoni wakati huo.

Pozi hilo limetengeneza jina lake lenyewe - 'Epic Brozo' - ambalo limekuwa Lebo ya Brozovic na hata ana hakimiliki ya neno hilo.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, baadaye alifungua baa huko Velika Gorica, karibu na alikozaliwa Zagreb, iitwayo 'Epic Brozo'.

Baa hiyo inayoendeshwa na Brozovic, baba yake Ivan na dada yake Ema, inafahamika kujengwa kwenye moja ya mapenzi yake makubwa pia akiwa mpenzi wa darts (mchezo wa kulenga vishale).

Kurudi uwanjani, Brozovic pia amekuwa sawa kwa ujanja wa chapa ya biashara inayojulikana kama 'The Crocodile'.

Hili lilionekana kwa mara ya kwanza mwaka wa 2018.

Hii ni pale mchezaji anapoamua kulala chini ya ukuta wakati mpira wa adhabu ndogo ukipigwa.

Katika mechi dhidi ya Barcelona, Luis Suarez alionekana akipanga mpira wa adhabu na alipoenda kuuchukua, Brozovic alijiangusha chini na kuuzuia mpira huo baada ya ukuta kuruka na Suarez kujaribu kupiga.


Hatua hii ilikubaliwa kama 'Mamba' na baadaye mwaka huo, Brozovic alipiga picha akiifanya alama hiyo kama sehemu ya lebo za biashara zake.

Licha ya utukutu wake mkubwa zaidi wa maisha ndani na nje ya uwanja, utimamu wa afya na ubora wa Brozovic haututereki.

Ingawa mara yake ya mwisho kuichezea klabu yake kabla ya Kombe la Dunia ilikuwa katikati ya Septemba kutokana na jeraha la misuli ya paja, Brozovic hajaonyesha dalili zozote za kuwa majeruhi kule Qatar.

## Nukuu

"Ninajisikia furaha sana, kuweza kufanikisha hili, kumaliza safari yangu ya Kombe la Dunia kwa kucheza mchezo wangu wa mwisho kwenye fainali. Ni miaka mingi ijayo na sidhani kama nitaweza. Na kumaliza hivi, ni bora zaidi," **Nahodha wa Argentina, Lionel Messi.**



"Maradona ni soka kwangu. Messi ndiye mchezaji bora zaidi duniani kwa sasa, lakini bado yuko chini ya Diego," **Nyota wa zamani wa Italia, Francesco Totti.**



"Ni mchezaji wa kipekee, mmoja wa wale walionifanya niipende Barcelona, pamoja na Iniesta. Nilikaa naye kwa miaka minne," **Mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele, akizungumza kuvutiwa na Lionel Messi.**



## Soka Bongo

# SIRI WAPINZANI SIMBA, YANGA CAF HIZI HAPA



Kikosi cha Raja Casablanca ya Morocco, mabingwa mara tatu wa Ligi ya Mabingwa na mara mbili Kombe la Shirikisho Afrika. **PICHA: MTANDAO**

**Na Adam Fungamwango**

TAYARI wawakilishi wawili wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Simba na Yanga kila mmoja ameshawajua wapinzani wake kuelekea hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika itakayoanza Februari mwakani.

Simba ambayo itacheza Ligi ya Mabingwa Afrika, imepangwa Kundi C, ikiwa na timu za Horoya ya Guinea, Raja Casablanca ya Morocco na Vipers ya Uganda.

Itaanza kampeni yake ugenini kwa kucheza dhidi ya Horoya ya Guinea, Februari 10, baada ya hapo itacheza dhidi ya Raja Casablaca Uwanja wa Benjamin Mkapa, Februari 17, kabla ya kumaliza mzunguko wa kwanza dhidi ya Vipers nchini Uganda, Februari 24, mwakani.

Yanga ambayo ipo kwenye Kombe la Shirikisho, imepangwa Kundi D, ikiwa na timu za TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Real Bamako ya Mali na US Monastir ya Tunisia.

Nayo pia itaanzia ugenini Februari 12 nchini Tunisia kucheza dhidi ya US Monastir, kabla ya kurudi nchini kucheza dhidi ya TP Mazembe, Februari 19 na kumaliza mzunguko wake wa kwanza, Februari 26, mwakani dhidi ya Real Bamako.

Baada ya droo na ratiba hiyo, katika makala haya tumekusanya taarifa za timu zote zitakazopambana na wawakilishi hao wa Tanzania, ubora, zimefuzu vipi, udhaifu wao na hata uwakilishi wao kwenye ligi za kwao.

**Horoya - Guinea**

Ni timu ambayo mara kwa mara imekuwa ikiingia kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Msimu uliopita ilishika mkia kwenye msimamo wa Kundi B lililoongozwa na Raja Casablanca ambao msimu huu kwa mara ya pili mfululizo wapo kwenye kundi moja tena.

Horoya iliyo Kundi C pamoja na Simba, ikiwa ugenini iliifunga Asec Mimosas nchini Ivory Coast kwa bao 1-0 kwenye mechi ya raundi ya kwanza na sare ya bao 1-1 ikiwa nyumbani na kufuzu hatua ya makundi kwa jumla ya mabao 2-1. Kwenye Ligi Kuu ya Guinea iko kileleni kwa pointi 22, ikicheza mechi nane, sare moja na haijapoteza mechi yoyote ile.

**Raja Casablaca - Morocco**

Ndiyo timu inayoonekana kuwa tishio kwa zingine zote tatu zilizobaki kwenye Kundi C la Ligi ya Mabingwa Afrika. Imeshawahi kutwaa ubingwa wa Afrika mara tatu. Imefanya hivyo 1989, 1997 na 1999, huku mafanikio mengine yakiwa ni kutwaa Kombe la Shirikisho Afrika mara mbili, mwaka 2018 na 2021.

Imefanikiwa kutinga Ligi ya Mabingwa msimu huu, kwa kuitwanga Nigelec ya Niger jumla ya mabao 3-0, ikishinda ugenini 2-0, baadaye nyumbani bao 1-0.

Msimu uliopita ilitolewa kwenye hatua ya nusu fainali kwa jumla ya mabao 3-2 dhidi ya Al Ahly ya Misri, ikifungwa ugenini mabao 2-1 na kulazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani.

Al Ahly iliyofanikiwa kuitoa Raja Casabanca, ilifungwa fainali na mahasimu wao wa jadi, Wydad Casablaca mabao 2-0. Wydad ndiyo mabingwa watetezi. Kwenye Ligi Kuu nchini Morocco inakamata nafasi ya tano mpaka sasa, ikicheza mechi nane, kushinda tatu, sare tatu, kupoteza mbili ikiwa na pointi 12.

**Vipers FC - Uganda**

Kwenye kundi hili kuna timu ngeni katika michuano hii, nayo ni Vipers ya Uganda. Watanzania wengi walianza kuiona kwenye Tamasha la Siku ya Mwananchi ilipocheza dhidi ya Yanga Uwanja wa Benjamin Mkapa, wakawateketeza wenyeji wao mabao 2-0.

Imewashtua wengi kwa kuiondosha kwenye Ligi ya Mabingwa, timu tishio Afrika, TP Mazembe kwa mikwaju 4-2 ya penalti nchini DR Congo, baada ya suluhu kwenye mechi zote mbili. Kwenye Ligi Kuu nchini Uganda, inashika nafasi ya pili kwa pointi 27, ikiongozwa na KCCA yenye pointi 29, zote zikicheza mechi 13.

**US Monastir - Tunisia**

Moja ya sifa ya timu hii iliyoko Kundi D pamoja na Yanga, Kombe la Shirikisho barani Afrika ni kwamba iliifungasha virago bingwa mtetezi, RS Berkane ya Morocco.

Imeingia hatua ya makundi baada ya kuichapa RS Berkane bao 1-0 nyumbani, na kwenda kukomalia suluhu ugenini. Ilianzia Ligi ya Mabingwa kama Yanga, lakini ilichomolewa huko na Al Ahly ya Misri kwa kipigo cha mabao 4-0, ikichapwa 3-0 nyumbani na 1-0 ugenini.

Kwa sasa inaongoza Ligi Kuu ya Tunisia kwenye Kundi B, ikiwa na pointi 13, ikicheza mechi sita, ikishinda nne, sare moja na kupoteza moja. Desemba 14 kwenye mechi ya ligi, iliichapa timu iliyotolewa na Yanga kwenye michuano hii, Club African kwa mabao 3-0.

**Real Bamako - Mali**

Ilianza safari yake kwenye michuano hii hii kwa kuiondoa Douanes ya Burkina Faso kwa penalti 3-1 ikiwa nyumbani, baada ya suluhu kwenye mechi zote mbili.

Ikaichapa Hearts of Oak ya Ghana jumla ya mabao 3-1, ikishinda 3-0 nyumbani na kupigwa 1-0 ugenini.

Ilitinga hatua ya makundi kwa kuiangamiza Royal Leopards ya Eswatini mabao 4-2, ikitoka sare ya bao 1-1 ugenini na kushinda nyumbani mabao 3-1.

Ina pointi 14 sawa na Djoliba kwenye Ligi Kuu nchini Mali, lakini inashika nafasi ya pili kwa alfabeti, kwani inalingana kila kitu na timu hiyo, zote zikicheza mechi sita, kushinda nne, sare mbili mabao tisa, na kuruhusu matatu.

**TP Mazembe - DR Congo**

Ndiyo timu yenye mafanikio zaidi kwenye kundi hili katika michuano ya kimataifa. Imetwaa ubingwa wa Afrika mara tano na Kombe la Shirikisho mara mbili 2016 na 2017.

Ilifurushwa kwenye Ligi ya Mabingwa na Vipers ya Uganda kwa penalti 4-2 ikiwa nyumbani, baada ya suluhu mechi zote mbili. Hasira zake zilimalizikia kwa Royal AM ya Afrika Kusini kwa kuichapa nyumbani 2-0 na bao 1-0 ugenini, ikakata tiketi ya kutinga hatua ya makundi.

TP Mazembe inakamata nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu nchini DR Congo, ikiwa na pointi 15 kwa mechi tisa ilizocheza.


**NDANI YA 18**



KIPA wa Morocco, Yassine Bounou, amekuwa mlinda mlango wa kwanza kutoka Afrika kuweza kucheza mechi tatu za Kombe la Dunia bila kuruhusu bao.

# FUNDI WA WIKI...



| | |
|---|---|
| JINA KAMILI: | Luka Modric |
| KUZALIWA: | Septemba 9, 1985 (miaka 37) |
| ALIPOZALIWA: | Zadar, SR Croatia, SFR Yugoslavia |
| KIMO: | 1.72 m (5 ft 8 in) |
| NAFASI: | Kiungo |
| KLABU: | Real Madrid |
| JEZI: | Namba 10 |

## BADO YUPO SANA....

*"Ninahitaji kwenda hatua kwa hatua, ninafurahia kucheza timu ya taifa," anasema Modric ambaye amecheza dakika 656 kati ya 690 akiwa na Croatia Kombe la Dunia Qatar. "Bado ninahisi ninaweza kucheza kwa kiwango cha juu. Ninahitaji kuendelea angalau hadi michuano ya Euro 2024."*

# MODRIC

# WACHEZAJI 10 WENYE MAPATO MAKUBWA 2022

**LONDON, England**

INGAWA nafasi za juu za kwanza si tena za Lionel Messi au Cristiano Ronaldo, nyota hao wawili mashuhuri wa soka bado wanatarajiwa kupata angalau dola milioni 100 msimu huu, na hivyo kuchangia rekodi ya kukusanya dola milioni 652 kwa wachezaji 10 waliopata fedha nyingi zaidi, kwa mujibu wa Jarida la Forbes.

Hii haimaanishi kuwa wachezaji hao wawili wenye sifa zaidi katika soka wamepunguza uwezo wao wa mapato, haswa nje ya uwanja, katika siku za hivi karibuni za maisha yao ya soka.

Messi mwenye umri wa miaka 35, anatarajiwa kuingiza dola milioni 110 msimu huu (dola milioni 55 nje ya uwanja) huku Ronaldo mwenye miaka 37, akipangiwa kupata dola milioni 100 (dola milioni 60 nje ya uwanja, zaidi ya mchezaji mwingine yeyote).

Wote wawili hao walitia saini mikataba ya faida kubwa na makampuni ya fedha za siri katika mwaka uliopita, huku Messi akipata dola milioni 20 kila mwaka kutoka Socios.com na Ronaldo akishirikiana na Binance kwa kiasi ambacho hakijawekwa wazi.

Kwa jumla, wachezaji kumi wa soka wanaolipwa zaidi wanatarajiwa kukusanya mapato ya kabla ya ushuru ya dola milioni 652 msimu huu, juu ya asilimia 11 kutoka dola milioni 585 mwaka jana. Wachezaji walio katika nafasi tatu za juu wanachangia zaidi ya asilimia 50 ya takwimu hiyo kwa mujibu wa Forbes.



Mbappe

**10. Kevin De Bruyne - Dola Mil. 29**

Licha ya kusaini na Roc Nation mnamo 2019, De Bruyne na baba yake waliongoza mazungumzo ambayo yalizaa mkataba wake mpya na Manchester City, kwa kutumia usaidizi wa Kampuni ya Data ya Analytics FC katika mchakato huo.

Ana mikataba 11 ya chapa ambayo ni pamoja na Nike, Wow Hydrate, Credit Karma na Therabody.

**9. Andrés Iniesta - Dola Mil. 30**

Mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona mwenye umri wa miaka 38, alizindua chapa yake ya mavazi ya michezo mnamo Septemba mwaka huu.

Lebo hiyo inaitwa Capitten, ilianza kwa uzinduzi wa toleo pungufu la uondoaji sahihi na inalenga soko la Japan. Iniesta pia ameshirikishwa katika filamu kuhusu Kombe la Dunia la FIFA.

**8. Eden Hazard - Dola Mil. 31**

Muda wa kukatisha tamaa wa Hazard akiwa na Real Madrid - mabao sita katika mechi 72 za LaLiga na Ligi ya Mabingwa ulioenea kwa misimu minne umechochea tetesi za mchezaji huyo kurejea Chelsea.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, hapo awali alionekana kwenye jarida la mchezo wa video wa FIFA 20 wa EA Sports.

**7. Robert Lewandowski - Dola Mil. 35**

Lewandowski amekuwa mwepesi kuhalalisha ada ya uhamisho ya takriban dola milioni 45 ambayo FC Barcelona ililipa mwaka 2022 kumnunua kutoka Bayern Munich, akiwa na mabao 12 katika mechi kumi alizocheza.

Alisitisha makubaliano ya muda mrefu na Huawei kulingana na ripoti kwamba kampuni hiyo iliunga mkono uvamizi wa Urusi nchini Ukraine.

**6. Erling Haaland - Dola Mil. 39**

Forbes inakadiria kuwa Haaland hupokea dola milioni nne kila mwaka kutoka kwa wafadhili kama Hyperice, Samsung na Viaplay, lakini idadi hiyo inakaribia kuongezeka.

Ripoti zinaonyesha kuwa mkataba unaofuata wa viatu wa Haaland unaweza kuwa na thamani ya dola milioni 18 kila mwaka. Mkataba wake wa awali na Nike uliisha mwaka huu.

**5. Mohamed Salah - Dola Mil. 53**

Baada ya kampeni nzuri ambayo ilikaribia kuipa Liverpool taji la Ligi Kuu England siku ya mwisho ya msimu, Salah alitawazwa Mwanasoka Bora wa Mwaka kwa Wanaume wa England na Mchezaji Bora wa Msimu, pia alipokea Tuzo ya Kiatu cha Dhahabu cha ligi hiyo.

Mnamo Julai, alisaini nyongeza ya miaka mitatu kusalia na Liverpool hadi 2025, na anasalia kuwa mmoja wa nyota wakubwa wa kimataifa wa Adidas.

**4. Neymar Jr. - Dola Mil. 87**

Neymar aliweka historia mwaka 2017 kwa uhamisho wa rekodi wa dola milioni 263 kwenda Paris Saint-Germain. Mnamo Mei 2021, aliongeza mkataba hadi 2025, mbali na kusaidia kumshawishi Messi kujiunga na timu hiyo baadaye mwaka huo.

Neymar anaendelea kufanya vema kama mchezaji, akiongeza Kundi la Ooredoo kama mfadhili kabla ya Kombe la Dunia.

**3. Cristiano Ronaldo - Dola Mil. 100**

Licha ya kupungua kwa kiwango chake cha kucheza, Ronaldo ndiye mchezaji wa soka anayelipwa fedha nyingi zaidi nje ya uwanja kutokana na washirika kama Nike, Herbalife na Livescore.

Ripoti zinaonyesha Ronaldo anatafuta klabu mpya wakati wa dirisha la usajili la Januari, ili kumpa nafasi ya kurejea kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya (Manchester United haikufuzu kwa 2022-23). Pia anajivunia wafuasi milioni 486 kwenye Instagram.

2. Lionel Messi - Dola Mil. 120

Messi tayari anapokea mshahara wa mfalme nje ya uwanja, lakini wataalamu wa sekta hiyo wanapendekeza kwamba idadi hiyo inaweza kukua kwa asilimia 20. Inasemekana pia kuwa anafikiria kurejea FC Barcelona, ambapo aliitumikia miaka 17 ya kwanza ya kazi yake, mnamo 2023.

**1. Kylian Mbappe - Dola Mil. 128**

Baada ya kukusanya tuzo tatu kati ya nne zilizopita za Mchezaji Bora wa Mwaka wa Ligue 1, Mbappe amejidhihirisha kama uso wa soka la Ufaransa. Amebadilisha ushawishi huo hivi karibuni.

Mbappe alikataa kushiriki katika upigaji picha na shughuli nyingine za wafadhili kupinga makubaliano ya haki za picha ya Timu ya Taifa ya Ufaransa na wachezaji wake; Shirikisho la Soka la Ufaransa limetangaza kulipitia suala hilo.

## JE, WAJUA?

KIPA wa Ufaransa, Hugo Lloris, aliokoa michomo sita dhidi ya England kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Dunia, ambayo ni mingi zaidi kufanywa na kipa yeyote katika michuano hiyo tangu alipofanya yeye mwenyewe dhidi ya Afrika Kusini wakati wa Kombe la Dunia 2010.





## Kampuni yachochea ongezeko uzalishaji wa maziwa

Na Grace Mwakalinga, RUNGWE

UPATIKANAJI wa mbegu bora za madume ya ng'ombe kwa wafugaji wilayani Rungwe, kumechochea ongezeko kwa uzalishaji maziwa kufikia zaidi ya lita 200,000 kwa siku na kuingizwa sokoni.

Mwenyekiti wa Muungano wa Chama cha Wafugaji wilayani Rungwe (MUHAMARU), Asha Lukaja, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na Nipashe kuhusu hatua walizochukua ikiwa ni siku kadhaa kupita baada ya kufanya kikao cha kujadili mambo ya kufanya ili kukuza uzalishaji wa maziwa wilayani humo.

Alisema mafanikio ya upatikanaji wa mbegu bora za madume ni kupata elimu ya kuzalishaji pamoja na masoko, kabla ya elimu hiyo walikuwa wakikabiliwa na tatizo la masoko na mbegu bora, kiwanda cha maziwa cha Asasi kimewapatia madume ya mbegu bora za ng'ombe ambayo yamesaidia ongezeko la majike ambayo yamekuwa kochocheo kikubwa cha ongezeko la uzalishaji maziwa.

"Licha ya ongezeko la uzalishaji wa maziwa na uwepo wa masoko ya uhakika bado tatizo kwa baadhi ya wafugaji kuingiza sokoni maziwa yasiyokuwa na ubora jambo linalochangia kuchafua na kutia doa maziwa yanayozalishwa wilayani Rungwe," alisema Lukaja.

Miongoni mwa wafugaji wilayani Rungwe, Fadhili Mbilinyi alisema kuwapo kwa kampuni ya ununuzi wa maziwa wilayani Rungwe kumeleta tija wa wafugaji kuongeza uzalishaji na kufuga kisasa.

Alisema kwa sasa wanazalisha kiasi kikubwa cha maziwa na uhakika wa upatikanaji wa soko ndani na nje ya wilaya hiyo.

Ofisa Mifugo Wilaya ya Rungwe, Dk. Dennis Kamily, alisema wafugaji wengi hawapendi kuwatumia maofisa ugani kujifunza namna bora ya kuzalisha maziwa bila kutumia vyakula visivyo salama kwa ng'ombe.

Mkaguzi wa Maziwa Wilaya ya Rungwe, Henry Mokiwa, alisema asilimia 20 ya maziwa yanayozalishwa na wafugaji wilayani humo yanakosa ubora kutokana na baadhi ya wafugaji kuongeza maji.

"Ukamuaji wa maziwa kiholela kwa baadhi ya wafugaji kunachangia kuzalisha bakteria 500 hadi 1,000 kila baada ya saa tatu na kusababisha madhara kwa watumiaji na kushauri wafugaji kuwatumia maofisa ugani ili kuboresha sekta ya maziwa nchini," alisema Mokiwa.

# Wajasiriamali walipiwa gharama kuthibitisha bidhaa

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

SERIKALI imeendelea kuwalipia wajasirimali wadogo gharama zote za kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha ikiwamo ya huduma za ukaguzi, upimaji na ufuatiliaji wake bila malipo ili kuwawezesha wajasiriamali wote kuingiza sokoni zinazokidhi vigezo vyenye ubora na kuonya zisizokidhi viwango hazipaswi kuingizwa sokoni.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Lazaro Msasalaga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki mkoani hapa kwenye hafla ya kuwatunuku vyeti na leseni za uthibitisho wa ubora wajasiriamali 59 kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi waliokidhi vigezo vya ubora wa bidhaa zao.

Alisema gharama zinazolipiwa na serikali kuwawezesha wajasiriamali wadogo kusajili bidhaa zao ni upimaji wa sampuli kwenye maabara za TBS, ukaguzi wa kiwanda, ufuatiliaji viwandani na sokoni pamoja na uhuishaji wa leseni na vyeti kila mwaka.

"Serikali imebeba jukumu la kulipigia gharama zote za ukaguzi na upimaji kwa kipindi cha miaka mitatu, utaratibu wa kuanzia kulipia wao wenyewe umeshawekwa kupitia sera ya madeni ya shirika ambapo hata baada ya miaka mitatu kufika, mjasiriamali anaweza kuendelea kulipiwa na serikali endapo itathibitika kwamba hajapata uwezo huo baada ya tathmini kufanyika," alieleza Msasalaga.

Alifafanua kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Magharibi, leseni na vyeti 39 sawa na asilimia 66.1% vilitolewa kwa wajasiriamali wadogo huku akisema walihudumiwa na shirika bila malipo.

Akizungumza na wajasiriamali waliotunukiwa vyeti na leseni hizo, Katibu Tawala Msaidizi Uwekezaji Viwanda na Biashara Mkoa wa Mbeya, Mwajabu Nyamkomora ambaye bidhaa yake imethibitishwa na TBS anajenga imani kwa wanunuzi hivyo ni rahisi kuingia sokoni na kumudu soko la ushindani.

Nyamkomora aliwapongeza waliopata vyeti na leseni hizo na kuwataka kuwa mabalozi wazuri kwa wengine wanaoingiza sokoni bidhaa ambazo hazijakidhi viwango kuhakikisha zinathibitishwa na TBS ili waweze kuingia kwenye masoko ya ushindani ndani na nje ya nchi. "Leseni na vyeti mlivyopata zitasaidia bidhaa zenu kukubalika katika masoko, sasa hivi tuna masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi nyingine lakini tulishindwa kuyafikia kutokana na vigezo kutokamilika lakini kupata nembo ya TBS utaweza kuingia sehemu yoyote kuuza bidhaa yako," alisema Nyamkomora.

Baadhi ya waliopata vyeti na leseni hizo waliipongeza serikali kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa kuandaa hafla hiyo na kutoa wito kwa shirika hilo kujenga mazingira rafiki kwao na kutoa elimu juu ya umuhimu wa bidhaa zao kuwa na nembo ya TBS. Mkurugenzi wa Double Natural Product, Damas Madembwe, aliishukuru serikali kupitia SIDO na TBS kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa utoaji leseni bila malipo na kuwashauri wajasiriamali kuondokana na dhana potofu kwamba hawawezi kupata huduma hiyo bila malipo.

Glory Urio, kutoka Kampuni ya Al-Shawafi Trading, alisema baadhi yao wamekuwa wakiwakwepa maofisa wa TBS wanapowatembelea wakihofia kufungiwa bidhaa zao na kuwaomba TBS kuwa marafiki.




Kaimu Meneja wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Kanda ya Magharibi Kigoma, Rodney Alananga, akizungumza na viongozi wa shirika hilo pamoja wazalishaji wa bidhaa mbalimbali kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Magharibi (hawapo pichani) ambao walipatiwa vyeti na leseni za kutumia alama ya ubora mwishoni mwa wiki jijini Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wazee waomba shule vidato vya tano na sita ziongezwe

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

WAZEE wadau wa maendeleo mkoani hapo (WAMAMBE), wameiomba serikali kuanzisha shule za kidato vya tano na sita zisizopungua 10 na kwa Jiji la Mbeya zisizopungua 20 ifikapo mwaka 2025 ili watoto wa mkoa huo wanufaike na elimu ya juu.

Walitoa kauli hiyo jana kwenye Ofisi za Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya walipomtembelea na kumpongeza kwa kuchaguliwa mwenyekiti mpya, Dk. Stephen Mwakajumilo.

Walisema wazee wadau wa maendeleo ni chachu katika kuleta mabadiliko mkoani humo watahakikisha wanashirikiana na viongozi wa serikali na chama tawala kushauri na kukosoa pale mambo yanapokwama.

Mwenyekiti wa wazee hao, Mwaiseje Polisya, alisema wameandaa vipaumbele vyao ambavyo serikali na chama ikizingatia mkoa utapiga hatua kubwa ya maendeleo.

Walimweleza Dk. Mwakajumilo vipaumbele hivyo ni kuhakikisha ujenzi wa umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi ili kusonga mbele, kuimarisha maridhiano na ushirikiano wa vyama vya siasa.

Alisema wazee hao wanatamani kuona ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Tukuyu-Lwangwa- Katumba na Mbambo-Ipinda unakamilika ifikapo mwaka 2025 licha ya kwamba tayari umeanza lakini unasuasua.

"Pia tunatamani kuboreshewa reli ya Tazara kuwa ya umeme kama ilivyo reli mpya inayojengwa kutoka jijini Dar es Salaam kwenda Mwanza ili kuongeza kasi ya usafiri na usafirishaji Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kuchochea maendeleo," alisema Polisya. Aliongeza kuwa wanatamani sekta ya usafiri na usafirishaji mkoani Mbeya inaendelea kuimarishwa kwa kujengewa miundombinu rafiki kama kujenga upya barabara ya Tanzania- Zambia (TANZAM) kuanzia Nsalaga mpaka Songwe ulipo Uwanja wa Ndege kwa upana wa njia nne ili kuondoa msongamano wa magari jijini Mbeya na kuleta mandhari mazuri kwa jiji.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo, alisema, wazee hao wamempa nguvu ya kutekeleza majukumu yake ikiwamo kutoa ushauri kwa serikali mambo ya kufanya ili kuwaletea maendeleo wakazi wa Mbeya.

Alisema hamfumbii macho kiongozi yeyote wa serikali anayefanya uzembe mkoani humo atasimamia na kutekeleza kikamilifu matakwa ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Mambo yanabadilika sana zamani wanasiasa tulikuwa tunaogopa kuwashauri viongozi wa serikali pindi wanapokosea, lakini kukua kwa demokrasia kumetupa nguvu ya kukemea na kuonya pale mambo yanapokwenda tofauti ndani ya chama na kwa watumishi wa serikali," alisema Dk. Mwakajumilo.

Mjumbe wa wazee, Allan Mwaigaga alisema wataendelea kuwashauri viongozi wa mkoa huo ili waweze kutekeleza na kusimamia vyema majukumu yake ikiwamo ujenzi wa miradi mbalimbali kwenye sekta ya Afya, maji, barabara, elimu na kilimo.





# Masauni atatua mgogoro wa ardhi uliodumu kwa miaka 44

**Na Felix Mwagara,** KONDOA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni amemaliza mgogoro wa ardhi ulioanza mwaka 1978 kati ya Gereza la Mifugo la King'ang'a na wananchi wa vijiji vya Kata ya Kingale wilayani Kondoa mkoani Dodoma.

Akifuatana na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, wataalamu wa ardhi kutoka Ofisi ya Kamishna wa Ardhi pamoja na maofisa wa Jeshi la Magereza, Masauni aliwasili kwenye gereza hilo lililoko Mtaa wa Chemchem jana na kufanya kikao cha ndani kwa zaidi ya saa mbili.

Baada ya kikao hicho, kabla ya Waziri Masauni kuzungumza na wananchi wa kata hiyo, alitembelea na kufanya ukaguzi wa eneo la mgogoro na kuona eneo linalogombewa na pande zote mbili kwa miaka yote hiyo.

Akizungumza na mamia ya wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Kijiji cha Iyori, Waziri Masauni alitoa pole kwa wananchi hao kutokana na mgogoro huo uliodumu kwa miaka mingi na kuwaambia kuwa mgogoro huu umefikia mwisho na ile kauli ya kusema kuwa jambo hili limeshindikana miaka nenda rudi, sasa itakuwa historia iliyopitwa na wakati.

"Kabla ya kufika hapa tulikuwa na kikao, tumekaa, tumejadili kwa kina, na mimi ndio nimepewa dhamana hii ya kulisimamia Jeshi la Magereza kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, na kwa maelekezo ambayo nimepewa na Mheshimiwa Rais kuhusu utatuzi na uondoaji wa changamoto za wananchi ikiwamo hapa Kondoa, tumepeana muda wa wiki mbili.

"Tarehe 30, mwezi huu, serikali inataka kulifunga rasmi jambo hili, liishe kwa kuzingatia maslahi mapana ya wananchi mliopo hapa ambao mnatumia ardhi ile kwa kilimo, muweze kupata ardhi ya kuendeleza shughuli zenu za kilimo bila bugudha, bila usumbufu wowote.

"Pia tumekubaliana katika kipindi cha siku hizi za wiki mbili, kupitia wataalamu wetu, tukae tufanye tathmini ya kina uhitaji wa matumizi kati yenu ninyi na Magereza ili tuweze kutoa mgawo utakaokidhi pande zote mbili.

"Ninaombeni sana mapendekezo na uamuzi huo utakapotoka muunge mkono kwa sababu utakuwa umezingatia sana maslahi yenu wananchi wa Wilaya ya Kondoa," alisema.

Waziri Masauni alisema baada ya uamuzi huo, kuanzia sasa wananchi hao wataendelea kufanya shughuli zao za kilimo na watatumia fursa nyingi ambazo serikali imezitoa, ikiwamo kuiongezea bajeti kwa kiwango kikubwa ya sekta ya kilimo.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema mgogoro huo umeukuta ofisi kwake, akikiri ni wa muda mrefu na mara kadhaa umeshughulikiwa pasipo na ufumbuzi, hivyo kwa ujio wa Waziri Masauni mgogoro huo utamalizwa.

"Mheshimiwa Waziri, jambo alilokuwa amelisema mheshimiwa mbunge ni la muda mrefu, kwa namna moja au nyingine makundi mbalimbali yamekuwa yakishughulikia hayakufanikiwa, hawakufika mwisho, jambo hili linawahusisha Magereza na wapo hapa," alisema Senyamule. Mwakilishi wa Kamishna Jenerali wa Magereza, Kaimu Kamishna wa Magereza Huduma za Urekebu, Omary Salum, alisema jambo hilo linawakwamisha kiutendaji na hawapendi mgogoro huo uendelee.

Awali wananchi walitoa malalamiko yao na mateso waliyopitia katika kipindi cha miaka yote hiyo na kumweleza waziri huyo wamechoka na wanataka ufumbuzi wa mgogoro huo ambao wanadai Magereza imechukua ardhi yao. "Magereza wamevuka mpaka kisheria na kuvamia eneo letu na licha ya viongozi tofauti kujaribu kutafuta suluhu ya mgogoro huo bila ya mafanikio yoyote, na kusababisha wanakijiji kukosa mahali pa kulima na kulisha mifugo," alisema mwanakijiji Shaban Mohamedi.

Gereza la King'ang'a lilianzishwa Februari 25, 1975 kama shamba la Magereza la mifugo baada ya kupata ardhi kutoka kwenye Kitongoji cha Chemchem na upimaji wa awali wa eneo kwa minajili ya kuanzisha mipaka ya Gereza ulianza Juni 25, 1978 na kumalizika Oktoba 1978.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Iyori, Kata ya Kingale, wilayani Kondoa mkoani Dodoma jana, kuhusu mgogoro wa ardhi wa Gereza la Mifugo la King'ang'a na wananchi uliodumu kwa miaka 44. **PICHA: WIZARA MAMBO YA NDANI**

# CHAVITA yataka watoto wote kutambuliwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHAMA cha Wasioona Mkoa wa Dodoma (CHAVITA) kimesema wazazi na walezi wanapaswa kushirikiana na serikali ili kuhakikisha watoto wote wanatambuliwa na kuandikishwa kwa ajili ya kupelekwa shule mwaka 2023.

Katibu wa Chama cha Wasioona Mkoa wa Dodoma, Enock Mbawa, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo.

Alisema ni muhimu watoto wakatambuliwa ili wapate haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Aidha, alisema serikali kwa kushirikiana na maofisa elimu kata, walimu wakuu wa shule za msingi pamoja na viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu, wameendesha kuwabaini watoto wenye ulemavu ambao umri wao wanatakiwa kuandikishwa shule.

"Wazazi msiwafiche watoto wanaostahili kupata haki ya kusoma bali watoe ushirikiano wa kuhakikisha wanapata masomo kama ilivyo kwa wengine wasio na ulemavu," alisema.

Alisema kuwa watoto hao wakiendelea kufungiwa majumbani wanawaongezea ukatili mkubwa kwenye maisha yao ikiwamo umaskini utakaomfanya pia kuwa ombaomba hata atakapokuwa mtu mzima.

"Hasara zingine ambazo zitakazosababisha mtoto mwenye ulemavu kumkosesha elimu ni pamoja na kukosa stahiki zake maisha na kumsababishia kuwa mkatili pia."

"Hata hivyo Chama cha Wasioona Mkoa wa Dodoma tunakila sababu ya kulishukuru Kanisa la Free Pentecostal Church Tanzania (FPCT) kupitia mradi wake wa elimu jumuishi kwa kusaidia uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia shuleni kwa watoto wenye ulemavu," alisema.

Naye mratibu wa mradi wa elimu jumuishi kupitia kanisa la FPCT, Jeni Mgidange, aliiomba jamii kuwafichua wazazi na walezi ambao wamekuwa tabia ya kuwaficha watoto pindi serikali wanapohitaji kuwatambua kwa ajili ya kuwapatia huduma mbalimbali zikiwamo za elimu na kiafya.

Alisema elimu bado inahitajika kwa wazazi wanaoishi na watoto hao baadhi yao kwa kufikiri kuwa wakiwasomesha na kumwendeleza kielimu watakuwa wakipoteza mali na fedha zao kwa madai kuwa watapata hasara tofauti na kama watoto wengine wasiokuwa na ulemavu.

Mgidange alisema kutokana na dhana hiyo potofu serikali kwa kushirikiana na jamii iendelee kutoa elimu ambayo wazazi na walezi wenye watoto hao waweze kubadilika na mtizamo huo potofu ili wasiendelee kuwaficha na wakawakosesha kupata huduma hizo muhimu.

# Watakaovujisha siri za Jeshi Magereza kukiona cha moto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza limesema litawachukulia hatua kali maofisa, askari na watumishi watakaovujisha siri za jeshi hilo ikiwamo nyaraka muhimu za kumbukumbu ndani ya taasisi hiyo.

Kaimu Kamishna wa Utawala na Rasilimali Watu wa Jeshi hilo, DCP Jeremiah Katungu, alitoa kauli hiyo alipokuwa akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa askari na watumishi juu ya namna ya kutunza kumbukumbu jijini hapo.

Alisema jeshi hilo limeamua kuitisha mafunzo hayo ili kuwapa elimu ya namna ya kutunza kumbukumbu za serikali.

"Nisingependa kusikia siri au nyaraka za serikali zinatoka nje katumie mafunzo hayo vizuri kivitendo," alisema Katungu.

Alisema anaamini baada ya mafunzo hayo maofisa wote watakuwa na uwezo wa kutunza siri na kumbukumbu za serikali na kuwa makini na mafunzo yanayoendelea.

Alifafanua zaidi ya kuwa hivi sasa wanakwenda kuwa na mfumo wa kisasa wa utunzaji kumbukumbu badala ya ule wa zamani ambao walikuwa wakitumia kuhifadhi nyaraka.

Alisema mafunzo hayo yatasaidia kuajiri watu katika sekta hiyo ambao wamechunguzwa kabla ya kuingia katika kitengo hicho.

Aliwasisitiza maofisa hao kuwa makini na kinachofundishwa ili waweze kwenda kukitumia katika ofisi zao.

Kadhalika alisema wanajipanga kujenga chumba maalum kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu ili ziweze kuwa salama na zitumike na wengine.

Alisema ujenzi huo utaanza mara moja ili kuhakikisha wanakuwa na sehemu maalum kwa ajili ya kutunza kumbukumbu.

Naye Kaimu Kamishna wa huduma za urekebu, Omary Salum, alisema jumla ya washiriki 136 wamehudhuria mafunzo hayo ambayo yanatolewa na wakufunzi kutoka serikalini ili kuhakikisha wanaimarika katika kitengo hiko.

Alisema washiriki wametoka katika mikoa mbalimbali kupata elimu ya utunzaji kumbukumbu katika ofisi za serikali.



## Mbunge mteule Jimbo la Amani atangazwa rasmi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Taifa ya Uchaguzi NEC imemtangaza Abdul Yussuf Maalim kuwa mbunge mteule wa Jimbo la Amani baada ya kushinda katika uchaguzi huo mdogo uliofanyika juzi.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo msimamizi wa uchaguzi wa jimbo hilo, Safia Iddi Muhammed, alisema mbunge huyo kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) amepata kura 4,242 sawa na asilimia 84.1 ya kura zote zilizopigwa katika j imbo hilo.

Mteule alimshinda mpinzani wake wa Chama cha ACT-Wazalendo, Muhammed Khamis, ambaye alipata kura 728 sawa na asilimia 14.4 ya kura zote zilizopigwa.

Jumla ya wapigakura 9,919 walijiandikisha katika daftari la wapigakura, lakini waliopigakura ni 542 sawa na asilimia 98.4 huku kura zilizoharibika zikiwa 84.

Jumla ya vyama 14 vilisimamisha wagombea katika uchaguzi vikiwamo SAU, UPDP, UDP, DP, CUF, TLP NA Demokrasia Makini.

Mbunge huyo mteule, alisema kazi kubwa iliyo mbele yake kwa sasa ni kuwatumikia wananchi wa jimbo hilo bila ya kujali itikadi za kisiasa.

Kabla ya matokeo hayo mgombea wa Chama cha ACT-Wazalendo, Muhammed Khamis, alilalamika kuwa uchaguzi huo ulijaa dosari ikiwamo kutawaliwa na mamluki ambao hawakustahiki kupiga kura.

Tuhuma hizo zilipingwa na Tume ya Uchaguzi ikisema watu wote wenye sifa ya kupiga kura katika jimbo hilo ndiyo waliopiga kura.

# ZRB kuwabana wasiotoa, kudai risiti ununuzi bidhaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISHNA wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), Yusuphu Juma Mwenda, amewataka wananchi wa Kijiji cha Kijini Matemwe, Mkoa wa Kaskazini Unguja kuhakikisha kila wanachokinunua wanadai risiti ili kuipa uwezo serikali kutoa huduma mbalimbali za kimaendeleo.

Aliyasema hayo jana visiwani humo wakati akitoa msaada wa vyakula kwa wananchi wa kijiji hicho ikiwa ni mwezi wa kuwashukuru walipa kodi na kuwafanya wawe na furaha.

Alisema kitu chochote wanachokinunua ndani yake kuna kodi inayoiwezesha serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa barabara, shule, huduma ya majisafi na salama na vituo vya afya.

Alisema bodi hiyo inawajali walipakodi wake na ndio maana imeamua kutoa msaada wa vyakula ikiwamo mafuta, unga wa ngano, sukari na mchele kwa kaya zote 583 wananchi wa kijiji hicho wanaokabiliwa na hali duni ya umaskini.

Alisema ikiwa wananchi watatekeleza kwa vitendo kudai risiti kwa kila unununzi wanayofanya itaipa uwezo serikali kuwasaidia kupata huduma muhimu na kuiwezesha serikali kutimiza wajibu wake.

"Lazima mfahamu kuwa msipodai risiti wakati mnapofanya manununzi mnainyima uwezo serikali ya Zanzibar kutoa huduma vizuri ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara maji, elimu afya na mingine muhimu katika maeneo ya mjini na vijijini," alisema.

Alisema kitendo cha kutodai risiti ni kuikosesha serikali mapato na kuwanufaisha wafanyabiashara kwa sababu bila ya mapato serikali haitoweza kuleta maendeleo.

Sheha wa Shehia hiyo, Msiyakwe Makame Haji, alishukuru ZRB kwa msaada huo ambao utasaidia wananchi kuwapunguzia ukali wa maisha.

Aliomba bodi hiyo kufika tena kijijini hapo kutoa elimu ya kodi kwasababu wananchi wengi hawana elimu hiyo hawadai risiti wanapofanya ununuzi.

Wananchi waliopatiwa msaada huo akiwamo Patima Makame Ali, Sichana Othman Kombo na Ame Ali Ame, wameipongeza bodi hiyo kwa msaada huo ambao utawapa uhakika wa kupata mlo angalau mara moja kwa siku.

Walisema wanakabiliwa na ugumu wa maisha na kijiji chao mvua zimeadimika na hakuna shughuli yoyote ya kilimo kuwawezesha kwa chakula.

"Hapa unaponiona hadi sasa majira ya saa saba mchana sina chakula nyumbani kwangu, lakini naishukuru ZRB kwa kunipatia msaada huu wa chakula na kwa sasa ninauhakika wa kupata mlo wangu pamoja na familia yangu," alisema Ame.

Aliziomba taasisi zingine na watu wenye uwezo kuwapatia misaada mbalimbali kwa sababu hali ya ukame ni mbaya kijijini hapo.



Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), Yusuph Juma Mwenda, akimkabidhi mafuta ya kula Hamida Mosi Khamis mkazi wa kijiji cha Kijini Matemwe Mkoa wa Kaskazini Unguja, bodi hiyo ilipofika kijijini hapo kutoa msaada wa vyakula mbalimbali kwa kaya 583 za wananchi wa kijiji hicho. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Onesho kubwa utalii kimataifa kufanyika mwakani

**Na Mwandishi Wetu**

ZANZIBAR inatarajiwa kuwa mwenyeji wa onesho kubwa la utalii la kimataifa mwanzoni mwa mwaka ujao litakalodumu kwa siku mbili.

Onesho hilo linaloandaliwa na kampuni ya maonesho ya utalii nchini Tanzania 'Kilifair Promotion Co. Ltd', limepangwa kufanyika Februari 23 na 24, mwakani katika hoteli ya Golden Tulip uwanja wa ndege visiwani humo.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo yenye uzoefu wa kuandaa maonesho makubwa nchini na Afrika Mashariki, Dominick Shoo, alisema tukio hilo litawakutanisha wasafirishaji, wanunuzi, wawekezaji na wafanyabiashara ya utalii kutoka ndani na nje ya Tanzania.

Alisema, lengo kuu la onesho hilo ni kuhakikisha wanaifikia dunia na kufikisha ujumbe kwamba Zanzibar imefunguka na iko salama ili kuwahamasisha watalii kutoka mataifa mbalimbali kutembelea visiwa hivyo.

"Sote tunaona kuwa kila mmoja sasa ana kiu ya kusafiri baada ya dunia kutikiswa na janga la UVIKO-19. Ni juu yetu kuwatangazia kwamba Zanzibar na Tanzania ziko tayari kuwapokea na nchi iko salama kwa mapumziko ya likizo," alisema.

Shoo alisema utalii wa Zanzibar umerudi kwa kishindo na nchi imefunguka kikamilifu tayari kupokea wageni wengi kwa kuwa hoteli za madaraja tofauti zipo za kutosha sambamba na miundombinu muhimu inayopaswa kuhudumia watalii.

Alisema matarajio yalikuwa kupokea kampuni 100, lakini kuna dalili za kuvuka lengo na kufikia 130 na hadi anatoa taarifa, kampuni 95 zilikuwa zimeshajisajili.

Alisema dhamira yao ni kuunga mkono azma ya Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi, kutumia uchumi wa buluu unaojumuisha pia utalii kwa ajili ya kuongeza pato la taifa, sambamba na ziara ya Rais wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan 'Royal Tour' kuvitangaza vivutio vilivyomo nchini.


Akizungumzia ujio wa onesho hilo, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar Rahim Bhaloo, alisema ni fursa nzuri kuitangaza zaidi Zanzibar yenye vivutio vingi na sifa ya ukarimu kwa wageni.

Bhaloo ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii Zanzibar (ZATI), aliahidi kuwapa ushirikiano mkubwa waandaaji wa onesho hilo, wakijua linasaidia nchi kuongeza idadi ya watalii.

"Nilikuwa Kigali Rwanda hivi karibuni na tulikutana na Jumuiya kama ya ZATI, tukasaini makubaliano ya kushirikiana kukuza utalii katika ukanda wetu. Pia Shirika la Ndege la Rwanda linajiandaa kuanza safari za moja kwa moja Zanzibar," alibainisha Bhaloo.

Alisema ushirikiano huo, na onesho la Kilifair litakalofanyika hapa mwakani, ni njia sahihi ya kuifungua Zanzibar na Tanzania na kukata kiu ya watalii waliolazimika kujifungia ndani wakati wote wa UVIKO-19.

Hilo litakuwa onesho la kwanza la aina yake kuandaliwa na Kilifair Co. Ltd. hapa Zanzibar, likitarajiwa kuhamasisha kampuni nyingine ya safari kuona umuhimu wa kuitangaza Zanzibar na Tanzania kwa jumla.





# Wasomi washauri vyuo vikuu kutoa mafunzo ya ujuzi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya wasomi wameshauri vyuo mbalimbali nchini kutoa mafunzo ya ujuzi sambamba na kuweka ushirikiano kwa viwanda ili kuwajengea uwezo wanafunzi kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

Walitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki wakati wa kongamano la kutambua nafasi ya wahitimu wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (SAUT) katika kujenga ubora na ushindani wa kitaaluma kitaifa, kikanda pamoja na kidunia lililofanyika jijini Mwanza.

Kongamano hilo ambalo lilifanyika katika chuo hicho liliwakutanisha wanafunzi waliowahi kusoma chuoni hapo.

Akizungumza katika kongamano hilo, Makamu Mkuu wa chuo hicho, (Taaluma), Prof. Hosea Rwegoshora alisema licha ya vyuo kuwekeza katika kuhakikisha wanatoa elimu bora na ufaulu wa alama za juu kwa wanafunzi wao kuna umuhimu wa kuweka masomo ya ujuzi ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha na viwanda ili kuendeleza ujuzi huo.

Alisema hatua hiyo itawasaidia wasomi hao kujiajiri pamoja na kupata fursa nyingine za ajira ndani na nje ya nchi.

Prof. Agrey Nyomora akizungumza katika kongamano hilo, alisema tatizo la upatikanaji wa ajira kwa sasa ni la dunia nzima.

Hivyo aliwataka wahitimu wao kujihusisha na fursa zinazoendana na ujuzi wao kuliko kutegemea kuajiriwa.

“Ukiachana na kujiajiri idadi kubwa ya wahitimu wanakosa nafasi za kazi kutokana na kutokuwekeza katika ujuzi unaoendana na taaluma zao,” alisema Prof. Mutagahywa.

Prof. Mutagahywa alisema hatua hiyo inasababisha wasomi wengi kubaki mtaani na hivyo kuongeza idadi ya watu wasio na ajira nchini.

Baadhi ya wahitimu wa vyuo vikuu akiwamo Pius Lufutu alisema: “Ukifanya kazi kama sisi tuliojiajiriwa katika kufanya usafi wa mazingira watu wanatuona kama vituko na kama mtu siyo mvumilivu anaweza kuamua kuacha shughuli hizo na kubaki nyumbani”.

Aliyewahi kuwa mhitimu wa chuo hicho ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Nyamagana, Peter Begga aliwataka wasomi kutojifunga kifikra na kupuuzia fursa nyingine ikiwa ni pamoja na siasa.

“Ukiwa msomi hutakiwi kusema huku niende huku niache bali popote ambapo unafanya kitu cha halali shikilia hapo bila kujali wengine wanasema nini,” alisema.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, akikabidhi cheti kwa mkufunzi wa Chuo cha VETA – Mwanza, Bakari Mahundu (kulia), katika hafla ya kufunga mafunzo ya stadi za maisha kwa wakufunzi na watendaji wa masuala ya watu wenye ulemavu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ‘Wasiofanyiwa tohara hatarini kupata maambukizi VVU’

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

VIJANA balehe wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 19, ambao hawajafanyiwa tohara wapo katika hatari ya kuambukizwa Virusi Vya Ukimwi (VVU), magonjwa ya zinaa pamoja na saratani ya kichwa cha uume.

Hayo yalibainishwa jana na Mratibu wa Tohara wa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Dk. Haji Sued.

Alisema kupitia mradi walionao wanafanyiwa upasuaji watu hao bila malipo yoyote tofauti na kundi la vijana wenye chini ya miaka 14 ambao hulazimika kulipia.

Kadhalika alisema wanaume wanaofanyiwa huduma hiyo mitaani kwa Sh. 10,000 kuogopa kufika vituoni wapo hatarini kupata maambukizi hiyo kwa sababu wanahudumiwa na watu wasiokuwa na ujuzi.

Alisema vijana wenye umri huo wasipofanyiwa tohara mapema wanauwezekano wa kusababisha saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake au mabinti na ndiyo sababu serikali kwa kushirikiana na wadau wa afya wameendelea kuhimiza kundi hilo kufanyiwa tohara ili kuepukana na maradhi hayo.

Dk. Sued alisema ili kulifikia kundi hilo lililoko pembezoni mwa mji, walianzisha kliniki tembezi hali ambayo imeleta mafanikio makubwa ikiwa sambamba na kulifikia kundi la watu wenye umri wa miaka 50 na kuendelea.

Alisema katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kuna vituo vitano vya kutolea huduma ambavyo ni Kituo cha Afya Iyenze, Nyasubi, Mwendakulima, Kagongwa na Hospitali ya Manispaa na vijana 2,641 wameshafanyiwa tohara katika Kituo cha Nyasuni, Kagonga.

Alisema matatizo wanayokutana nayo ni wanaume kuhoji ngozi inayotolewa inapelekwa wapi na kwa nini huduma itolewa bure kwa vijana wenye umri kuanzia miaka 14.

Ally Shaban mkazi wa Zongomela alisema ili kuwafikia vijana wengi ni bora serikali ikatangaza ratiba ya kliniki tembezi na maeneo itakayofika siku za kazi ili wasiokuwa na uwezo wafike na kupatiwa huduma.

# Ofisa Elimu awapeleka mbugani wanafunzi waliofaulu

**Na Mobini Sarya,** SERENGETI

OFISA Elimu wa Kata ya Nyamuswa, Andrew Matogoro amewapa zawadi wanafunzi waliofaulu mtihani pamoja na walimu wao kwa kuwapeleka kutalii kwenye Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, ikiwa sehemu ya kuwapa motisha.

Akizungumza na Nipashe Matogoro alisema aliandaa ziara hiyo ya siku mbili kwa kushirikiana na viongozi wa kata pamoja na wazee maarufu wa kata hiyo kama sehemu ya kuinua elimu na kuwapa motisha walimu wa shule za msingi na sekondari waliofanya vizuri.

“Tulianzia kwenye geti la Ndabaka, lengo ni kutambua juhudi za walimu hawa na kuwapa motisha namna wanavyofanya kazi, mwaka jana tulienda Kisiwa cha Saa Nane Mwanza, tuna lengo la kuwaunganisha walimu na jamii ndiyo maana tumekuja na wazee maarufu wa kata yetu wafahamiane ili walimu waweze kufanyakazi katika mazingira mazuri,” alisema.

Akizungumza katika ziara hiyo, Mwenyekiti wa Chama cha Walimu (CWT), Wilaya ya Bunda, Emmanuel Majura, aliwapongeza viongozi wa kata hiyo kwa kutumia fursa hiyo kuunganisha walimu na kuwapa nafasi ya kwenda kutalii na kupumzisha akili.

Alishauri viongozi wengine kuiga mfano huo kwa kuandaa ziara za ndani na nje ya wilaya ambazo zinasaidia kutoa motisha kwa walimu na wanafunzi.

Baadhi ya walimu walioshiriki ziara hiyo walipongeza mratibu wa kuwapeleka kutazama wanyama kwenye Hifadhi ya Serengeti ambayo inatajwa kuwa na vivutio vingi ikilinganishwa na hifadhi zingine hapa nchini.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Nyamswa A, Elika Bukumbi alisema katika ziara hiyo amejifunza namna wanyama wanavyoishi na kuzaliana.

Diwani wa kata hiyo, Ibrahim Igai, aliwapongeza walimu hao namna wanavyojituma katika majukumu yao ya kuinua elimu na kuahidi kuwapa ushirikiano wa kutosha katika kutatua kero zao.

Alisema: “Kwanza niwapongeze walimu wa kata yangu namna wanavyojituma kuhakikisha ufaulu unaongezeka nina ahidi kutoa ushirikiano kwa walimu wote na nitatatua kero zote zinazowakabili walimu”.

## Mtoto anusurika kuuawa na kiboko nchini Uganda

**WASHINGTON,** MAREKANI

MTOTO wa miaka miwili Iga Paul amenusurika kushambuliwa na kiboko karibu na nyumbani kwao kusini magharibi mwa Uganda, wakati akicheza karibu na ufukwe wa Ziwa Edward wakati kiboko alipomshambulia.

Polisi nchini humo walibainisha kuwa mnyama huyo alimnyakua mtoto huyo mchanga na kumeza nusu ya mwili wake na kwamba mwanaume mmoja wa eneo hilo alipambana na kiboko huyo kwa kumrushia mawe.

Mamlaka ya Wanyamapori nchini Uganda imepinga kauli hiyo na kuiambia BBC kwamba mvulana huyo alishambuliwa badala ya kumezwa.

Kwa mujibu wa polisi, baada ya shambulio hilo lililotokea tarehe 4 Desemba, mtoto huyo alipelekwa katika kituo cha afya kilicho karibu ambako alitibiwa majeraha yake. Baadaye alihamishiwa katika Hospitali ya Bwera, ambako madaktari walimpa chanjo ya tahadhari ya kichaa cha mbwa.

Polisi walisema tukio hilo lilikuwa la kwanza kwa kiboko kupotea kutokea ziwani na kumshambulia mtu yeyote.

Inaelezwa kuwa wanyama hao ambao wanaweza kuwa na uzito wa tani 1.5 kilo 1,500 wanakadiriwa kuua takribani watu 500 kwa mwaka barani Afrika.

Maofisa waliwaonya wenyeji kwamba wanyama hao wanaweza kuona wanadamu kama tishio na kusema kwamba maingiliano yoyote yanaweza kuwafanya wafanye fujo.

Viboko ni mamalia wa tatu kwa ukubwa wa nchi kavu na meno yao yanaweza kufikia urefu wa 50.8 cm ambazo ni sawa na inchi 20. **BBC**

## 12 wauawa na wenye silaha DRC

**KINSHASA,** DRC

NCHINI Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), watoto watano ni miongoni mwa watu 12 waliouawa Kaskazini Mashariki mwa nchi hiyo, baada ya kushambuliwa na kundi moja la waasi, ambalo halikushiriki kwenye mazungumzo yaliyofanyika jijini Nairobi.

Kwa mujibu wa viongozi wa eneo tukio lilipotokea shambulio hilo mwishoni mwa juma lililopita, katika kijiji cha Walendu Watsi, ambako wakazi walikatwa kwa mapanga na wengine kuteketezwa hadi kufa.

Ripoti zinasema, watu waliolengwa ni kutoka kabila la Lendu kwa mujibu wa msemaji wa kabila hilo Jean Marie Ndjaza.

Katika hatua nyingine, mapigano mapya yalizuka juzi kati ya waasi wa M23 na wanajeshi wa serikali ya DRC, ripoti zikielezea kuwa, yameendelea mpaka jana, wilayani Rutshuru baada ya kuanzia Bwiza eneo ambalo limekuwa likidhibitiwa na waasi hao.

Mapigano haya yamekuja siku 10 baada ya kushuhudiwa kwa utulivu na waasi hao kukutana na maofisa wa Jeshi la DRC na wadau wengine, huko Kibumba. **RFI**

# Kamati kutafuta mashtaka ya Trump

**WASHINGTON,** MAREKANI

UCHUNGUZI wa bunge kuhusu ghasia za mwaka jana katika Bunge la Capitol utaripoti kupendekeza mashtaka matatu ya uhalifu dhidi ya Rais wa Marekani wa zamani Donald Trump.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Marekani, kamati teule ya Baraza la Wawakilishi itatafuta mashtaka ambayo hayajawahi kushuhudiwa ya uasi dhidi ya Rais wa zamani wa Marekani.

Jopo hilo linatarajiwa kuchapisha ripoti yake ya mwisho wiki hii, Wafuasi wa Trump walivamia Congress Januari 6, 2021 kwa nia ya kusimamisha uidhinishaji wa Joe Biden kama rais.

Idara ya haki ambayo tayari inachunguza jukumu la Trump katika machafuko hayo hailazimiki kuzingatia rufani kutoka kwa jopo lolote la bunge.

Aidha, inaripotiwa kwamba Trump alikanusha kufanya makosa hayo. Huku msemaji wake Steven Cheung, akieleza kuwa kamati isiyochaguliwa ya Januari 6 ilifanya majaribio na wafuasi wa Never Trump ambao ni doa katika historia ya nchi hii.

Inabainishwa kwamba kamati teule imeratibiwa kufanya mkutano wake wa mwisho jana wakati mapendekezo yoyote ya kesi yatabainiwa.

Kulingana na vyombo mbalimbali, jopo hilo litapendekeza Trump ashtakiwe kwa kuzuia utaratibu rasmi na kula njama ya kulaghai taifa la Marekani.

Wana jopo tisa wanatarajiwa kuidhinisha ripoti ya mwisho ya sura nane, ikitegemea mahojiano na zaidi ya mashahidi 1,000, na kuiwasilisha kwa Idara ya Haki (DoJ).

Mwenyekiti Bennie Thompson, Mwanademokrasia wa Mississippi ambaye anaongoza kamati teule, alisema ripoti kamili inatarajiwa kuwekwa wazi Jumatano. **BBC**



Rais Kais Saied wa Tunisia akipiga kura katika uchaguzi wa Bunge. **PICHA: DW**

# Tunisia yafanya uchaguzi uliosusiwa na upinzani

**ENNASR,** TUNISIA

WANANCHI wa Tunisia wamepiga kura kuchagua bunge jipya, huku ikibainishwa kuwa uchaguzi huo unafanyika chini ya kiwingu cha mzozo wa kidemokrasia, hali ngumu ya uchumi na mfumuko mkubwa wa bei.

Kwa mujibu wa ripoti iliyochapishwa jana na DW, vyama kadhaa vya upinzani ikiwamo muungano wa Salvation Front ambao unakijumuisha chama maarufu cha Ennahda vimeususia uchaguzi huo kwa sababu vinasema ni sehemu ya mpango wa Rais Kais Saied kuimarisha nguvu na madaraka yake.

Mmoja wa viongozi wa vyama vya upinzani nchini humo, Ezzeddin Hazgui, alisema kwamba wanaususia uchaguzi huo kwa kuwa hawawezi kujiunga na mtu anayesambaratisha taasisi za dola.

Uamuzi wa kususia uchaguzi huo unatajwa kusababisha bunge lijalo kuwa na wanasiasa watiifu kwa Rais Saied ambaye wakosoaji wake wanamtuhumu kuchukua mwelekeo wa udikteta. Vituo vya kupigia kura vilifunguliwa mapema saa mbili asubuhi za Tunisia na vilitarajiwa kufungwa jioni ya saa kumi na mbili, huku wagombea 1,500 wakiwania viti vya bunge la taifa hilo.

Kwa mujibu wa tume ya uchaguzi vyama vitano na wagombea 1,500 wameidhinishwa kuwania nafasi za bunge.

Idadi ya wapigakura waliojitokeza mapema asubuhi ya jana ilikuwa ndogo ingawa waandishi wa Shirika la Habari Associated Press waliokuwa eneo la tukio walibainisha kuwa walishuhudia misusuru ya watu kwenye vituo kadhaa mjini Tunis.

Rais Kais Saied na mkewe Ichraf Chebil, walipiga kura huko Ennasr kitongoji cha nje kidogo ya mji mkuu Tunis.

Uchaguzi kwenye taifa hilo la Afrika Kaskazini unafanyika wakati kuna hisia za wazi za kuporomoka kwa imani ya umma wa Tunisia kwa utawala wa Rais Saeid na ajenda yake ya kuufanyia mageuzi mfumo wa kisiasa wa nchi hiyo.

Kiongozi huyo aliyechaguliwa kuwa Rais wa Tunisia miaka miwili iliyopita alianza vitimbi katikati ya mwaka uliopita kwa kutangaza kusitisha shughuli za bunge la taifa na kumtimua waziri mkuu wa wakati huo Hichem Mechichi.

Februari mwaka huu alisitisha kazi za Baraza la Mahakama ya Juu ya nchi hiyo na mwezi mmoja baadaye akatangaza kulivunja kabisa bunge la Tunisia.

Hakuishia hapo, aliitisha kura ya maoni Julai mwaka huu kuifanyia marekebisho katiba ya Tunisia ambayo yanamwongezea nguvu za kutowajibika kokote.

Sheria za uchaguzi za nchi hiyo pia zilibadilishwa mwezi Septemba na ndiyo zitatumika kuongoza uchaguzi unaofanyika sasa.

Nafasi za majimbo zimepunguzwa kutoka 217 hadi 161 na kwa mara ya kwanza Rais wa Tunisia wanachagua wagombea mmoja mmoja badala ya kuvipigia kura vyama vya siasa.

Masuala yote hayo yamejenga msingi wa uchaguzi wa sasa kukosa sura ya uhalali miongoni mwa wadau wa siasa wa nchi hiyo. **DW**

# Nyumba 43 zaezuliwa, watatu wajeruhiwa

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

NYUMBA 43 kwenye Kijiji cha Tamasenga mkoani Rukwa zimeezuliwa na upepo ulioambatana na mvua ya mawe na radi huku wengine watu watatu wakijeruhiwa.

Vilevile, mvua hiyo imesababisha uharibifu mkubwa wa mali na akiba ya chakula kilichokuwapo huku wananchi wakibaki bila makazi, wakiomba msaada ili waendelee na maisha.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, Aesh Hillary, alisema ni vyema wadau wa maendeleo na wenye mapenzi mema wakajitokeza kuwasaidia wananchi hao ili waendelee na maisha.

Kiongozi huyo aliwatembelea wananchi hao kuwapa pole kutokana na madhila yaliyowapata na kubaini kuwa wananchi hao wanahitaji msaada wa haraka.

"Watu hawa wanahitaji tuwasaidie, wananchi wenye mapenzi mema na wadau wa maendeleo ninawaomba mjitokeze, mguswe na tukio hili na kuwasaidia, mimi nimetoa magodoro na mablanketi, wanahitaji vyakula na nguo, kumbukeni vitabu vitakatifu vinatuhimiza upendo, basi tujitolee kwa ajili ya ndugu zetu hawa," alisema Hillary.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Alistide Mwanisenga, alisema janga hilo lilitokea juzi majira ya saa 11 jioni.

Alisema wananchi wengi wamepoteza mali zao kutokana na kusombwa na maji na nyingine kuharibika.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Maria Kapele, alimshukuru mbunge huyo kwa msaada aliowapa huku akiwaomba watu wengine kujitokeza kuwasaidia kwa kuwa mahitaji ya huduma za msingi ni makubwa.



Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, akimtunuku Shahada ya Uzamili katika Sayansi ya Lojistiki na Usafirishaji, Farida Salum, katika mahafali ya 38 ya Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askofu ataka viongozi wa dini wasaidie vita dhidi ya ukatili kijinsia

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

ASKOFU na Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Amani Christian Centre (ACC), Dk. Laurence Kametta, amesema endapo viongozi wa dini watasimama kwenye nafasi zao, wataipunguzia serikali mzigo wa kukemea uhalifu na ukatili unaoendelea kwenye jamii.

Dk. Kametta aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kutunukiwa shahada ya uzamivu katika masomo ya biblia na theolojia kwenye mahafali ya Chuo cha Zoe Institute of Apostolic and Testimony, Mbwawa wilayani Kibaha.

Alisema wajibu wa viongozi wa dini ni mkubwa na wakiamua kusimama kwenye nafasi zao kukemea matendo maovu kwa kuhubiri injili, watu wataacha utapeli, uhalifu na matukio mengine yasiyompendeza Mungu.

"Matatizo yapo na yamekuwapo lakini falsafa ya kuyatatua imekuwa shida kiroho na kiimani kwa sababu wapo watu wanaozorotesha ufahamu wa watu wasijikwamue na wanawapa matumaini kwenye mambo ambayo watu wangeweza kutumia nguvu waliyopewa na Mungu kujikwamua.

"Kama viongozi wa dini wakiishi kwa mfano wa maisha ya vielelezo na watu wakaona kweli maisha wanayoishi viongozi wetu ni halisi, wataacha maovu na watapokea nguvu tunayoihubiri na watakuwa wananchi wazuri wanaompendeza Mungu na serikali haitakuwa na kazi ya kukemea mambo hayo," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Kametta, wajibu wa viongozi wa dini ni kufundisha wananchi kufanya kazi, kuwaelimisha mbinu nzuri za kiuchumi, maisha ya kimchakato ili kufanya vizuri kwenye maisha yao na kuepukana na uhalifu.

Alisema viongozi wa dini wanapaswa kuwa kiungo kizuri kati ya serikali na wananchi, hivyo wakitumiwa vizuri, wanaweza kuisaidia serikali kutekeleza mipango yake kwa urahisi.

Mkuu wa chuo hicho, John Mwakilema alisema mtumishi wa Mungu akijengwa kwa namna sahihi na kanisa litajengwa vizuri, kutakuwa na watu wazuri kwenye jamii.

# Serikali yaahidi kuiwezesha NIT kuandaa wataalamu wa uchukuzi

**Na Prosper Makene**

SERIKALI imesema itaendelea kukiwezesha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) ili kitimize majukumu yake ya kuandaa wataalamu, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika Sekta ya Uchukuzi kwa maendeleo ya taifa.

Akizungumza wakati wa mahafali ya 38 ya chuo hicho yaliyofanyika mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alisema soko la ajira katika sekta ya usafirishaji limeongezeka kutokana na maboresho mbalimbali yanayofanywa na serikali kwenye bandari, ujenzi wa meli, viwanja vya ndege na ununuzi wa ndege.

"Nimepokea hotuba ya Mwenyekiti wa Baraza la Chuo na hotuba ya Mkuu wa Chuo kuhusu malengo makubwa ya chuo kama yalivyoainishwa kwenye Mpango Mkakati wa Nne wa Miaka Mitano (2020/21-2025/26) pamoja na utekelezaji wa shughuli za chuo. Hivyo, tunawaahidi kuendelea kuwasaidia ili kufikia malengo mliyojiwekea.

"Idadi hii ya wahitimu kwa mwaka huu ni ushahidi tosha wa juhudi kubwa za chuo za kuhakikisha tunakuwa na wataalamu wa kutosha katika Sekta ya Uchukuzi.

"Malengo ya chuo ya miaka mitano yanaonyesha dhahiri dhamira ya chuo kuendelea kuzalisha wataalamu wa Sekta ya Uchukuzi kwa kuzingatia jitihada za serikali za kuimarisha sekta hii.

"Pamoja na juhudi hizi kubwa mnazofanya, ninatoa wito kwa uongozi wa chuo kuendelea kuwa wabunifu na kufanya kazi kwa bidii ili kukifanya chuo chetu kuwa mahali sahihi pa kujifunzia," aliagiza.

Mwakibete aliendelea kusema kuwa serikali imeendelea kuwekeza katika Sekta ya Uchukuzi hasa katika ujenzi wa barabara na madaraja, reli ya kisasa, meli, viwanja vya ndege na ununuzi wa ndege.

Alisema uwekezaji huo mkubwa unahitaji wataalamu watakaoendesha na kusimamia kwa ustadi miradi hiyo kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi.

"Kama serikali tumefarijika kusikia kwamba chuo kimeendelea kutanua wigo wa kutoa mafunzo katika sekta hii muhimu ya uchukuzi, ikiwa ni pamoja na kujiimarisha kwenye njia zote za usafirishaji, yaani usafiri wa anga, majini, reli, barabara na usafiri kwa njia ya mabomba. Tunawapongeza sana," alisifu.

Naibu Waziri huyo pia alikipongeza chuo hicho kwa kuanza kutoa mafunzo ya usafiri kwa njia ya maji pamoja na kupanua wigo wa utoaji mafunzo ya reli.

"Kozi hizi ni muhimu sana kwa taifa letu kwani zitapunguza mzigo kwa serikali wa kugharamia mafunzo haya nje ya nchi ambayo hutolewa kwa gharama kubwa," alisema.

Aliongeza kuwa serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, inafahamu vizuri mahitaji muhimu kwa chuo ikiwa ni pamoja na ubora wa miundombinu na majengo, ofisi za wahadhiri na nafasi za mabweni kwa wanafunzi.

"Aidha, ninatambua kuwa chuo kinaendelea na ujenzi wa baadhi ya miundombinu hiyo kupitia mradi wa EASTRIP unaofadhiliwa na serikali kupitia Benki ya Dunia. Serikali itaendelea kushirikiana na chuo katika kuhakikisha mahitaji haya yanapatiwa ufumbuzi endelevu.

"Ninauagiza uongozi kuendelea kutumia mapato ya ndani katika kuendeleza na kuboresha miundombinu ya chuo," aliagiza.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Zacharia Mganilwa alisema idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa na chuo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka, hivyo kusababisha ongezeko la wataalamu katika Sekta ya Uchukuzi.

"Katika kipindi cha miaka mitano idadi ya wanafunzi imeongezeka kwa asilimia 121 kutoka 6,748 mwaka wa masomo 2018/19 hadi wanafunzi 14,933 mwaka wa masomo 2022/23," alibainisha.

Aliongeza kuwa kwa sasa chuo kina jumla ya wafanyakazi 358. Kati yao, wanataaluma ni 214 na waendeshaji ni 144.

"Idadi hii ni ndogo hasa kwa wanataaluma kulinganishwa na mahitaji halisi ya chuo, hivyo chuo kinalazimika kutumia fedha nyingi kuwalipa wahadhiri wa muda ili kuziba upungufu wa wanataaluma uliopo.

"Tunaishukuru serikali katika mwaka wa fedha 2022/23 imetupatia kibali cha kuajiri watumishi 42, tunaamini katika mwaka ujao wa fedha serikali itaendelea kutupatia kibali cha ajira mpya ili kukabiliana na upungufu uliopo," Prof. Mganilwa alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Dk. Gemma Kishari Modu alisema: "Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa serikali kwa kuendelea kuidhinisha bajeti ya utekelezaji wa miradi ya chuo kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

"Pia tunaishukuru serikali kwa kutoa fursa kwa NIT kuanza kutekeleza miradi mbalimbali ukiwapo Mradi wa Uanzishaji wa Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Taaluma za Anga na Operesheni za Usafirishaji (CEATO) kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia pamoja na Mradi wa Uanzishwaji wa Kituo cha Kikanda cha Umahiri cha Mafunzo ya Usalama Barabarani (RCoERS) kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB)."

## BURUDANI




# ZUCHU: NILITAKA KUWA MWANASIASA

MSANII Zuchu, amesema kama asingekuwa mwanamuziki basi mipango yake ilikuwa kuwa mwanasiasa.

Zuchu ambaye anatajwa kuwa kwenye mapenzi na bosi wake, Diamond Platinum, alisema kuwa kipindi yupo chuoni, alizunguka mataifa mengi kama kiongozi wa wanafunzi na kuona jinsi siasa za nje zilivyokomaa kuliko za mataifa mengi ya Afrika.

"Kama nisingekuwa mwanamuziki basi ningekuwa mwanasiasa, wakati nasoma chuo nilichagua kuwa mwanasiasa baada ya kuzunguka nchi mbalimbali duniani ikiwamo India," alisema Zuchu.

Mwanamuziki huyo ambaye kwa sasa yupo chini ya Lebo ya WCB, alisema alilazimika kuasi siasa na kukumbatia muziki kutokana na ushawishi mkubwa wa mama yake.

Ikumbukwe mama yake Zuchu, Khadija Kopa, ni mwanamuziki wa muda mrefu ambaye anatamba kwenye muziki wa taarab.



## WAHU NUSURU AVUNJE NDOA NA NAMELESS

NYOTA wa muziki wa Kenya, Wahu, amefunguka kuwa alikaribia kuvunja ndoa yake na mwanamuziki Nameless miaka ya mwanzoni tu baada ya kuoana.

Wahu amesema hawakuwa wanaelewana kabisa na mumewe na alitaka kuondoka kwenye ndoa hiyo baada ya miaka miwili tu.

Wahu alikuwa anazungumza na mchekeshaji Celestine Ndinda ambapo alifunguka kuwa muda mwingi katika miaka ya awali alikuwa anatoroka nyumbani baada ya kukosana na Nameless kwa kitu kidogo tu mpaka wakati mmoja aliondoka na kwenda kupanga peke yake.

Wahu alisema kuwa ilifika mahali akakomaa kiakili na kujiaminisha kuwa kutoroka si suluhisho.

"Inafika mahali unasema wewe ndio rafiki yangu, na mimi ndio niko kwako, wacha nibakie tu. Itabidi sasa tupendane. Lakini bila shaka hapo mwanzoni, weeh! Kwanza ile miaka miwili ya awali, nilikuwa nishaenda hata kutafuta nyumba, Nilikuwa najiambia kuwa mimi siwezi kukosa kitu chochote hii Nairobi kwa sababu najitegemea," alisema Wahu.


Aliongeza kuwa anadhani kufikiria kwake sasa na kipindi kile ni nyakati mbili zilizotofautiana huku akisema kukasirika kwake kumepungua, jambo ambalo limerahisisha maisha yake na mumewe.

"Tofauti ni kwamba, sasa mimi nimeacha kukasirika sana."

Wawili hao wamedumu pamoja kwa miaka 25, miaka 17 ikiwa ni ndoa rasmi waliyofunga mwaka 2004.

Miezi miwili iliyopita Wahu alijifungua mtoto wao wa tatu na Nameless.

## MAUA AREKODI KALI NANE



NYOTA wa Bongo Fleva, Maua Sama, amewataka mashabiki wake kukaa mkao wa kula, kwani anakuja na nyimbo kali nane.

Kwa mujibu wa Maua hadi sasa ameshatengeneza ngoma nane ambazo zote zimeandaliwa na mtayarishaji, S2kizzy.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Maua aliweka picha yenye maneno yaliyosomeka: "After Recording 8 bangers (baada ya kurekodi nyimbo kali nane."

Hata hivyo, Maua hajaweka wazi kama ngoma hizo zitatoka kwa mfumo gani.

Lakini amewataka mashabiki wake kuvuta subira kupata muziki mzuri kutoka kwa mtoto mzuri.

# RAIS SAMIA NA MCHENGERWA WATUNUKIWA TUZO ZA HESHIMA

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, wametunukiwa tuzo maalum ya shukrani kwa mchango wao katika kuleta mapinduzi makubwa kwenye sekta ya sanaa nchini.

Tuzo hizo zimetolewa kwenye kilele cha utoaji wa Tuzo za Filamu 2022, kilichofanyika usiku wa kuamkia jana kwenye kituo cha Kimataifa cha Mikutano jijini Arusha, AICC.

Awali, kabla ya kukabidhi tuzo hizo, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Filamu, Dk. Kiagho Kilonzo, alisema Waziri Mchengerwa amechaguliwa kwa kuzingatia mchango wake mkubwa alioufanya katika kipindi kifupi tangu achaguliwe kusimamia sekta hiyo ambayo inaongoza kwenye kuchangia ukuaji wa uchumi na kwamba maelekezo ambayo amekuwa akiyatoa na kuyasimamia yamesaidia kukuza sekta hiyo kwa kiwango kikubwa.

"Ni kutokana na maelekezo thabiti ya waziri ndiyo maana leo tunashuhudia kufanyika kwa mafanikio makubwa ya utoaji wa tuzo za msimu wa pili," amefafanua Kilonzo.

Aidha, alieleza kuwa Mchengerwa anakuwa kiongozi wa pili kupata tuzo hiyo baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyepata tuzo kama hiyo kutokana na mchango mkubwa anaoutoa kwenye sekta ya sanaa katika kipindi chake.

" Rais Samia tumemtunukia tuzo hii ya heshima na shukrani kwa mambo makubwa mawili, kwanza kutenga muda wake kama rais na kucheza Filamu ya Royal Tour sio kitu cha kawaida, na pili ni kuturejeshea Mfuko wa Sanaa utakaosaidia wasanii kukopa fedha kwa ajili ya kufanya kazi zao," amefafanua Kilonzo.

Tuzo ya rais ilikabidhiwa na Msanii, Nguli Mzee Chilo na kupokewa kwa niaba yake na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mchengerwa.

Wakati huohuo, Mchengerwa ameelekeza Idara ya Sanaa kwa kushirikiana na Bodi ya Filamu kuhakikisha ifikapo Jumatano wiki hii wasanii wawe wameanza kupata fedha katika mfuko huo ili waweze kutengeneza kazi nzuri zitakazopata masoko hatimaye kuboresha maisha yao.

Katika hotuba yake rasmi ya ufunguzi wa utoaji wa Tuzo za Filamu, Mchengerwa alisisitiza kuwa dhamira ya serikali ni kuendelea kuwekeza katika kuwasaidia wasanii ili waweze kufanya vizuri.

Jumla ya Tuzo 32 zilitolewa katika msimu huu ambapo kumekuwa na tuzo maalum zilizotolewa ambazo si za ushindani katika eneo la viongozi, wadau na wasanii ambapo mara ya kwanza wasanii 10 waliotoa mchango mkubwa kwenye sekta hii walitunukiwa Tuzo ya TFB fahari.

Wasanii hao ni pamoja na Dk. Cheni, Bishanga, Musa Banzi, Rey, Single Rich, JB, Monalisa, Wema Sepetu, Thecla Mgaya (Aisha) na William Mtitu.

Pia Msanii, Marehemu Kanumba alitunukiwa Tuzo ya Heshima ya mafanikio katika kipindi chote kwa upande wa wanaume (Lifetime Achievement Male) na Joyce Mhavile kwa upande wa Wanawake. Tuzo nyingi za msimu huu zimekwenda kwa wasanii wapya kwenye tasnia hiyo zikipokelewa kwa hisia kali huku wasanii wakibubujikwa na machozi ya furaha kutokana na ushindi huu wa kihistoria.

Tukio hilo lilihudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Pauline Gekul na viongozi na wadau mbalimbali wa sanaa huku likipambwa na burudani nzuri kutoka kwa vikundi mbalimbali vya wasanii.



Msanii wa maigizo nchini, Tecla Mjata (kulia), akimkabidhi Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, Tuzo Maalum ya Shukrani kwa mchango wake katika kuleta mapinduzi makubwa kwenye sekta ya sanaa nchini. Tuzo hiyo ilitolewa kwenye kilele cha utoaji wa Tuzo za Filamu 2022, kilichofanyika juzi kituo cha Kimataifa cha Mikutano jijini Arusha (AICC). **MPIGAPICHA WETU**

## Makata aianika Ruvu Shooting

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Ruvu Shooting, Mbwana Makata, amefunguka kinachoifelisha timu hiyo kuwa kuna baadhi ya wachezaji wanacheza namba ambazo si zao kutokana na wengine kwenda kwenye kozi za kijeshi.

Kocha huyo amesema unahitajika usajili kwenye kipindi cha dirisha dogo ili kila mchezaji arejee kwenye namba yake aliyoizoea.

Makata ambaye amechukua jukumu la kuifundisha timu hiyo badala ya Charles Boniface Mkwasa aliyejiuzulu hivi karibuni kutokana na matokeo mabaya kwenye kikosi hicho, alisema kwa sasa analazimika kuwachezesha mawinga kwenye nafasi ya ushambuliaji na mabeki kwenye nafasi za kiungo kutokana na uhaba wa wachezaji kwenye nafasi hizo.

Makata alisema hayo baada ya timu yake kutandikwa mabao 2-0 dhidi ya Ihefu Ijumaa iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, yaliyofungwa na Obrey Chirwa na la kujifunga la Michael Aidan.

**"Tunahitaji mabadiliko mengi ya usajili, tuna wachezaji wanane wa kikosi cha kwanza wame kwenda kwenye kozi, hata hawa waliocheza nafasi ya ushambuliaji siyo nafasi zao, mawinga ndiyo nime walazimisha wacheze kama washambuliaji, hala fu baadhi ya mabeki wa mecheza nafasi ya viungo wa kati.**

Kuna marekebisho mengi yanatakiwa kufanyika ya kuleta wachezaji wazuri na wenye viwango, mawinga tunao wa kutosha, hapa tunahitaji washambuaji, viungo na tutaangalia pia nyumba kwa mabeki, maana nina wachezaji wazoefu, lakini wanashindwa kuhimili presha na wanajifunga, hii si mechi ya kwanza kwa mabeki kujifunga.

Kipigo hicho kimeifanya Ruvu Shooting kuwa kwenye nafasi ya 15 kwa pointi 11, ikicheza mechi 16, kushinda tatu, sare mbili na kupoteza 11, ikiwa ni moja kati ya timu mbili zilizopoteza mechi nyingi zaidi mpaka sasa, sambamba na Polisi Tanzania.

# BMT yasitisha uchaguzi mjumbe DRFA

**Na Saada Akida**

BARAZA la Michezo Tanzania (BMT), limesitisha uchaguzi mdogo wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), wa nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF).

Uchaguzi huo uliokuwa ufanyike jana katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa DRFA, ambapo Kaimu Katibu Mkuu, Ramadhan Misilu, alifafanua hilo mbele ya wajumbe baada ya kusoma ajenda za mkutano huo.

Uchaguzi huo ulikuwa wa kujaza nafasi ya aliyekuwa Mjumbe wa Mkutano Mkuu, Shafii Dauda, ambaye amefungiwa miaka mitano kutojihusisha na mchezo wa mpira wa miguu nje na ndani ya nchini.

Misilu alisema uchaguzi umesitishwa kwa muda kutokana na kuwapo kwa shauri lililowasilishwa na BMT na mmoja wa wajumbe.

"Katika mkutano huu kulikuwa na ajenda pia ya uchaguzi, lakini umesogezwa mbele kwa sababu ya serikali kupitia BMT, kusitisha uchaguzi huo na kusogezwa mbele hadi hapo mchakato huo utakapomalizika," alisema katibu huyo.

Katika hatua nyingi, Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Salum Madadi, aliwataka DRFA kusimamia na kusukuma mbele soka la wanawake ili lipige hatua.

"Kwa bahati nzuri Mkoa wa Dar es Salaam mnaongoza, zipo timu zenye nguvu ila Fountain Gate ipo juu, mfanye juhudi kubwa ya kuhakikisha soka la wanawake linapiga hatua zaidi," alisema Madadi.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**NKUNKU SAFI CHELSEA**
CHELSEA imeripotiwa kukamilisha usajili wa straika wa RB Leipzig na Ufaransa, Christopher Nkunku na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, atajiunga rasmi na klabu hiyo Julai 2023. (***Fabrizio Romano, Twitter***)

**SOUTHGATE KUENDELEA ENGLAND**
GARETH Southgate imeamua kubakia kama kocha wa England baada ya kutolewa na Ufaransa kwenye robo fainali ya Kombe la Dunia nchini Qatar. (***Telegraph***)

**HOWE ATAKA AENDELEE**
EDDIE Howe mwenye umri wa miaka 45, pia amesema anataka Gareth Southgate mwenye miaka 52 kubaki kuwa kocha wa England – licha ya yeye ambaye anainoa Newcastle United kuhusishwa na nafasi hiyo. (***Chronicle***)

**MOUKOKO BADO DORTMUND**
NYOTA anayewaniwa na Liverpool, Manchester United na Chelsea, Youssoufa Moukoko mwenye umri wa miaka 18, hajakaribia kusaini mkataba mpya na Borussia Dortmund, wakala wa straika huyo wa Ujerumani, amethibitisha. (***Sky Germany via Liverpool Echo***)

**OUNAHI KUONDOKA ANGERS**
MWENYEKITI wa Angers, Said Chabane, amesema klabu hiyo ya Ligi Kuu Ufaransa, French, Ligue 1, inajiandaa kumpoteza kiungo wa Morocco, Azzedine Ounahi, mwenye umri wa miaka 22, wakati wa dirisha dogo la Januari, huku Leicester, Leeds United na West Ham zikiripotiwa kumwania. (***Talksport***)

**JUDE NA LIVERPOOL**
LIVERPOOL imeongeza nia ya kumsajili kiungo wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19. (***Mirror***)

**GVARDIOL AWANIWA CHELSEA**
CHELSEA inapanga kuweka presha kwa Real Madrid katika mbio za kumsajili mlinzi wa RB Leipzig na Croatia, Josko Gvardiol, mwenye umri wa miaka 20, wakati wa dirisha la januari. (***Mirror***)


**KVARATSKHELIA HAUZWI**
KLABU ya Newcastle United ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazomwania fowadi wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia, mwenye umri wa miaka 21, lakini Napoli haina mpango wa kumuuza kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 50. (***90min***)

**DE GEA KUONDOKA**
GOLIKIPA wa Manchester United, David de Gea, mwenye umri wa miaka 32, anaweza kuondoka Old Trafford kwa uhamisho huru wakati wa dirisha la Januari, wakati klabu hiyo ikiwa haijaonyesha nia ya kutaka kuongeza mkataba wake ambao umebaki miezi 12. (***Sky Germany via Sun***)

**PULISIC HAJUI HATIMA**
KIUNGO wa Marekani, Christian Pulisic, mwenye umri wa miaka 24, amesema "mambo yanabadilika haraka na chochote kinaweza kutokea" baada ya kuhusishwa na mpango wa kuondoka Chelsea kwenda Manchester United. (***Indirect Podcast via Metro***)

**CUNHA ATAKIWA EVERTON**
EVERTON ni moja ya klabu nne ambazo zinamwania fowadi wa Atletico Madrid na Brazil, Matheus Cunha, mwenye umri wa miaka 23, baada ya kuvunja mkataba na mchezaji wa kimataifa wa Venezuela mwenye umri wa miaka 33, Salomon Rondon. (***Fabrizio Romano, Twitter***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MODRIC: BADO NAWEZA KUCHEZA HADI EURO 2024

**Kuhusu mustakabali wangu, ninaifurahia timu ya taifa, najisikia furaha, bado nadhani naweza...**

**DOHA,** Qatar

LUKA Modric amedokeza kwamba, anaweza kuichezea Croatia kwenye michuano ya Euro 2024, baada ya nahodha huyo mwenye umri wa miaka 37, kuisaidia timu yake kupata medali ya shaba kwenye Kombe la Dunia kwa kushika nafasi tatu.

**Hiyo inaweza kumaanisha Modric atasalia katikati ya safu ya kiungo ya Croatia kwenye Euro 2024, wakati huo atakuwa anakaribia kutimiza umri wa miaka 39.**

Mchezaji huyo wa Real Madrid Modric hatazamii mbele sana kwa sasa, lakini bado anaweza kuichezea Croatia kwenye mashindano makubwa yajayo.

Hatua ya kwanza kwa Modric itakuwa kuelekea Fainali za Ligi ya Mataifa ya Uefa nchini Uholanzi mwakani, huku Croatia ikijiunga na wenyeji, Italia na Hispania katika mchuano huo wa timu nne.

Akiwa amefurahishwa na medali nyingine ya Kombe la Dunia, baada ya kushinda medali ya fedha miaka minne iliyopita nchini Urusi waliposhika nafasi ya pili, Modric aliiambia beIN SPORTS: "Medali hii ni muhimu sana kwetu, kwangu, kwa Croatia kama timu ya taifa na kama nchi.

"Tunathibitisha kwa medali hii kwamba Croatia ina jukumu muhimu katika ulimwengu wa soka na tunaiacha Qatar kama washindi.

"Kuhusu mustakabali wangu, sijui kama nitakuwa kwenye michuano ya Euro nchini Ujerumani. Nahitaji kwenda hatua kwa hatua.

"Ninaifurahia timu ya taifa, najisikia furaha, bado nadhani naweza kucheza kwa kiwango cha juu na ninataka kuendelea angalau hadi Ligi ya Mataifa ya Uefa na kisha kutakuwa na muda zaidi wa kufikiria kuhusu Euro."

Kulikuwa na wasiwasi katika baadhi ya maeneo kwamba Modric angestaafu soka la kimataifa baada ya Kombe la Dunia, lakini kocha Zlatko Dalic alionyesha matumaini kwamba angecheza hadi fainali za Ulaya za 2024 nchini Ujerumani.

Sasa baada ya ushindi wa 2-1 Jumamosi dhidi ya Morocco katika mchujo wa kuwania nafasi ya tatu, matakwa ya Dalic yanakaribia kutimia.

Croatia wana Wales, Armenia, Uturuki na Latvia katika kundi lao la kufuzu Euro 2024, na wangependelea sana kupitia hilo na kutinga fainali.

Inabaki kuonekana kama Dejan Lovren atacheza, huku beki huyo wa kati mwenye umri wa miaka 33, akiwa amesalia na kufikiria kufanya kuhusu mustakabali wake.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI

PYRAMIDS
VERSUS
ASWAN

1 | 1.61
X | 3.40
2 | 6.40

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# VAN NISTELROOY KUMRUHUSU GAKPO KUONDOKA JANUARI



**AMSTERDAM, Uholanzi**

KOCHA Mkuu wa PSV, Ruud van Nistelrooy, amekubali kwamba, fowadi anayehitajika sana, Cody Gakpo, huenda akaondoka katika klabu hiyo katika dirisha la usajili la Januari.

Gakpo amekuwa akihusishwa na Klabu za Real Madrid, Manchester United, Bayern Munich na Liverpool baada ya kuonyesha kiwango kizuri akiwa Qatar 2022 na Timu ya Taifa ya Uholanzi.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, amekuwa mchezaji wa pili katika historia ya Kombe la Dunia, baada ya Alessandro Altobelli wa Italia mwaka 1986, kufunga mabao katika michezo yote mitatu kwenye hatua moja ya makundi.

Alishindwa kuzifumania nyavu katika hatua ya mtoano dhidi ya Marekani na Argentina, huku Uholanzi ikitolewa kwa mikwaju ya penalti katika hatua ya robo fainali.

Mkurugenzi wa Soka wa PSV, Marcel Brands, majuzi alisema kwamba ada ya mchezaji huyo itakuwa rekodi na Van Nistelrooy hatamzuia Gakpo iwapo atataka kuondoka.

"Nilifurahia kumtazama (nchini Qatar). Anastahili hii kwa sababu amekuwa kwenye kiwango bora," alisema Van Nistelrooy akiiambia Voetbal International.

"Niliweza kumsaidia kutoka karibu sana na hiyo inanifanya nijivunie. Na kisha nitampa njia yake itakapofika."

Gakpo anajivunia mabao 17 na asisti nane katika michezo 31 msimu huu.

Akizungumza wakati akiwa kwenye Kombe la Dunia, Gakpo alisema "atafikiria" ofa yoyote itakayowasili kutoka kwa Manchester United, ambayo ilionyesha nia mapema mwaka huu.

# Allegri hajui Pogba atarudi lini dimbani

**TURIN, Italia**

KOCHA Mkuu wa Juventus, Massimiliano Allegri, amekiri kuwa hana uhakika ni lini Paul Pogba atarejea kutoka chumba cha majeruhi.

Pogba bado hajaichezea klabu hiyo kwa mara ya kwanza baada ya kurejea Turin kwa uhamisho wa bila malipo kabla ya kuanza kwa msimu huu, akiuguza jeraha la goti katika mechi za kujiandaa na msimu mpya ambalo pia lilimfanya kukosa kuichezea Ufaransa kwenye Kombe la Dunia.

Kiungo huyo wa zamani wa Manchester United awali alitarajiwa kurejea kwa ajili ya mechi dhidi ya viongozi wa Serie A, Napoli Januari 13, mwaka huu, lakini kurejea huko kwa sasa kunaripotiwa kuchelewa.



Allegri, akizungumza baada ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Arsenal kwenye Uwanja wa Emirates Jumamosi katika mchezo wa kirafiki, hakuweka muda wa kurejea kwa Pogba na alisema wazi kuwa anataka kuepuka maswali zaidi kuhusu kupona kwake.

"Paul bado hajakuwa fiti katika mazoezi, kwa hiyo siwezi kusema ni lini atarejea," aliiambia Sky Sport Italia.

"Huu ndio ukweli na ni muhimu kusema hivyo, la sivyo kila siku tutapata maswali haya juu ya jinsi ya kupona kwa Pogba kunaendelea."

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# MESSI AIPA ARGENTINA

INATOKA UK. 32

di Maria kuwafanya Waargentina hao kuwa mbele kwa mabao 2-0 katika kipindi cha kwanza.

Messi alirejesha uongozi wao katika kipindi cha nyongeza, kabla ya Mbappe kuwashangaza Waamerika Kusini hao tena kwa mkwaju wa penalti na kumfanya kukamilisha hat-trick ya kwanza katika fainali ya Kombe la Dunia tangu 1966.

Mbappe sasa amefunga hat-trick ya kwanza kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Dunia na kuisaidia Ufaransa kwenda muda wa nyongeza, tangu Sir Geoff Hurst alipofanya hivyo mwaka 1966.

Argentina imetwaa ubingwa huo tangu 1986 wakati Ufaransa ilikuwa ikilenga kuwa timu ya tatu kutwaa kombe hilo mara mbili.

Ufaransa imekuwa timu ya kwanza kushindwa kupiga shuti hata moja katika kipindi cha kwanza cha fainali ya Kombe la Dunia, na kumlazimu Didier Deschamps kufanya mabadiliko ya kihistoria wakati Argentina wakiwa mbele kwa mabao 2-0.

Lakini pia Deschamps amekuwa kocha wa kwanza kubadilisha wachezaji wawili kabla ya muda wa mapumziko katika mechi ya Kombe la Dunia, huku mabingwa hao watetezi wakiwa kwenye kamba kwa kushindwa kuwa na jaribio la kulenga goli.

Ousmane Dembele na Olivier Giroud walitolewa nje baada ya dakika 41 pekee, huku Ufaransa ikiwa na mlima wa kupanda baada ya mkwaju wa penalti wa Messi na shuti la ajabu la Di Maria kuitanguliza Argentina.

Dembele alifanaya makosa kwa bao la kwanza la Argentina kwa kumwangusha Di Maria katika eneo la hatari kabla ya Messi kupachika bao lake la sita la michuano hiyo na la kwanza kwa Argentina katika mchezo huo, na Di Maria akaongeza la pili muda mfupi baadaye.

Huku Ufaransa wakiwa kwenye kasi, Deschamps alilazimika kuchukua hatua kwa kuwatoa Dembele na Giroud na kuwaingiza Randal Kolo Muani na Marcus Thuram.

Hata hivyo, uamuzi wa Deschamps kumtoa Giroud utakuwa gumzo kubwa, baada ya Kocha huyo Mkuu wa Ufaransa kukataa kumrejesha mshindi wa Ballon d'Or, Karim Benzema kwenye mechi hiyo ya fainali.

Benzema alilazimika kuwekwa kando kwenye michuano hiyo ya Qatar 2022 kutokana na jeraha la paja, lakini kulikuwa na maoni kwamba mshambuliaji huyo wa Real Madrid anaweza kuungana na kikosi kwa ajili ya fainali jana Jumapili.

Lakini Deschamps hakumpigia simu Benzema, ambaye aliandika ujumbe wenye utata kwenye mitandao ya kijamii siku zilizofuata ambao ulitafsiriwa kama "Sipendezwi".

Deschamps alichagua kumwanzisha Giroud licha ya mchezaji huyo wa Milan kuhangaika na jeraha siku chache kabla ya fainali.

Mbali na Argentina kutwaa ubingwa huo, Messi alitangazwa kuwa mchezaji bora wa michuano hiyo huku Mbappe akitwaa Kiatu cha Dhahabu kwa kuibuka mfungaji bora wakati kipa Martinez akibeba tuzo ya kipa bora wakati Enzo Fernandez akiondoka na tuzo ya mchezaji bora kinda.

# SIMBA YAFIKIA REKODI YAKE

INATOKA UK. 32

Matokeo hayo yameipeleka kwenye nafasi ya pili iliyokuwa ikikaliwa na Azam FC kwa siku za hivi karibuni ambayo imesukumwa hadi nafasi ya tatu.

Imefikisha pointi 37, mabao 36 ikiwa timu iliyofunga mabao mengi zaidi kwenye ligi, huku ikiruhusu wavu wake kuguswa mara saba tu, ikiwa pia ni timu iliyoruhusu mabao machache zaidi. Geita Gold imebaki kwenye nafasi ya saba na pointi zake 22.

Mechi ilianza kwa kasi, huku Simba ikifanya mashambulizi kadhaa langoni mwa wapinzani wao jambo lililowalazimu kucheza kwa tahadhari kubwa dakika za mwanzo.

Ilikuwa ni dakika ya tisa Bocco alipopata pasi ya kichwa kutoka kwa Mosses Phri, lakini wakati anataka kupiga shuti alianguka na mabeki wa Geita Gold wakaufagia mpira huo.

Dakika moja baadaye, Juma Luzio alipiga shuti dhaifu akiwa amebaki na kipa Aishi Manula.

Baada ya kosakosa nyingi, Simba ilifanikiwa kuandika bao la kwanza dakika ya 11, Bocco akiruka juu na kuupiga kichwa mpira wa krosi iliyotoka winga ya kulia kwa Shomari Kapombe, ukajaa ndani ya wavu na kumuacha kipa Mac Arthur Arakaza akinyoosha mikono bila mafanikio.

Luzio kwa mara nyingine tena aliikosesha Geita Gold bao, kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Yusuph Kagoma aliyewazidi mbio mabeki wa Simba, akamimina majalo iliyoguswa kidogo na Joash Onyango ukamkuta mchezaji huyo aliyepiga shuti lililokwenda juu ya lango.

Bao la pili la washindi lilifungwa dakika sita kabla ya kwenda mapumziko na Chama ambalo lilianzia kwa pasi mzunguko na mpenyezo kutoka kwa Moses Phiri, Mzamiru Yassin na mfungaji mwenyewe.

Chama aliiruka pasi ya Phiri akatangulia mbele, mpira ukaenda kwa Mzamiru ambaye moja kwa moja aliupeleka mbele alipo mfungaji.

Kwa utulivu wa hali ya juu akiwa ndani ya eneo la hatari, aliwageuza mabeki wa Geita Gold na kutishia kama anapiga upande wa kushoto kwa kipa, lakini akapiga shuti dhaifu upande wa kulia ukimpita tobo pia mlinzi wa timu hiyo na kujaa wavuni.

Dakika ya pili tu baada ya mapumziko, Sakho aliandika bao la tatu kwa shuti kali, baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Chama pamoja na Bocco kuwanyang'anya mpira mabeki wa Geita Gold.

Chama aliunyang'anya mpira akampa Bocco aliyerudisha tena kwa mtoa pasi ya bao, kabla ya Sakho kuujaza wavuni.

Luzio kwa mara nyingi alikaribia kuifungia Geita Gold bao alipopata pasi kutoka kwa Danny Lyanga, lakini shuti kali liligonga nguzo ya pembeni kabla ya kuokolewa na Onyango.

Sakho tena dakika ya 74 alipachika mpira wavuni kwa shuti kali la mbali. Ni baada ya kipa Arakaza raia wa Burundi kujitosa kuokoa kwa ustadi shuti la Chama aliyekuwa akitaka kufunga, lakini mpira aliouokoa ulimkuta mfungaji akiwa mita takribani 35 akapiga shuti la kunyooka lililokwenda moja kwa moja wavuni, huku juhudi za kipa huyo zikiishia kujigonga kwenye mlingoti wa lango kiasi cha kushindwa kuendelea na nafasi yake ikachukuliwa na Sebusebu Samson.

Timu zote zilifanya mabadiliko kadhaa, lakini ni Simba iliyonufaika nayo kwa Kibu aliyeingia kipindi cha pili kupachika bao la tano dakika moja kabla mechi haijamalizika, akipata pasi mpenyezo kutoka kwa kinara wa pasi za mwisho kwenye Ligi Kuu, Chama ambaye alikuwa anafikisha 'assist' ya tisa.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 19/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3373 | Khosheh Talaei vs Saipa Karadj | 2.81 | 2.62 | 2.76 |
| 13:30 | 3630 | Chooka Talesh FC vs Chador Malu Yazd | 3.35 | 2.80 | 2.43 |
| 13:30 | 4398 | Arman Gohar Sirjan vs Vanpars | 2.07 | 2.86 | 3.74 |
| 13:30 | 5145 | Fajr Sepasi vs Shahrdari Astara | 1.61 | 3.32 | 5.66 |
| 13:45 | 2710 | Esteghlal Mollasani vs Mes Shahr-e Babak | 2.43 | 2.53 | 3.41 |
| 13:45 | 4929 | Shahrdari Hamedan vs Pars Jonoubi Jam | 3.20 | 2.38 | 2.72 |
| 14:00 | 3200 | PSM Makassar vs Psis Semarang | 2.38 | 2.87 | 3.01 |
| 14:00 | 5132 | Diagoras FC vs Apollon Larisas | 1.37 | 4.29 | 7.21 |
| 14:00 | 5532 | SC Farense U23 vs Portimonense U23 | 2.19 | 3.80 | 2.63 |
| 14:30 | 2080 | Nassaji Mazandaran vs Sanat Naft Abadan | 2.03 | 2.77 | 4.08 |
| 14:30 | 5018 | Sanat Mes Kerman FC vs MES Rafsanjan | 3.50 | 2.65 | 2.44 |
| 14:30 | 5233 | Malavan Bandar Anzali vs Sepahan Esfahan | 5.26 | 3.16 | 1.68 |
| 15:05 | 3634 | AL Qaisoma vs Najran SC | 2.26 | 2.82 | 3.31 |
| 15:25 | 5107 | Al Orubah vs Jeddah Club | 2.36 | 2.77 | 3.16 |
| 15:45 | 2483 | Al Nasr Dubai vs Dibba Al Fujairah | 1.46 | 4.09 | 5.84 |
| 15:45 | 3939 | FC Veria vs Panserraikos | 6.62 | 3.60 | 1.49 |
| 15:45 | 4291 | Anagennisi Karditsas vs Thesprotos | 1.16 | 6.01 | 13.57 |
| 15:45 | 4684 | Ceramica Cleopatra vs El Daklyeh | 1.89 | 3.15 | 4.40 |
| 15:45 | 4966 | Apollon 1926 vs Almopos Arideas | 2.08 | 3.02 | 3.46 |
| 15:45 | 5183 | PAO Rouf vs Panachaiki | 7.76 | 4.27 | 1.36 |
| 15:45 | 5881 | Al Dhafra vs Ajman Club | 3.21 | 3.40 | 2.02 |
| 16:00 | 3101 | AL Nasr vs AL Sahel | 2.31 | 3.26 | 2.78 |
| 16:00 | 4962 | Bahir Dar Kenema FC vs Mekelakeya | 2.12 | 2.77 | 3.74 |
| 16:15 | 1092 | Kallithea FC vs Olympiacos Piraeus B | 1.52 | 3.69 | 5.82 |
| 16:15 | 3953 | Bali Utd Pusam vs PSS Sleman | 1.47 | 4.10 | 5.66 |
| 16:30 | 1808 | Zob Ahan vs Aluminium Arak | 2.50 | 2.60 | 3.18 |
| 16:30 | 3957 | Gol Gohar vs Havadar | 1.84 | 3.10 | 4.90 |
| 17:00 | 1345 | Chennaiyin FC vs Kerala Blasters FC | 3.01 | 3.44 | 2.10 |
| 17:50 | 1167 | Al Faisaly (KSA) vs AL Hazm | 2.27 | 2.90 | 3.50 |
| 18:00 | 1339 | Smouha Club vs El Ittihad Alexandria | 3.04 | 2.84 | 2.54 |
| 18:00 | 4115 | Coca Cola vs Ghazl EL Mahallah | 1.64 | 3.48 | 5.58 |
| 18:30 | 1552 | LYS Sassandra vs Asi D Abengourou | 1.88 | 2.86 | 4.56 |
| 18:30 | 2142 | Sporting Gagnoa vs Denguele Sport | 2.13 | 2.78 | 3.71 |
| 18:30 | 3583 | Al Wasl Dubai vs Shabab AL Ahli Dubai Club | 2.82 | 3.41 | 2.21 |
| 18:30 | 5711 | AL Bataeh (UAE) vs Jazira Abu Dhabi | 6.46 | 4.89 | 1.35 |
| 18:40 | 2200 | Kazma SC vs Al Jahra | 1.48 | 4.20 | 6.20 |
| 19:00 | 4850 | Ethiopia Electricity vs Hadiya Hosahina FC | 3.79 | 2.97 | 2.00 |
| 20:00 | 2498 | Karmiotissa vs Pafos FC | 5.81 | 4.01 | 1.54 |
| 20:00 | 3416 | Adanaspor vs Denizlispor | 1.62 | 3.79 | 4.56 |
| 20:00 | 4332 | Pyramids vs Aswan | 1.61 | 3.40 | 6.40 |
| 20:00 | 4599 | SC Kfar Qasem vs Hapoel Ramat Gan | 2.13 | 3.10 | 3.60 |
| 20:00 | 4668 | Ironi Kiryat Shmona vs Sectzya Nes Ziona | 1.94 | 3.35 | 3.49 |
| 20:00 | 5789 | Maccabi Jaffa vs Hapoel Rishon Lezion | 2.36 | 3.10 | 3.10 |
| 21:00 | 4961 | Steaua Bucuresti vs Botosani | 1.43 | 4.26 | 6.93 |
| 21:15 | 1302 | Maccabi Bney Reine vs Maccabi Tel Aviv | 9.35 | 5.07 | 1.26 |
| 21:30 | 2678 | Maccabi Haifa vs Bnei Sakhnin | 1.22 | 5.65 | 9.75 |
| 22:30 | 2708 | Usd Audace Cerignola vs Juve Stabia | 2.10 | 3.05 | 3.75 |
| 22:30 | 4323 | Perugia vs Venezia | 2.41 | 3.03 | 2.98 |
| 23:00 | 1764 | Leganes vs Zaragoza | 2.43 | 2.83 | 3.17 |
| 23:00 | 4844 | Wigan vs Sheffield Utd | 3.66 | 3.32 | 1.98 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Desemba 19, 2022

Nipashe




UKURASA 29

**Modric: Bado naweza kucheza hadi Euro 2024**



# MESSI AIPA ARGENTINA KOMBE LA DUNIA 2022

●●●Mbappe atwaa Kiatu cha Dhahabu, Messi mchezaji bora, Martinez kipa bora, rekodi kibao zaandikwa huku....

**Lusail, Qatar**

Lionel Messi ameiongoza Argentina kutwaa Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar jana baada ya kuifunga Ufaransa kwa mikwaju ya penalti katika fainali ya kihistoria.

Gonzalo Montiel ndiye alihitimisha ubingwa huo kwa Argentina baada ya kufunga mkwaju wa penalti na kufanikisha Argentina kushinda kwa mikwaju 4-2 katika mechi hiyo ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Lusail nchini Qatar jana.

Hata hivyo, kipa Emiliano Martinez, alifanya kazi ya kupongezwa kwa kuokoa mkwaju wa Kingsley Coman.

Penalti za Argentina zilifungwa na Messi, Paulo Dybala, Leandro Paredes na Gonzalo Montiel huku mbili za Ufaransa zikifungwa na Kylian Mbappe na Randal Kolo Muani wakati Coman na Aurelien Tchouameni wakikosa.

Argentina ilionekana ingeweza kupoteza kombe hilo, baada ya Mbappe kufunga mabao mawili katika dakika 10 za mwisho na kusababisha timu hizo kumaliza dakika 90 matokeo yakiwa 2-2, hivyo kwenda muda wa nyongeza, hiyo ikiwa ni baada ya mkwaju wa penalti wa Messi na bao la Angel

INAENDELEA UK. 31

# Simba yafikia rekodi yake

**Na Adam Fungamwango**

MABAO yaliyofungwa na nahodha John Bocco, Clatous Chama, Pape Sakho (mawili) na mchezaji aliyetokea benchi, Kibu Denis, yameiwezesha Simba kuipiga Geita Gold 'mkono' 5-0, katika mechi iliyochezwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza jana.

Bocco na Sakho wanafikisha mabao matano kila moja kwenye orodha ya wafungaji Ligi Kuu Tanzania Bara huku Chama aliyefunga bao moja na kutoa pasi za mabao mbili katika mchezo huo, akifikisha mabao matatu na 'assist' tisa wakati Kibu ndiyo kwanza akiwa amefungua akaunti yake ya mabao msimu huu.

Ni ushindi wa pili mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, baada ya ule ambao Simba yenyewe iliupata Oktoba 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikiifunga Mtibwa Sugar mabao 5-0. Hakuna timu nyingine iliyoshinda kwa idadi kubwa ya mabao hayo kwenye ligi mpaka sasa.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >